**26 MEI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 26 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha Thelathini na Nne.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu ninamwita Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe aulize swali lake.

Na. 439

**Kuhakikisha pesheni zinalipwa kwa wakati**

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha pesheni za wastaafu zinalipwa kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Mheshimiwa Patrobas Katambi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwneyekiti, pensheni ni mafao wanayolipwa wanachama waliostaafu kwa kila mwezi katika kipindi chote cha maisha yao. Katika kuhakikisha wastaafu wanalipwa pensheni zao kwa wakati, Serikali kupitia Mifuko ya Pensheni ya *PSSSF* na *NSSF* imeweka utaratibu mahsusi wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki kupitia kwenye akaunti zao za benki kila au ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 idadi ya wastaafu wanaolipwa pensheni katika Mifuko ya *PSSSF* na *NSSF* imefikia

186,605 ikijumuisha *PSSSF* wastaafu 158,735 na *NSSF* wastaafu 27,870.

Mheshimiwa Mwneyekiti, mifuko inaendelea kuimarisha mifumo ya ndani ya ulipaji wa mafao ili kuhakikisha maombi ya wastaafu wapya yanafanyiwa kazi kwa haraka na kuanza kulipwa pensheni ndani ya kipindi kisichozidi siku 60 kama sheria inavyotaka, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemus Maganga swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza niseme kabisa Mheshimiwa Waziri sijaridhishwa na majibu haya, hii takwimu uliyoionesha hapa kwamba bado wastaafu 1,780 hawajalipwa lakini niende kwenye maswali mawili labda nitaridhika.

Sasa Mheshimiwa Waziri mnawatambuaje wastaafu ambao walistaafu miaka mingi wakahamia wengine vijijini, hawako kwenye mifumo hii ya kieletroniki na umesema wanafanyiwa uhakiki kuwatambua kupitia akaunti zao tayari wengine walishafungiwa na akaunti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; hauoni ni kumweka mtu kwenye mazingira magumu sana ambaye anaitumikia Serikali wakati wake unapofika wa kustaafu halafu zinaanza chenga za kumlipa mafao yake.

Je, ungekuwa ni wewe ukamaliza Ubunge wako halafu mafao yasipatikane ungefikiriaje Mheshimiwa Waziri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali na anasema hajaridhika na majibu, lakini takwimu sahihi za Serikali chini ya mifuko na hizo kwamba wastaafu ambao wanalipwa ni hao 186,605 na kama ana takwimu tofauti basi tunamkaribisha ili tuweze kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusiana na suala la wastaafu ambao wako vijijini anasema masuala ya mtandao na kadhalika. Hao wanaendelea kuhudumiwa, katika ofisi zetu zote za mifuko na wanachama wale wamefunguliwa na hawa niliowataja wote wana akaunti hizo za benki na bado kuna *desk* ambalo linawahudumia wastaafu wetu na tumeajiri watu maalum kabisa wa kutoa huduma hiyo kwa wateja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama ana jambo mahususi haliwezi kuwa la watu wote ni la hao watu wachache ambao anawasema na kama wapo anifikishie ili niweze kuchukua hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kuhusiana na kwamba ucheleweshaji wa ulipaji wa mafao, imebaki kuwa historia, tumeshafanya mabadiliko sasa hivi tunalipa kieletroniki na kuhusiana na mafao kama ni ulipaji kila mwezi kabla ya tarehe 25 tunalipa fedha hizo. Kwa hiyo, hilo ni suala la kihisroria analolielezea sasa hivi tumefanya mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwaagiza Wakurugenzi na Mameneja wote wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika Mikoa waendelee kusimamia na kufanya lile suala la *compliance* kufatilia michango ya wanachama, lakini pili kuendelea kuhakikisha kwamba hakuna mstaafu

yoyote ambaye anapata shida katika kipindi hiki, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI namwita Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni aulize swali lake, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mtemvu.

Na. 440

**Kuanza Mradi wa *DMDP* Awamu ya II- Kigamboni**

**MHE. ISSA J. MTEMVU K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili utaanza kwa lengo la kutatua changamoto ya miundombinu Kigamboni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili kupitia mkopo wa Benki ya Dunia unatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2024 na utahusisha ujenzi wa miundombinu ya barabara, mifereji ya maji ya mvua pamoja na madaraja. Kwa sasa mradi upo katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu. Hatua hiyo itakapokamilika, ombi la fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo litawasilishwa Benki ya Dunia.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza nipongeze sana majibu ya Serikali na nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Mawaziri wa Fedha, TAMISEMI na Ujenzi kwa kuendelea kuchakata jambo hili liende vizuri katika mchakato huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza; kwa sababu Serikali ipo katika hatua za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina maana yake tayari imeshafanya utambuzi wa barabara zote zitakazoingia kwenye mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili.

Je, ni barabara zipi ndani ya Jimbo la Kibamba ambazo na zenyewe zitakuwa sehemu ya mradi huu *DMDP* Awamu ya Pili?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, namna mradi huu ulivyokuwa *design* kwamba kila Halmashauri katika Mkoa wa Dar es Salaam imewasilisha mapendekezo ya barabara ambazo zitatakiwa kufanyiwa ukarabati kupitia mradi huu wa *DMDP II.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumjulisha Mheshimiwa Mtemvu na Wabunge wote wa Dar es Salaam kwamba kwa maelekezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Anjela Kairuki wiki ijayo mtaitwa wote Waheshimiwa Wabunge wa Jiji la Dar es Salaam ili kushuhudia utiaji saini wa mradi huu wa *consultancy* ambazo anaenda ku-*design* barabara zetu hizi.

Kwa hiyo, nimtoe hofu ni barabara zote kama walivyoziwalisha wao katika halmashauri zao ambazo zitawekwa katika mradi huu.

**MWENYEKITI:** Sijaona aliyeomba kuuliza swali la nyongeza, kwa hiyo, tunaendelea namwita Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge ya Kyerwa aulize swali lake.

Na. 441

**Kujenga lami nyepesi *Mabira Station* Wilaya ya Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kujenga kilometa moja ya lami nyepesi *Mabira Station* ili kuboresha mazingira mazuri kwa wafanyabiashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga bajeti ya ujenzi na matengenezo ya barabara hiyo ambapo katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 shilingi milioni 117.14 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa kilometa saba za barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, shilingi milioni 83.1 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa kilometa nne kwa kiwango cha changarawe na ujenzi umekamilika.

Vilevile katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, barabara ya *Mabira Station* imetengewa shilingi milioni 47.6 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga kilometa moja ya lami nyepesi *Mabira Station* kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuboresha mazingira mazuri kwa wafanyabiashara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naishukuru Serikali kwa majibu angalau yenye matumaini.

Swali langu la kwanza; barabara ya Rulama - Kanyantama - Ruita mpaka Mabira barabara hii inaunganisha kata nne; Kata ya Kibale, Businde, Kamuli mpaka Mabira na inaunganisha Tarafa mbili na ni muhimu sana kuna wakulima wengi. Ni lini barabara hii itatengewa fedha iweze kutengenezwa ili iweze kupitika kipindi chote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini barabara ya Nkwenda mpaka Mabira itapandishwa hadhi iwe chini ya *TANROADS* kwa sababu inahitaji fedha nyingi na ni muhimu sana kwa wananchi wa Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bilakwate, kwanza nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako tukufu kumwarifu Mheshimiwa Bilakwate kwamba ombi lake kama mwakilishi wa Wanakyerwa la fedha kwa ajili ya barabara ya Kasoni - Mkuyu tayari pesa hiyo imepatikana na muda si mrefu Mheshimiwa Mbunge mkandarasi

atapatikana ili kuingia *site* na kuanza ujenzi wa barabara hii kama alivyokuwa ameiomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye maswali yake; hii barabara ya Ruhama – Kanywaa – Ntama - Ruhita ambayo inaunga kata nyingine na Kata ya Mabira tayari andiko lilikuwa limewasilishwa na Meneja wa *TARURA* katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa na Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Kagera lilishawasilishwa Makao Makuu ya *TARURA* na walikuwa wameomba shilingi milioni 700 kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri ya upatikanaji wa fedha *TARURA* itapeleka fedha katika Mkoa wa Kagera kwa ajili ya utengenezaji wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili barabara ya Nkwenda inayokwenda Mabira kupandishwa hadhi na kuwa barabara ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kisheria ziko wazi, ni lazima wao wenyewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa waanze na vikao vyao ikiwemo *DCC* ikitoka *DCC* waipeleke katika *RCC* halafu kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa na baada ya Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wanawasilisha ombi lile kwenda kwa Waziri mwenye dhamana ya barabara yaani Waziri wa Ujenzi ndipo barabara hiyo iweze kupandishwa hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi naomba niwaase waanze mchakato huo kwa ajili ya kuwasilisha kwenda kwa Waziri wa Ujenzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na namwita Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 442

**Hitaji la watumishi wa afya Hospitali ya Wilaya - Meatu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza watumishi wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali iliajiri watumishi 7, 736 wa Afya na Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ilipangiwa watumishi 104 na watumishi saba walipangwa Hospitali ya Halmashuri ya Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2022/2223, Serikali itaajiri watumishi wa kada ya afya 8,070. Aidha, baada ya taratibu za ajira kukamilika watumishi hao watapangwa kwenye Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Meatu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mafupi, Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanste na nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; katika Wilaya ya Meatu kuna vituo vya afya ambavyo vimefunguliwa viwili Iramba Ndogo pamoja na Mwasengela. Iramba ndogo ina wafanyakazi watatu; mmoja ni mganga na wawili ni wauguzi, kwa hiyo hawatoshi kabisa, lakini katika Kituo cha Afya cha Mwasengela chenyewe hakina kabisa watumishi wa afya na kinategemewa kufunguliwa tarehe 1 Julai; naomba majibu ya Serikali kuhusu wafanyakazi katika vituo hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani swali la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili liko katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa; Hospitali ya Maswa ni kubwa sana lakini watumishi hawatoshi, naomba nipate jibu la uhakika kwamba ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa maswali mawili ya msingi ya muuliza swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Minza, la kwanza la Iramba Ndogo kupata watumishi wa ziada na Mwasengela; niseme tu kama nilivyokwishakutoa maelezo kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Serikali inaajiri watumishi wa afya 8,070 na katika hawa tutapanga kwanza kwenye maeneo yale yenye upungufu mkubwa ikiwemo Iramba Ndogo, lakini vilevile kwa sababu kituo hiki cha Mwasengela ni kituo kipya ambacho

kinaenda kufunguliwa tarehe 1 Julai na kama sikosei kipo Kisesa, tutahakikisha hizi ajira mpya kwa sababu wataingia kazini mwaka huu wa fedha ambao tunautekeleza sasa na tarehe 1 Julai ni mwaka ule mwingine wa fedha, tayari kituo hichi kinapofunguliwa watumishi hawa wa afya watakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda tu kwenye hili alilogusia la Hospitali ya Wilaya ya Maswa vilevile kwenye hizi ajira tutapeleka maeneo ambayo yana upungufu mkubwa ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Maswa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona maswali ya nyongeza yako mengi, lakini swali la msingi linazungumzia watumishi katika hospitali. Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na ukubwa wa jiografia wa Wilaya ya Hanang; je, ni lini Serikali itaongeza watumishi wa afya katika Hospitali ya Wilaya pamoja na vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halamga kuhusu Hanang na vituo vya afya, zahanati, hospitali ya wilaya na vituo vya afya ambavyo vina upungufu wa watumishi, kama nilivyokwishakusema kwenye majibu yangu ya msingi katika ajira hizi zilizotangazwa na Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu ajira 8,070 nitahakikisha pia Hanang wanapata watumishi wa afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu ameshajibu kwa ujumla kuhusiana na watumishi kwenye sekta ya afya, nadhani majibu tumeshayapata. Namwita Mheshimiwa Deo Mwanyika aulize swali lake la nyongeza.

**MHE: DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi linaendana na vifaa tiba. Njombe tuna vituo vya afya viwili vimejegwa kwa nguvu za wananchi na mapato ya ndani. Watumishi wameshapelekwa tunashukuru Serikali, lakini watumishi hao sasa ni kama hawana kazi kwa sababu vifaa tiba havijapelekwa.

Sasa swali langu, Serikali haioni ni busara kuhakikisha kwamba pale ambapo watumishi wamepelekwa, lakini vifaa tiba havijaenda basi wakafanya haraka kupeleka vifaa tiba ili watumishi hao sasa wafanye kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanyika la vifaa tiba, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Njombe kwa kujenga kwa nguvu zao wenyewe vituo hivi vya afya na vilevile Halmashauri ya Mji kwa kujenga pia kwa kupitia mapato yao ya ndani na hili ndio tunatamani kuliona kila Halmashauri ikitenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kusaidia wananchi katika sekta ya afya na sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la vifaa tiba ni kipaumbele cha Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha vifaa tiba vya kisasa vinakwenda katika maeneo

yote nchini ikiwemo kule Wilayani Njombe na tutakaa na Mheshimiwa Mbunge na kuangalia kwenye bajeti iliyotengwa ni kiasi gani kimetengwa kwa jaili ya vifaa tiba na hiyo fedha iliyokuwepo basi vifaa tiba hivyo viweze kupataikana mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Kata ya Soya, Wilaya ya Chemba tulijengewa na wafadhili, kuna baadhi ya vifaa tiba vipo na baadhi havipo ikiwemo *x–ray machine*, lakini na watumishi mpaka leo kituo kimekamilika tangu mwaka jana. Hivyo vifaa tiba havijakamilika na watumishi hatuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatupelekea vifaa tiba pamoja na watumishi ili hospitali kwa maana ya kituo cha afya hicho kiweze kufanyaa kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Afya cha Kata ya Soya, Wilayani Chemba Serikali itapeleka watumishi, katika hawa watumishi wanaoajiriwa kama nilivyokwisha sema katika majibu yangu ya msingi na kwenye vifaa tiba tutaangalia kwenye bajeti iliyotengwa ni kiasi gani inatakiwa kwa ajili ya kwenda kununua hivi vifaa kama *x–ray* na vinginevyo basi Serikali iweze kupeleka fedha hizo na vifaa hivi viweze kununuliwa na wananchi wa Soya waweze kupata huduma hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wimbi kubwa la kuhama watumishi kwenye Idara ya Afya kwenye Halmashauri hasa zile za pembezoni. Mfano Liwale tulipata watumishi 80 lakini watumishi wale leo ukienda kuwahesabu hata 15 hawafiki, wanahama 36 wanahamia wawili; je, Serikali ina mpango gani kudhibiti huo uhamaji wa watumishi holela?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo ananiuliza Mheshimiwa Kuchauka Serikali imelitambua na tayari tunaweka mikakati hasa kwenye ajira hizi ambazo wanaingia kazini muda siyo mrefu, kuona tutaweka mikakati ambayo itadhibiti hili la watu kuhama. Lakini pia nichukue nafasi hii kuwaeleza Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ndio waajiri katika maeneo haya wahakikishe hawapitishi barua za watumishi ambao hawajathibitishwa kazini. Mtumishi anatakiwa walau akae miaka mitatu katika kituo chake kipya cha ajira, kwa hiyo, wafuate taratibu hizi, wasipitishe barua hizi ili watumishi hawa maana yake wameajiriwa kwenda kujaza upungufu ule ambao upo katika maeneo hayo. Sasa wanapopitisha barua hizi ili hawa wahame tayari wanazidisha upungufu katika maeneo haya.

Kwa hiyo, niliona nichukue muda kulizungumzia hili hapa ndani ili Wakurugenzi wetu wa Halmashauri ambao ni waajiri waweze kuelewa kufuata taratibu hizi za kiutumishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, je, Serikali haioni haja ya kuweka kipaumbele kuongeza watumishi wa afya kwenye Halmashauri mpya ikiwepo Halmashauri ya Mji wa Nanyamba pamoja na Newala Vijijijni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa Hokororo, ni kweli tunaona haja ya kuongeza watumishi hasa katika Halmashauri hizi mpya kama ya Nanyamba na ndiyo maana Serikali ilitenga bajeti katika mwaka huu wa fedha kuajiri watumishi 21,390 nchi nzima katika sekta ya elimu na afya, kwa ajili ya kupeleka katika maeneo yenye uhitaji mkubwa kama Halmashauri ya Nanyamba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Naibu Waziri wa Afya alitembelea Zahanati ya Kata ya Lemooti, Kijiji cha Lemooti, Wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha na kuwaahidi kuwa Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kumalizia miundombinu.

Je, ni lini sasa pesa hizo zitaenda ili kina mama wapate huduma ya uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupeleka fedha katika Zahanati hii ya Lemooti kule Wilayani Monduli, tutaangalia katika bajeti ambayo imepitishwa na Bunge lako tukufu ya mwaka 2023/2024 kuona ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa zahanati katika Wilaya ya Monduli ili iweze kuelekezwa katika Zahanati hii ya Lemooti na kama haikutengewa fedha, basi tutaangalia katika mwaka wa fedha 2024/2025 zahanati hii iweze kutengewa fedha.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza la mwisho kutoka kwa Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu yake mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya watumishi na mikakati ambayo ataiweka. Sasa swali langu ni kwamba je, mkakati gani wa ziada utakaouweka hasa kwa Mkoa wa Lindi kwa sababu suala la uhamaji wa watumishi ni kubwa sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga ni kama ambavyo nimetoa maelezo wakati namjibu Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale ambao wote wanatoka Mkoa wa Lindi na kweli Waheshimiwa Wabunge hawa wamekuwa wakilifuatilia sana suala hili Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha Mkoa wao unapata watumishi wa kutosha na watabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati ambao tumeuweka ni wa kuhakikisha wale wote walioomba ajira hizi, watambue kwanza tutawafahamisha wanapochukua barua zao za ajira

kwamba ajira hizi ni zimekwenda kujaza nafasi katika maeneo yenye upungufu mkubwa hapa nchini wa watumishi ili wahudumie Watanzania ikiwemo Mkoa wa Lindi. Hivyo basi itakuwa ni lazima atumikie nafasi hiyo katika eneo hilo ule muda ambao anatakiwa awe katika mtazamio *(probation period)* wa mwaka mmoja na baada ya hapo bado hatohama walau kwa miaka mingine miwili ina maana jumla inakuwa ni miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nirudie tena hapa kusema na kuongea na Wakurugenzi kupitia Bunge lako tukufu hili, wasipitishe barua ya mtumishi yeyote ambaye ni ajira mpya kwa sababu wakati anaomba ajira hiyo alitambua Serikali inafanya kazi kila pembe ya nchi yetu, na kwamba unapoomba kazi hiyo utapangiwa kwenda kuwatumikia Watanzania mahali popote nchini hapa. Kwa hiyo, wanapopewa barua za ajira waende wakatumikie Watanzania katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, namuita Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Maryam…

**MWENYEKITI:** Naomba ujitambulishe hilo swali ni Mheshimiwa nani?

Na. 443

**Uhakiki wanufaika wa *TASAF***

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID K.n.y. MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya uhakiki ili kuwarejesha walengwa 2,500 waliosimamishwa kupokea ruzuku ya *TASAF?*

**MWENYEKITI:** Haya, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, namuona Waziri mwenyewe yuko pale Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya *TASAF,* mwaka 2019 na 2021 Serikali iliagiza kufanyika uhakiki wa walengwa wote wa *TASAF* ili kupata taarifa sahihi ya walengwa wote waliomo katika kanzidata. Zoezi la uhakiki lilifanyika katika maeneo yote nchini na baadhi ya kaya zilibainika kukosa vigezo vya kuwa kwenye orodha ya walengwa na hivyo kusimamishwa kupokea ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaya ambazo zilithibitika kuwa na vigezo zimepewa nafasi ya kukata rufaa kwa mujibu wa sheria na taratibu na zilizobainika kuwa ni kweli zilikuwa na vigezo vya kuendelea kuwa kwenye mpango zilirejeshwa**.**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid kwa niaba ya Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba uhakiki umefanyika na wananchi hao wamesharejeshwa, lakini ni lini sasa watapatiwa malimbikizo yao ya ruzuku kutoka pale ambapo walisimamishwa na ukizingatia kwamba hasa hawa ambao walisimamishwa ni wanawake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makundi mawili; la kwanza ni wale ambao baada ya uhakiki walionekana wamekosa sifa na hawa ni 2,500 lakini wako ambao walipokosa sifa walikata rufaa wakarejeshwa, tutaangalia uwezekano wa kuanzia pale walipokuwa wamesimama au taratibu zinatakaje ili waweze kulipwa au wataendelea kuanzia hapa ambapo wamekuwa *cleared*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo la kulifanyia kazi, tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge muuliza swali Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi ili atuambie hasa ni wapi, lakini kimsingi Serikali ili wapembua kwa makundi hayo mawili na uamuzi huo ndio ulikuwa umefikiwa mpaka hatua za mwisho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kati ya waliopata sifa ni pamoja na wanawake na kaya nyinginezo za Mkoa wa Kilimanjaro ambao walipewa sasa ajira za muda, lakini baada ya kufanya ajira hizo vizuri hawajalipwa kwa vipindi viwili sasa.

Je, ni lini, Serikali itatoa malipo hayo ili malalamiko yaondoke katika mioyo yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyomgeza la Mheshimiwa Shally Raymond kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni taarifa na nimeisikia sasa kutoka kwake kwamba Mkoa wa Kilimanjarpo kuna wale ambao waliofanya kazi za *TASAF* za miradi ya kipindi maalumu na kwamba bado hawajalipwa basi acha tukalifanyie kazi halafu tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu.

Tunaendelea Wizara ya Mifugo namuita Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake na swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kwa niaba.

Na. 444

**Mpango wa kukomesha uvuvi haramu**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y. MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kukomesha uvuvi haramu wa kuvua samaki kwa kutumia nyavu zenye matundu madogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaboresha mfumo wa utoaji wa vibali vya kuingiza zana za uvuvi nchini ili kudhibiti uingizwaji wa zana haramu ikiwemo nyavu zenye matundu madogo na makokoro. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha shughuli za ukaguzi wa zana za uvuvi zinazoingizwa nchini kupitia njia za mipakani na bandarini kwa kuongeza idadi ya watumishi na vitendea kazi. Hili litaongeza wigo wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo ya mipakani na bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeandaa Mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kudhiti vitendo vya uvuvi haramu nchini. Utekelezaji wa mkakati huo utashirikisha viongozi wa ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mikoa ili kudhibiti matumizi ya zana haramu ikiwemo nyavu zenye matundu madogo, kokoro na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wavuvi, waingizaji na wasambazaji wa zana za uvuvi pamoja na jamii kwa ujumla kuhusu athari za matumizi ya zana haramu za uvuvi zikiwemo nyavu zenye matundu madogo, kokoro, timba, freemaya pamoja na matumizi ya vilipuzi katika uvuvi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema kuwa wawekezaji kuingiza hizi nyavu zilizo bora wanahamasisha; je, kuna mkakati gani wa Serikali wa kuhamasisha hawa wawekezaji wanaoleta hizi nyavu badala ya kuleta wakaanzisha viwanda hapa Tanzania vya kutengeneza hizi nyavu zinazotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mto Kilombero kuna wavuvi wanaovua sana sana kutoka Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi; je, kuna mpango gani wa kuhamasisha na kuwapatia nyavu bora za uvuvi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, je tumejipangaje kwenye kuhamasisha juu ya ujenzi wa viwanda vya nyavu hapa nchini? Jambo hili tayari linafanywa na tumekwisha kuanza kupata viwanda ambavyo vinatengeneza nyavu. Pale

Mwanza tunacho kiwanda kipya kinaitwa *Ziwa Net* ambacho kinatengeneza nyavu na kuwauzia wavuvi na tunayo maombi pia vilevile ambayo tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ajili ya uwekezaji kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni suala la zana kwa ajili ya wavuvi kwenye mto Kilombero. Jambo hili nimelichukua kama ombi la Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum na nitakwenda kuzungumza naye ili kuweza kuandaa wavuvi wa Mto Kilombero katika vikundi na baadae na wao ikiwezekana waweze kupata hizi zana kama ambavyo wanapata wavuvi wengine nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, namuita Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge aweze kuuliza swali lake.

Na. 445

**Kupeleka suluhisho la kudumu kwa wanyama waharibifu wa mazao**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatafuta suluhisho la kudumu la kudhibiti wanyama waharibifu wa mazao na ugonjwa wa mnyauko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge Nkenge wa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kila mwaka hutenga fedha kwa ajili ya kudhibiti makundi mbalimbali ya wanyama waharibifu wa mazao hususani panya, kweleakwelea, viwavijeshi na nzige.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, jumla ya shilingi bilioni 4.9 zimetolewa kwa ajili ya kudhibiti wanyama hao. Aidha Serikali inaendelea kuimarisha timu ya kusimamia kilimo anga ambapo ndege moja iliyokuwa mbovu imesharekebishwa na taratibu za kununua ndege mpya zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na ugonjwa wa mnyauko katika mazao mbalimbali ikiwemo ndizi, viazi, maharage na kahawa, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzalisha miche bora yenye ukinzani na magonjwa ya mnyauko; kutoa elimu kwa wakulima na Maafisa Ugani kuhusu kukata au kung'oa mashina yote yaliyoathirika na kuyachoma moto ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa na kuzalisha miche bora kutoka mashina yaliyoathirika kutumia teknolojia ya *tissue culture* ambayo inasaidia kusafisha na kuzalisha miche ambayo haitakuwa na ugonjwa huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali katika eneo ambalo imeongelea la kudhibiti kweleakwelea, viwavijeshi, nzige na wanyama wengine waharibifu, lakini katika eneo hilo suala la ngedere ni ngumu sana kulidhibiti kwa aina ya kupitia kilimo anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Missenyi imekuwa ni janga kubwa na sisi kama wananchi kupitia juhudi za Mbunge na Waheshimiwa Madiwani tulitafuta suluhisho la kununua dawa aina ya *carbofuran* ambayo inaua ngedere hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mchango wa Waheshimiwa Madiwani na Mbunge kununua dawa hiyo; je, Serikali haioni kuna haja ya ku–*support* juhudi hizo kuchangia hizo fedha au kuelekeza Halmashauri ikatenga bajeti kwa ajili ya kununua dawa hiyo ili wananchi sasa wakilima waweze kuvuna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Tunajua Serikali imefanya kazi kubwa katika kupambana na suala la mnyauko, lakini mpaka sasa hivi bado unaleta usumbufu katika maeneo yetu.

Je, ni hatua gani ambayo Serikali imefikia katika kufanya utafiti ili sasa tuweze kupata suluhisho la kudumu la ugonjwa wa mnyauko? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la kwanza la kuhusu dawa ambayo inatumika pale Missenyi nataka nichukue fursa hii kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya waende kuangalia dawa hiyo ambayo inatumika, na kama ina ufanisi sisi kama Serikali pia, tutaunga mkono kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu mkakati wa kudumu; kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, moja kati ya kazi kubwa ambayo tunaendelea kuifanya hivi sasa ni kuhakikisha kwanza kabisa tunang'oa na kuchoma moto mashina yale yote ambayo yalikuwa yana ugonjwa wa mnyauko ili ugonywa huu usisambae, lakini la pili, tunawajengea uwezo Kituo chetu cha Utafiti wa Kilimo cha *TARI* - Maruku, ili waweze kufanya utafiti na badae kuzalisha miche bora ambayo itakuwa na ukinzani na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi milioni 800; shilingi milioni 400 inakwenda kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa miche bora ya migomba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itakuja na mkakati wa uzalishaji miche kwa kutumia teknolojia ya chupa?

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi kabisa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu ya mwaka 2023/2024 zimetengwa shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuwajengea uwezo *TARI* – Maruku ili waweze kuanza teknolojia mpya ya uzalishaji wa miche safi kupitia *tissue*

*culture* ambayo itasaidia sana katika kutatua changamoto hii ya ugonjwa wa mnyauko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kitunguu linalolimwa sana Wilayani Kilolo limekumbwa na ugonjwa unaoitwa kaukau kwa lugha ya mtaani ambao haujulikani na vitunguu vinakauka mara tu vinapokuwa vimepandwa.

Je, Serikali iko tayari kutuma wataalamu ili kufanya uchunguzi na kutafuta suluhisho katika ugonjwa huu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa taarifa hii, Jumatatu wataalam kutoka Wizara ya Kilimo watakuwepo jimboni kwake kwa ajili ya kushughulikia tatizo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, namuita Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, aulize swali lake.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi, lakini kabla ya kuuliza swali naomba kufanya marekebisho kidogo, Kijiji cha Mdunduaro,

badala ya Mdunduaro tuandike Mtunduaro. Kijiji cha Mtunduaro sio Mdunduaro, hiki kiko Songea cha kwetu kinaitwa…

**MWENYEKITI:** Haya, uliza swali Mheshimiwa.

Na. 446

**Kuweka upya alama za Hifadhi – Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapitia upya mipaka na kuweka alama za Hifadhi katika Vijiji vya Ndongosi, Mtunduaro, Litumbandyosi na Kiwombi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Ndongosi, Mtunduaro, Litumbandyosi na Kiwombi vinapakana na Hifadhi ya Msitu wa Litumbandyosi katika Wilaya ya Mbinga. Kwa sasa Serikali inaendelea na utaratibu wa kuhakiki msitu huo wa Hifadhi wa Litumbandyosi kwa kuwashirikisha wananchi, baada ya kukamilika kwa uhakiki huo zitawekwa alama za mipaka zinazoonekana ili kuwezesha wananchi kutambua eneo la hifadhi na hivyo kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na kutokuwepo kwa mipaka inayoonekana wazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini niiombe uhakiki huu unaoshirikisha wananchi uhusishe pia Kijiji cha Chunya - Kata ya Mpapa; Kijiji cha Barabara - Kata ya Matili; lakini pia Kijiji cha Kimbindachini - Kata ya Muungano. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbinga ni milimani, na kwa hiyo, sasa kutokana na uhifadhi maeneo mengi ya milimani tunapewa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga naomba uulize swali moja kwa moja. Swali la kwanza na la pili, tafadhali; uliza swali lako la msingi.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nilikuwa nauliza swali hapo, kwamba basi acha ulivyonielekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kuwafanya wananchi hawa waweze kuishi na misitu katika milima iliyopo Wilaya ya Mbinga? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali inatoa kauli gani katika maeneo yaliyoanzishwa Miradi ya Panda Miti Kibiashara bila kushirikisha wananchi, ili kuwarejeshea maeneo haya wananchi husika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa kutoa elimu, nitoe tu maelekezo kwa watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii hususan Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, tunapoenda kuainisha hii mipaka wahakikishe kwamba tunashirikisha wananchi walioko katika maeneo hayo ili kuwepo na urahisi wa kutambua mipaka iliyopo na kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutalizingatia, lakini pia tutaendelea kutoa elimu ya namna ya uhifadhi wa mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la pili ambalo amelisema kwenye Mradi wa Panda Miti Kibiashara; kikawaida mradi huu unawawezesha wananchi kujiinua kiuchumi kupitia mazao ya miti, na mara nyingi tunashirikisha wananchi kabla ya mradi huu kufika katika eneo husika. Kwa hiyo, kama kuna maeneo ambayo tumepeleka mradi huu halafu hatukushirikisha wananchi, basi tumefanya makosa na tutaenda kupitia upya utaratibu uliopo ili wananchi waweze kufaidika na miradi hii ya Panda Miti Kibiashara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamuita Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 447

**Mkakati wa kuongeza watalii Mbuga ya Wanyama Ruaha**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, watalii wangapi walitembelea Mbuga ya Ruaha kwa mwaka 2019/2020 na upi mkakati wa kuongeza watalii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasilinna Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ilipokea jumla ya watalii 18,678 ambapo watalii 11,601 kutoka nje ya nchi na watalii 7,077 kutoka ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha idadi ya watalii inaongezeka, Serikali imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Kuanzisha na kuboresha miundombinu ya barabara za ndani ya hifadhi kwa kiwango cha changarawe na kuboresha barabara kuu kutoka Iringa Mjini hadi hifadhini.

(ii) Kuongeza na kuboresha viwanja vya ndege saba ndani ya hifadhi.

(iii) Kuongeza miundombinu ya malazi kwa kuongeza vitanda 263 na kutangaza maeneo ya uwekezaji.

(iv) Kuongeza na kuboresha mazao ya utalii kama utalii wa puto, boti, farasi, kuvua samaki, utalii wa kitamaduni na kihistoria, utalii wa mikutano na utalii wa michezo.

(v) Kuongeza utangazaji wa vivutio vya hifadhi katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika Awamu ya Tano ambayo kupitia *RIGRO* walipendekeza kwamba lengo kubwa ni kukuza utalii Kusini na walichagua Mkoa wa Iringa uwe ni makao makuu ya mradi huo. Sasa tumeshatenga eneo lipo na kila mwaka tunaadhimisha wiki ya utalii pale Mkoa wa Iringa.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha utekelezaji wa makao makuu haya unafanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi walioko pembezoni mwa mbuga hii wanapata elimu, wanawezeshwa kielimu na kiuchumi kuhakikisha kwamba wao ndio watakaokuwa watangazaji wa mbuga hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri tunaomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza niendelee kuwapongeza Wabunge wote wa Iringa, pamoja na kuwa swali hili na Mheshimiwa Grace Tendega, lakini mara nyingi wanafuatilia sana kwenye mradi huu wa *RIGRO* na ujenzi wa *information center* ambayo itajengwa Makao Makuu Iringa uko kwenye hatua za kuanza. Tayari tulikuwa kwenye mkakati wa mkandarasi ambaye tayari tulikuwa tumeshatangaza kazi na

tuko *anytime* kuanza kazi hii. Kwa hiyo, naomba niwataarifu tu kwamba Wana-Iringa na Watanzania wote kwa ujumla kwamba utalii na mkakati wa kukuza utalii Kusini mwa Tanzania uko mbioni kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili la kuwapa elimu wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi; kwenye Mradi wa *RIGRO* zimetengwa fedha kwa ajili ya kuwapeleka *training* wananchi mbalimbali waliozunguka katika maeneo yanayozunguka mradi huu, na ni shahidi tosha Wabunge wanaotoka katika maeeo hayo wanafahamu kwamba tumekuwa tukipeleka watoto ambao wanapelekwa shuleni kwa ajili ya kujifunza namna ya kuendeleza masuala mazima ya utalii na uhifadhi. Kwa hiyo, faida wameshaanza kuziona na wananchi wameshaanza kuona faida ya mradi huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Naomba maswali yawe mafupi na majibu yawe mafupi. Mheshimiwa Zaytun Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa kwenye sekta hii ya utalii ni uhaba wa hoteli zenye hadhi ya kulaza wageni wetu; je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naomba arudie swali sijalielewa vizuri.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa kwenye sekta hii ya utalii ni uhaba wa hoteli zenye hadhi ya kulaza watalii wetu; je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hii?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa sasa tayari Serikali imeshaanza kutangaza maeneo ya uwekezaji na tayari wawekezaji wameshaanza kujitokeza. Kwa hiyo, suala la uhaba linaenda kupungua ama kuisha kabisa kutokana na uzinduaji wa filamu ya *Royal Tour* na mkakati wa uwekezaji ambao tayari tumeshaanza kuuweka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa ajili ya kuongeza idadi ya watalii na kuboresha uhifadhi katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti; je, ni lini ujenzi wa uwanja wa ndege wa Serengeti utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba tu niwataarifu ndugu zangu wana-Serengeti, hususan Mugumu kwamba mchakato unaendelea na uko kwenye hatua za utekelezaji kwa maana ya kuanza. Tayari tulishaanza mchakato na namna ya ku-*identify* hayo maeneo na lengo ni kuhakikisha kwamba tunapunguza muingiliano wa shughuli za uhifadhi katika Hifadhi ya Serengeti, hivyo uwanja tutauhamisha usogee katika Eneo la Mugumu. Kwa hiyo, mchakato unaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jitihada za kuongeza watalii dunia nzima ni kurahisisha miundombinu, hasa

barabara na mageti kutokea kila upande. Kuna maelekezo ya Serikali pale Mbuga ya Mikumi kufungua geti lingine kwa upande wa Kilangali na Tindiga ili kurahisisha usafiri wa watalii kutokea Kilosa kwenye *station* ya *SGR* itakapokamilika.

Je, Serikali ina kauli gani? Lini geti hili linaenda kufunguliwa kuheshimu maelekezo ya Makamu wa Rais, lakini wewe pia Naibu Waziri ulipoitembelea Mikumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunatambua kwamba, geti hili ni la muhimu sana kwa ajili ya uchumi wa nchi, hususan katika masuala mazima ya utalii na tayari tulishaanza mpango wake. Kwa hiyo, nimuondoe shaka Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi kwamba geti hili tutalifungua na pale tu ambapo mchakato wa reli utakavyoanza tayari na sisi utekelezaji wake utakuwa umekamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Masanja kwa majibu.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, namuita Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali aweze kuuliza swali lake.

Na. 448

**Hitaji la anuani za makazi katika baadhi ya Kata za Mbarali**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, lini Kata za Miyombweni, Malilo, Songwe na Luhanga zitawekwa anuani za makazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 8 Februari, 2022 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi ufanyike kwa njia ya operesheni kwa usimamizi wa Wakuu wa Mikoa na kwamba utekelezaji wake ukamilike mwezi Mei, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais ulifanyika kwa tija na ufanisi mkubwa ambapo hadi Mei, 2022 Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa, Shehia zote nchini zilikuwa zimefikiwa. Aidha, utekelezaji ulifanyika kwa kuzingatia miongozo iliyopo ikiwa ni pamoja na kutotoa anwani za makazi maeneo ambayo ni hatarishi yasiyoruhusiwa kwa makazi mfano, mabondeni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo oevu, maeneo ya hifadhi, maeneo ya wazi na maeneo ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Kata za Miyombweni, Malilo Songwe na Luhanga zipo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, baadhi ya maeneo yale wamesharudishiwa wananchi kwa matumizi yao. Sasa ni lini Serikali itayaratibu na kuyapanga upya maeneo yale kwa maana ya vijiji, vitongoji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ikitokea wananchi wamechoka jina la mtaa, je, wanaweza wakabadilisha jina? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza; eneo ambalo limerudishwa katika vijiji tutashirikiana kwa sababu yanagusa Wizara mbalimbali, tutashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, tutashirikiana na Wizara ya Ardhi, lakini vilevile tutashirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuona jinsi ya kulifanyia kazi na pale ambapo tutajiridhisha kwamba limesharejeshwa kweli, basi anuani za makazi zitawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili, swali la pili, pale ambapo wananchi au Serikali inataka kubadilisha jina la mtaa au jina la barabara; kuna utaratibu ambao unapitiwa. Lazima vikao vifanyike kwa ngazi ya chini na wananchi washirikishwe na pale ambapo Serikali itajiridhisha kwamba ndani ya kata moja kuna jina la mtaa linalofanana na mtaa mwingine basi Serikali itawashirikisha wananchi ili kubadilisha, lakini hata pale ambapo wananchi

wanalalamika katika maeneo hayo yote hayo yatafanywa kulingana na utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kesi iko pale Goba, kwenye utaratibu ambao walishirikishwa mwanzoni waliamua kwamba jina lao liitwe Maghorofani, lakini baada ya kuwa wanatumia ile anuani wakajikuta kwamba jina lile linaitwa Janguo. Sasa tumeshatuma timu yetu kwenda kuhakikisha kwamba ni nani mefanya ujanja huo wa kubadilisha jina la mtaa bila wananchi wenyewe kujua kwamba utaratibu upi umetumika katika kubadilisha hilo jina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi wote kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, namuita Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 449

**Hitaji la Vyuo vya *VETA* – Lindi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Vyuo vya *VETA* katika Wilaya za Liwale, Nachingwea, Ruangwa na Lindi Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika Wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Tayari Serikali imeshakamilisha kuandaa michoro na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale na Nachingwea ni miongoni mwa Wilaya 64 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa Vyuo vya Ufundi Stadi kwa mwaka huu wa fedha. Tayari kiasi cha shilingi 228,942,380 kimeshatolewa kwa kila chuo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Ruangwa umeshakamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 2.3 na mafunzo yameshaanza kutolewa. Aidha, kwa Wilaya ya Lindi tayari kipo chuo cha mkoa kinachoweza kutumiwa na wananchi wa Halmashauri ya Lindi Vijijini, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; je, ni lini Serikali itatoa pesa au kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kilwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; vifaa vilivyopo kwenye Chuo cha *VETA* Lindi Mjini ni vya kizamani sana; je,

Serikali haioni haja ya kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya Lindi Mjini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha jibu kwenye majibu yangu ya swali la msingi kwamba vyuo hivi vinajengwa katika Wilaya 64, na Wilaya ya Kilwa ni miongoni mwa Wilaya 64 ambazo zinajengewa, na tayari tumeshapeleka shilingi milioni 228 kule Kilwa, na usimamizi wa chuo kile kinachojengwa pale unafanywa chini cha Chuo chetu cha *FDC* ambacho kipo katika Wilaya hiyo ya Kilwa.

Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, lakini niwaondoe hofu wananchi wa Kilwa, hata pale Kilwa napo ni miongoni mwa Wilaya 64 ambazo zinajengewa vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili, amezungumza suala la vifaa; ni kweli tukiri kwanza katika vyuo vyetu vya zamani tulikuwa na vyuo 45 vya zamani ikiwemo na hiki cha Lindi, lakini tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa utashi wake na maono yake, katika kipindi hiki kifupi tumeweza kukamilisha vyuo 29 na hivi sasa tunakwenda kujenga vyuo vingine 65, vyuo 64 katika Wilaya na kimoja cha Mkoa. Hivi sasa Serikali inafanya tathmini kwa vyuo vile vyote 45 vya zamani na hivi 29 ambavyo tulijenga katika mwaka uliopita wa fedha, tathmini ya vifaa pamoja na mitambo mbalimbali kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia. Kwa hiyo, tuko njiani kupeleka vifaa hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali langu ni hili; je, Serikali inaweza ikatoa kauli gani kuhusu uwezekano wa kuingia ubia na taasisi za kidini ambazo zilijenga Vyuo vya Ufundi Stadi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimtoe hofu Mheshimiwa Kimei, utaratibu huo upo. Naomba tu kwa vile ni suala mahususi, baada ya kikao chetu hiki au baada ya kipindi hiki cha maswali, tunaweza tukakutana ili tuweze kuangalia hilo eneo au hivyo vyuo ulivyovitaja namna gani tunaweza tukatengeneza huo ushirikiano wa kutoa mafunzo kwa pamoja baina ya wawekezaji pamoja na Serikali, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, namwita Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 450

**Ujenzi wa barabara ya Singida hadi Kizaga**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Singida – Sepuka - Ndago hadi Kizaga kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandaasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Singida kuanzia Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga yenye urefu wa kilometa 77.6 amepatikana na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kuwahakikishia Wana-Singida Magharibi kwamba kabla ya mwezi ujao tutakuwa tumesainiwa mkataba wa ujenzi wa barabara ya lami, kilometa 76; tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu; je, Serikali sasa iko tayari kuifanyia upembuzi yakinifu barabara ambayo inatoka Singida – Mtunduru – Ighombwe – Iyumbu mpaka Tabora ambayo itaunganisha na barabara inayokwenda Kwamtoro – Kiteto mpaka Tanga ili kuwarahisishia wananchi wa Singida mawasiliano ya Tanga, Singida na Tabora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali iko tayari kuipandisha hadhi barabara ya Puma – Ihanja – Iseke –

Mwintiri – Igelansoni mpaka Itigi ili kuwapunguzia adha wananchi kutokana na uharibifu mkubwa wa barabara hii unaotokana na hali za mvua zinapokuwa zikinyesha?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu katika barabara hizi zote na hatimaye tunakwenda kusaini mkataba mwezi ujao (Juni).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la kwanza kuhusu upembuzi yakinifu katika hii barabara ya Singida – Mtunduru – Ighombwe – Ngungira mpaka Iyumbu yenye kilometa 113, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Singida Magharibi kwamba katika bajeti ya mwaka tutakaoanza 2023/2024 ambao mlipitisha bajeti siku ya Jumanne, tumetenga fedha takribani shilingi 165,041,665 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, na kwa maana hiyo barabara hii ipo katika mpango kama maandalizi ya kuja kuijenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kupandisha hadhi barabara ya Puma – Ihanja – Mwintiri – Iyumbu; barabara hii inahudumiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji *(TARURA)* na sisi Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tuko tayari kama itapandishwa hadhi kwa kufwata utaratibu ule ambao umewekwa, kwa maana ya kupitia kwenye vikao maalum, kupitia *DCC,* inakwenda kwenye *Road Board* ya Mkoa, na hatimaye Mwenyekiti wa Bodi anaandika barua kwa Mheshimiwa Waziri ili Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi atume timu

kwenda kuikagua hii barabara na hatimaye tutoe hiyo ridhaa ya kupandishwa hadhi barabara hii, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, aulize swali lake.

Na. 451

**Ujenzi wa barabara ya Tarime – Nyamwaga hadi Serengeti**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, kwa nini ujenzi wa barabara ya Tarime – Nyamwaga – Serengeti umeanzia katikati badala ya kuanzia Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ya Tarime – Nyamwaga hadi Serengeti sehemu ya Mogabiri hadi Nyamongo yenye kilometa 25 umeanzia katikati kwa maana ya Mogabiri badala ya mjini kutokana na kipande cha Tarime Mjini hadi Mogabiri chenye urefu wa kilometa 9.3 kilichojengwa kwa kiwango cha lami miaka 10 iliyopita wakati zabuni ya kazi inatangazwa kilikuwa kinafanyiwa tathmini ya ubora wake na kuona nini kifanyike ili kiimarishwe, hivyo kilirukwa na zabuni ikatangazwa ya kuanzia katika eneo la Mogabiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini kukamilika kipande hicho kimejumuishwa kwenye awamu ya pili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Tarime Mjini hadi Mogabiri na Nyamongo hadi Mugumu kilometa 62.14. Mkataba wa kuanza kazi unategemewa kusainiwa kabla ya mwisho wa Juni, 2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa maamuzi hayo mazuri na jibu zuri ambalo wameweza kutujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati barabara hii inapanuliwa kuna wananchi ambao walikuwa wamejenga pale na walibomoa nyumba zile ili kupisha ujenzi wa barabara ile; je, ni lini watapata fidia yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; naishukuru Serikali kwa sababu imeleta taa za barabarani katika barabara hii ya *Kenya Road.* Lakini taa hizi zimewekwa kwa mbali sana kiasi kwamba hazimuliki vizuri.

Ni lini sasa zile sehemu ambazo hazina taa za barabani zikiwemo za Masara, barabara ya Musoma pamoja na Magena watawekewa taa za barabarani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia kwa wale waliobomolewa kupisha ujenzi wa barabara hii ni kweli kwamba wale wote waliobomolewa ni kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1967 na marekebisho yake ya mwaka 2007 Na. 13, kwamba waliokuwa ndani ya hifadhi ya barabara kwa maana ya mita 22.5, hawa ndio walioguswa, lakini waliokuwa nje ya hifadhi ya barabara, mpaka mita 30 hawakuguswa. Kwa hiyo hapa hakutakuwa na fidia kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la taa za barabarani; tumewaelekeza *managers* wote wa *TANROADS* nchi nzima kwamba lazima watenge fedha kwa ajili ya kuweka bajeti za taa barabarani na kwa maana hiyo kwenye mwaka wa fedha ujao katika eneo hili la Tarime Mjini, tumetenga shilingi milioni 270 kwa ajili ya kusimika taa za barabani na mitaa yake yote. Na hata hivyo, kuna taa nyingine ambazo zimeshasimikwa lakini tutaongeza zaidi ili huu mji uweze kupendeza zaidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; kwa nini ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Magole – Turiani – Mziha – Handeni umeanzia Magole na kuishia Turiani na kuacha kipande cha Handeni – Mziha – Turiani?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kwagilwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii aliyoitamka kwamba imeanzia sehemu hiyo kipande na kingine

kimeachwa, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Serikali ni kujenga yote. Kwa hiyo tumeanza hicho kipande, lakini hata kipande kingine pia tutakimalizia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweka taa za barabani katika Mji wa Nyamilangano ambao tayari umewekewa kilometa tatu za lami?

**MWENYEKITI:** Swali fupi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, taa za barabarani katika maeneo ambayo ameyasema tumetenga kwenye bajeti ambayo imepitishwa na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tutamuwekea katika eneo lake Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, swali la nyongeza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kampeni za Rais wa Awamu ya Tano, aliahidi katika Mkoa wa Shinyanga atatujengea barabara kilometa 10, na juzi, mapema mwaka huu, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mpango, aliahidi wakati akizindua Hospitali ya Rufaa ya Mwawanza pale Shinyanga, kwamba atatujegea kilometa 10.

Nini mpango wa Serikali kuhakikisha inatekeleza ahadi hizo za viongozi wa Kitaifa, hasa katika mwaka huu wa fedha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salome Makamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi zote za viongozi wa Kitaifa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika bajeti ya mwaka huu tumezizingatia kwa kiwango kikubwa. Na kwa maana hiyo, hata barabara aliyoisema Mheshimiwa Salome Makamba ni miongoni mwa barabara ambazo tunakwenda kuzijenga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kuanzia Kalela – Munzeze mpaka Buhingwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitamka kuanza Kalela na kuendelea ni barabara ambayo katika bajeti ya mwaka ujao tumeitengea fedha kwa ajili ya kufanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe, barabara ya kutoka Kibena – Lupembe – Madeke hadi Taveta, Mheshimiwa Swalle, Mbunge huyu, amekuwa akiizungumza sana barabara hii. Ni lini sasa barabara hii itaanza kujengwa kwa lami ili wananchi wa Lupembe wapate imani na Serikali yao?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali hili la nyongeza la mwisho.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii inaunganisha Mikoa ya Njombe, Iringa na inakwenda mpaka Morogoro, na katika mwaka wa fedha huu ambao tutaanza, ni miongoni mwa barabara ambazo tumezitengea fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cheti cha maswali la majibu. Tunaishukuru Serikali kwa majibu, lakini tunawashukuru Wabunge kwa kuuliza maswali mafupi ambayo yanatoa fursa kwa Wabunge wengi zaidi kuweza kupata fursa hiyo.

Hapa ninayo matangazo machache; tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge, anasema; naomba

uwatangazie Wabunge wote kuwa Wizara ya Nishati itaendesha semina kuhusu Rasimu ya Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia. Semina hii itafanyika Siku ya Jumamosi, tarehe 27 Mei, saa4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kuwajengea uelewa sambamba na kupata maoni yao kuhusu dira hiyo. Kwa hiyo, mnaombwa msikose Jumamosi, tarehe 27 Mei.

Lakini pia ninalo tangazo hapa kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Tarimba Abbas; anasema naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho, siku ya Jumamosi kutakuwa na mchezo wa mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na Umoja wa Machifu. Mchezo utafanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri saa 10.00; wote mnakaribishwa.

Sasa ninyi mnajua Machifu msipoenda wanaweza wakawaleta tu hata pasipo ninyi kutaka. Machifu watacheza kesho; wako pale, na mtawaona, wako hapa ukumbini leo. *(Makofi)*

Tangazo la tatu ni la wageni; *Speaker's Gallery* pale tunayo Timu ya Mpira wa Miguu ya Umoja wa Machifu Tanzania ikiongozwa Mwenyekiti wao ambaye nitamtaja baadaye, lakini naomba Machifu wote wasimame, kwa heshima kubwa. *(Makofi)*

Karibuni sana Machifu wetu na Timu yetu ya Bunge iko tayari kwa ajili ya kucheza na ninyi kesho ikizingatiwa kwamba ninyi ni Machifu, kwa hiyo tutajitahidi angalau kutokuvunja sana heshima yenu kubwa mliyonayo. Ikitokea mmeshinda goli moja mmetuzidi, basi ni kwa sababu ya heshima, lakini angalau tutawaonesha kidogo. *(Makofi)*

Naomba mketi, timu hii ya Machifu inaongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu ambaye ni Bi. Tonisiza Sangalali. Hawajakuona vizuri, punga vizuri wakuone vizuri. Nafikiri mnamuona pale. Ahsante sana, tunakushukuru. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni wengine waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika; ni wageni tisa wa Mheshimiwa Spika, ni wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma Programu ya *Master of Education (Med),* ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Angeline Mabula ambaye pia ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni kama ifuatavyo: -

Yuko Ndugu Ernest Majeshi, Mchungaji *Word Alive Center*, ahsante. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Hamida Hillary, Mjumbe wa Mkutano wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mwanza, ahsante. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Michael Lubala, Kaka yake na Mheshimiwa Waziri, ahsante. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Angelina Daudi, rafiki wa familia hiyo. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kama ifuatavyo; tuna wageni 19 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Viongozi wa Baraza la Ushauri la Wazee Taifa, nafikiri watakuja baadaye.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jonas Zeeland ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mvomero. Yuko wapi? Ahaa, Mheshimiwa Jaka, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Ally Kassinge ambao ni Kikundi cha Utunzaji wa Mazingira kutoka Kilwa Masoko Mkoa wa Lindi, ahsante sana *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo kutoka Singida Kaskazini, Mkoa wa Singida, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Marekani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Salome Makamba kutoka Jijini Arusha, hatujapewa jina lake hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia tunao wageni mbalimbali ambao wametembelea Bunge letu kwa ajili ya mafunzo na hapa nitaanza na wanafunzi 129 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi *Good Hope* ya Jijini Arusha, karibuni sana kwa ajili ya kujifunza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 154 na walimu 12 kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Misericordia ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Sr. Alfonsia Aloyce, karibu sana Sister Alfonsia Aloyce pamoja na timu yako. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG.MONICA MWAGA-KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na mjadala wetu na wachangiaji wetu ni kama wafuatao, lakini nitaanza kuwataja wale watatu wa kwanza; ataanza Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, akifuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay wakati huo Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto wanajiandaa.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu, lakini nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetupa uzima siku ya leo na hata siku zingine zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kujenga Taifa letu na Serikali yake yote kwa ujumla, Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Makatibu, Naibu Katibu Mkuu na wote ambao wanamsaidia Mheshimiwa Rais kufikia malengo yake ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa letu mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia mjadala huu kwa eneo la upimaji wa ardhi. Upimaji wa ardhi katika Taifa letu haiko vizuri na haliko vizuri kwa sababu kwanza wananchi kupata ardhi katika nchi yetu imekuwa ni

changamoto. Changamoto yake ni kwamba upimaji wa ardhi bei ni kubwa ukilinganisha na hali halisi ya wananchi wetu katika vijiji na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa hati Tanzania ni kama kupata lulu, sijajua huwa ni kwa nini Tanzania ukitaka kupata hati inakuwa kama vile sijui una nunua nini? Ile karatasi sijui inapatikana katika misingi gani! Kwa sababu ni kwa nini ardhi haikubaliwi kupimwa kwa urahisi Tanzania na mtu akapewa hati kwa uharaka. Wataalam wanasema sijui wanafanya michoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michoro inachukua muda mrefu, ardhi haipimwi matokeo yake migogoro kwenye vijiji, migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro ya Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa hatimaye tunaonekana tunaendelea kukataa kupima ardhi kwa sababu ya kuweka bei kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Wizara imeweka mawakala wa kupima ardhi, yale makampuni yamekwenda kule kwa wananchi wamekusanya fedha hawajarudi kuwapimia wananchi ardhi ili waweze kuwapa ardhi. Wengine wameingia mitini, lakini hii inatokana hivi kwa nini, nadhani ni kwa sababu Wizara mna jambo la kufanya kuhusu eneo hili la upimaji wa ardhi hasa makampuni ambayo mmeyaweka na kuyafanya yakapime ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaamini kwamba Serikali imetumia makampuni hayo ili iweze kuwachukulia fedha zao. Kila mwananchi ametoa shilingi 150,000 lakini hawajapimiwa ardhi, yale makampuni hayaonekani, sasa hii ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baadae Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuhusu fedha zilizochukuliwa wananchi kwa makampuni haya ambayo yamepima ardhi. Kwa

sababu tunakwenda kuwaletea wananchi wetu matatizo kwa kuweka makampuni ambayo sio waaminifu na sio waadilifu. Najua nia ya Serikali ni njema, najua nia ya Wizara ilikuwa ni njema, lakini sasa katika utekelezaji wa jambo hili limeenda kutuletea changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wageni kumiliki ardhi, wakati mwingine hili suala la wageni kumiliki ardhi tunaambiwa sana wageni hawamiliki ardhi, lakini mimi naona ni kinyume sana tukisema hivyo kwa maana hii *Derivative Right of Occupancy* ambayo anapewa mgeni ni kama amemiliki tu. Unawezaje kumpa mgeni amemiliki ardhi miaka 99 halafu yeye anasema ni mwekezaji, sawa anakuja pale ile ardhi inakuwa ni yake wala hawekezi chochote pale anatumia ile hati aliyopata kwenda kukopa benki. Akikopa benki ule mradi anauacha, anakimbia na fedha, anatelekeza ardhi matokeo yake ile ardhi inakuja inauzwa tena kwa kufidia zile fedha au yule mwekezaji amekaa na ile ardhi yote pale kwa miaka hiyo yote 99 anaamua kuuza ile ardhi kidogo kidogo anauza kidogo kidogo kwa maana anasema ana *sublease* hii sio sawa. Mimi naona kama hili suala la kusema wageni wamiliki ardhi haliko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima Wizara, Mheshimiwa Waziri mkae muone namna ya kurekebisha hii ya sheria ya wageni kumiliki ardhi kwa sababu kama mtu amekuja na mtaja labda milioni 500 viwekwe vipengele ambavyo mtu haruhusiwi kuuza ardhi, haruhusiwi kutumia ile hati kwa kukopa fedha, anatakiwa aje na mtaji wake kama ile Sheria ya *Tanzania Investment Centre* inavyosema. Kama hatufanyi hivyo bado tunajidanganya kwamba wageni hawamiliki ardhi. Kama unammilikisha miaka 99 wakati hakuna binadamu ambaye hata kwenye vitabu vya Mungu ni miaka 70, miaka 80 ni ya tabu na huzuni, hiyo miaka 99 nani anajua kwamba atafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa bado kuna changamoto inatakiwa muangalie kwa sababu bado hatuwatendei wananchi haki katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Mabaraza ya Ardhi; Mabaraza ya Ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi *(Land Act No. 113)* ya mwaka 1999 na Sheria ya *Land Disputes Courts Acts* iliyoanzisha mabaraza hayo mwaka 2002 na ikaanza kufanya kazi mwaka 2003, ni miaka 20 sasa imepita nadhani tuna mabaraza 92 Tanzania nzima. Hii sioni kama ni haki kwa sababu ukiangalia hata kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza katika Ibara ya 107(a) kwamba lazima Serikali iweke mazingira ya kutocheleweshа haki bila sababu zozote. Sasa katika mabaraza hayo hayana mfumo mzuri wa utoaji haki. Kama baraza linaweza kupiga kesi miezi sita, mwaka mmoja, miaka miwili, mitatu, mitano bila kutoa haki hii sio sawa kwamba wananchi hawa wanapata haki kupitia mabaraza haya. Martin Luther King aliwahi kusema; *"A right delayed is a right denied"* haki iliyochelewa ni sawa na haki iliyonyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira hayo ya mabaraza haya hatuwezi kuona kwamba haki inatendeka katika mabaraza ambayo hayana mfumo mzuri wa kimahakama, na kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka bayana kwamba mamlaka iliyopewa kutoa haki ni mahakama kwa nini mabaraza haya sasa isifike mahali tuachane na mfumo uliopo ambao udhibiti wake wa namna ya kutoa haki haupo sawa, tukaingiza kwenye mfumo wa mahakama ambayo itakuwa kwenye udhibiti. Mahakama imekaa vizuri sana katika utoaji wa haki kwa sasa. Kwa nini tunaendelea kung'ang'ania mabaraza hayo chini ya Wizara? Hatuoni tunawanyima wananchi haki? Ukizingatia kwamba tumeshindwa kufikia mabaraza yote katika Wilaya nzima. Unakuta katika Mkoa mmoja wenye Wilaya saba mpaka tisa kuna mabaraza mawili tu tena yapo pale Mkoani, hii haki iko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatutendi haki kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais amefika mahali anawataka wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wapate haki mpaka ameenda mbali zaidi ameunda Tume ya Haki Jinai; unafikiri anafikiria nini? Watu walioko magerezani na popote pale wakiteseka waweze kupata haki zao. Je, ni kwa nini sisi kama Wizara au ninyi kama Wizara msione sasa kwamba kuna haja ya ku-*handover* hayo mabaraza kwenye mfumo wa mahakama? Kuna tatizo gani na shida gani? Kwa sababu ukiangalia kwa maana ya *research* miaka 20 kama hamjaweza ku-*meet* vile vigezo vya kila Wilaya kuwa na mabaraza ina maana tume-*fail*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe baadae Mheshimiwa Waziri hili suala mlitolee tamko na sio suala gumu. Tuna mfumo mzuri wa mahakama yetu kuanzia Baraza la Kata, Mahakama ya Mwanzo mpaka juu hata hayo mabaraza yakiendelea kuwepo, lakini yaingie kwenye mkondo wa kimahakama hii itasaidia wananchi waweze kupata haki na kuepuka kufata haki kule mbali ambako sio sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaamini Mheshimiwa Rais aliyewaweka pale, Mheshimiwa Waziri, Rais anakutegemea umsaidie katika kuleta mabadiliko katika Wizara hii ya Ardhi. Mabadiliko yenyewe ni haya ambayo inatakiwa wananchi waone haki inatendeka kwa sababu sio tu haki itendeke, lakini haki ionekane ikitendeka.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, wananchi wanakutegemea, wanakuangalia unavyoweza kuwatoa katika dhiki hii ya mabaraza haya. Tume ya Kurekebisha Sheria inatakiwa iyaone haya kwa sababu ni kazi yao kuleta sheria ambazo hazina tija na zimepitwa na wakati. Sheria ya Ardhi irekebishwe, Sheria hii ya Mabaraza irekebishwe na

sheria zingine ambazo ni kandamizi na hazileti tija na mwelekeo mzuri kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, namuita Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay aweze kuchangia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya makadirio ya Wizara ya Ardhi. Kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sisi sote na Taifa letu kwa ujumla maana yeye ndiye anayewezesha haya yote na uwepo wetu sisi lakini na baraka zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumwombea na kumshukuru sana Hayati Baba wa Taifa Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere ambaye Serikali yake ya Awamu ya Kwanza iliona jambo hili la ardhi ya Tanzania kuwa mali ya Serikali ya Tanzania kinyume na nchi zinazotuzunguka. Hii imefanya thamani ya ardhi yetu kuwa mali yetu kama Watanzania lakini pia kutokuwa na mkanganyiko wa muingiliano kwa kuwa umilikishwaji wake unatolewa kwa Watanzania kwa dhamana ambayo Serikali inayo ili sisi wote kama Watanzania tuwe wapangaji kwenye ardhi. Kwa sababu tunaona migogoro mingi na umilikaji unaotumika katika baadhi ya nchi ambao unamilikiwa na watu kutoka nje na wageni na unao leta mkanganyiko kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Rais. Zipo kazi nyingi sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amejitahidi katika Serikali ya Awamu ya Sita na Serikali zote zilizopita kwa jinsi ambavyo nchi yetu inakwenda mbele na tunasonga mbele

katika muundo wa Serikali, lakini kwa maendeleo na huduma kwa wananchi. Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana. Hatutaweza kupata muda wa kutosha kuzungumzia jambo hili tukiwa humu, niwaombe Wabunge wenzangu wote tuwe wakalimani wa kwenda kuyazungumza hayo kwa wananchi na kutafsiri kwa wananchi wetu. Ushahidi kila Mbunge anao kwenye Jimbo lake na katika eneo lake kwa jinsi ambavyo Serikali imejitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi pia kwa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa sababu tunajua mapungufu hayataisha, lakini tunaona hatua zinavyochukuliwa na tunavyojaribu kusonga mbele na kupata mafanikio kupitia Wizara hii. Zipo changamoto nyingi lakini kwa ujumla nchi haijengwi siku moja. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu tunampongeza Waziri na timu yake na wale Mawaziri waliopita, Mbulu Mji tumepewa fedha za upimaji na umilikishwaji lakini kupima, kupanga na kumilikisha. Ni fedha ya maoteo inayotolewa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza zoezi hili la upimaji wa mipango miji. Zoezi hili la upimaji mipango miji na fedha hizi hazina riba, ni fedha zinazotolewa na Serikali na baadaye tunarudisha bila riba, lakini imefanya tatizo kubwa la ujenzi holela wa miji yetu kupungua kwa sababu kadri tunavyopima tunaondoa mgogoro wa upimaji, lakini pia tunaondoa mgogoro ambao unazalishwa na kesi za muingiliano na kesi za kunyang'anyana ardhi baina ya wananchi na wananchi, ama taasisi; ama mtu na mtu hali ambayo inaifanya na kuipeleka mipango miji, lakini na umilikaji wa ardhi kuwa na hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilipotolewa katika Halmashauri mbalimbali na Mbulu ikiwemo imekumbwa na changamoto nyingi sana na changamoto kubwa ni uhaba wa watumishi. Unakuta kwenye Halmashauri moja Afisa Ardhi ni mmoja, Afisa Mipango Miji ni mmoja lakini wanaohitajika kwenye zoezi zima wanaweza kufika kumi na ilipofika hapo

halmashauri nyingi zilitafuta makampuni kwa njia ya *tender* ama kwa njia ya nukuu za bei, lakini zile kampuni zilizopatikana kwa namna moja au nyingine hazijatusaidia kwa jinsi inavyopasa na jinsi ambavyo manufaa na matokeo mazuri ya zoezi hili au ya fedha hizi zinapatikana katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano fedha nyingi zinakwenda kwenye ukodishaji wa vifaa, kulipa wataalam lakini pia na uandaaji wa mipango kitu ambacho kinafanya eneo hili la upimaji kukosa mafanikio makubwa. Rai yangu hapa ni kwamba pengine Serikali katika mipango yake ya mwaka huu na miaka inayokuja iangalie zile kada muhimu sana za ajira katika Wizara hii ya Ardhi ili utekelezaji wa Serikali ipate ufanisi na mafanikio zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huu wa watumishi katika Sekta ya Ardhi unakwaza shughuli nyingi. Kwa hiyo, tusipouondoa ina maana huna rasilimali watumishi lakini pia na ufanisi unatarajiwa ili kufikiwa katika hatua inayofaa. Mara nyingi fedha hizi zinapotolewa elimu kwa wananchi ni ndogo sana kwa wale wanaosema upimaji umekuwa na gharama kubwa tatizo kwenye upimaji sikuona kwa upimaji ushirikishi kwa sababu gharama zinazotolewa kupima viwanja ni gharama zinazotekelezeka, tatizo kubwa ni uhamasishaji, tafsiri ya mwanzo kwa wananchi katika elimu kwa jinsi ambavyo tunataka eneo hilo liwe kwenye mipangoo miji na liweze kupimwa na kupatiwa michoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa nataka kuishauri Serikali, twendeni kwa pamoja kama Wizara tuone utatuzi wa jambo hili unafanyika ili kuondoa matatizo makubwa kwa sababu tayari shule zilizopimwa, taasisi zingine zilizopimwa lakini pia maeneo ya miji yaliyopimwa yana dosari mbalimbali na kwa zoezi lolote lile linalofanyika lazima lifike muda tufanye tathmini na changamoto zilizoko na mafanikio

yaliyopatikana ili zoezi lililotarajiwa liweze kufanikiwa na kupata mafanikio mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hivi kwa sababu fedha hizi kwa kadri zilivyotolewa kuna migogoro, unakuta Wilaya na Wilaya kuna migogoro, Mikoa na Mikoa kuna migogoro na Mkoa wa Manyara una migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa sana hasa hasa hizi za mipaka ya maeneo ya utawala, lakini pia migogoro ya taasisi na taasisi lakini pia na migogoro ya mtu na mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali walitupa Baraza la Ardhi kule Dongobesh, lakini hata hivyo msaada wa lile baraza utapatikana na utatoa tija endapo ardhi hii itapimwa, lakini pia mipaka ya kila mmoja ikaainishwa na zoezi hili likafanikiwa ili kuondoa kesi nyingi na malalamiko mengi kwa wananchi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali eneo la Mkoa wa Manyara, ukienda Wilaya ya Simanjiro ni migogoro isiyoisha. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri na timu ya Mawaziri imeenda mara kadhaa, Wilaya ya Kiteto ni migogoro isiyoisha Wilaya ya Babati ni migogoro isiyoisha, Wilaya ya Mbulu ni migogoro isiyoisha. Niombe tathmini ya ile timu ifanyike, mrejeshio upelekwe kwa wananchi baadae, na tafsiri ya Sheria zitakazokuja baadae zitolewe kwa wananchi kwamba baada ya mapendekezo yaliyotolewa fikra za wananchi wale, mrejesho wa wananchi upatikane na tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze eneo la mabaraza ya ardhi; Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Dongobesh Mheshimiwa Waziri anahudumia mabaraza mawili, kwa hiyo kesi nyingi huwa zinakwama pale Dongobesh kwa ajili ya kwamba anakuwa anahudumia Wilaya nyingine kule Ngorongoro na huku anahudumia Mbulu.

Nilikuwa naomba kwenye bajeti hii kama itawezekana baadhi ya mabaraza yaliyo anzishwa yapate Wenyeviti wake ili walau kupunguza msongamano wa kesi katika maeneo mengi na hili tuweze kupata manufaa ya wananchi kuhudumiwa kwa wakati, lakini pia kutokinung'unikia chombo hiki ambacho kinatarajiwa kutoa utatuzi wa matatizo hayo yaliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi sana yanahitaji kufanyiwa kazi katika sekta ya ardhi na kwa sababu hiyo eneo la Wizara hii tunaishukuru Serikali imeitengea fedha kwa yale mapungufu yanayoonekana basi Mheshimiwa Waziri mimi nikupongeze, lakini pengine Serikali ione kwa umuhimu fedha inazotenga kwenye Wizara hii ipeleke kwa kiasi kilichopendekezwa ili kutatua matatizo ya wananchi katika eneo hili la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo mahususi yatolewe na Wizara kwenda kwenye Halmashauri zetu. Shule za msingi, taasisi za dini, shule za sekondari, na maeneo mengine na mipaka ya vijiji yakipewa kipaumbele ina maana tunaenda chini kwa kadri ambavyo kila eneo tunakwenda kupima na kuonesha mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna zoezi linalolalamikiwa kwenye KKK; zoezi la KKK limekumbwa na tatizo, mwanzoni wakati tunakwenda kwa wananchi tunasema tunakuja kupima, halafu tunakuja na umilikishwaji. Katika hatua ya umilikishwaji hatufiki tunaishia kupima na kuweka *beacon,* kampuni zile zinaondoka, zikiondoka maeneo yale yaliyowekwa alama yanabaki kukosa alama za kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri, kuliko kuchukua eneo kubwa la upimaji lenye kupigwa nondo bila *beacon* na ambalo halipewi hatimiliki, mimi nadhani ni muhimu tukapima eneo dogo tukakamilisha

zoezi letu, lakini kwa tafsiri ya makubaliano ya pamoja kati ya Halmashauri zetu na wale wanopimiwa ili wapate hati na tujue zoezi la eneo hilo limekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu zile kampuni zikiishaondoka unakuta zile *beacon* baada ya muda hazina alama kwa sababu ni nondo zilipigwa, alama zile zinafutika, awamu nyingine tunaenda tena kupima yale maeneo na zile kampuni kwenye usimamizi na maombi ya fedha zilishaomba kwamba watamaliza mchakato wote na kila aliyepimiwa atapewa hati ili fedha zile ziwe na tija na manufaa kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza suala la Mabaraza ya Ardhi; Mabaraza ya Ardhi katika meneo mengi yanakaa kwa muda mrefu. Swali langu kwa Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na muda wako umekwisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie nashukuru sana na naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, wakati huo Mheshimiwa Robert Chacha Maboto na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga wanajiandaa.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanhu Wataallah* kwa kutujaalia uzima, salama na kuendelea kuijalia nchi yetu kuendelea

kuwa na usalama na kutamalaki kwa maisha mema nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependaa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya yeye pamoja na Naibu Waziri Ndugu Pinda, pamoja na timu nzima ya watendaji, kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Tumeona maendeleo makubwa tu katika mabadiliko ya ardhi na hili nafikiria ni *register* shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifaya na inaonesha wazi Mheshimiwa Rais, kwa kweli anapita katika nyanja zilezile ambazo alipita Hayati Julius Kambarage Nyerere, pamoja na Hayati Abeid Amani Karume, kwa kuweka usalama wa matumizi bora ya ardhi na kuwamilikisha wazawa na wananchi wanyonge kuendelea kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuelekeza mchango wangu katika maeneo matatu makubwa; la kwanza, mwenzangu jana Mheshimiwa Chege aliligusia kidogo kuhusu suala la sera. Nafikiria ni kipindi kirefu kidogo tumekuwa tukizungumzia suala la kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Ardhi pamoja na Sera ya Maendeleo ya Makazi nchini, na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na timu yake wamefanya kazi nzuri katika hili na hadi sasa tayari rasimu ipo na kuna mabadiliko machache ambayo yanasubiriwa hasa katika suala la diaspora pamoja na watu wa *real estate* kuweza kulikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa nina ushauri hapa; ushauri wangu ni kwamba nimuombe tu Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa zile changamoto ambazo zinaonekana ni ngumu kidogo kuweza kukamilika kwa haraka na kuikamilisha rasimu hii ya sera. Basi tungeendelea na mchakato tukaja tukaweka *provision* katika maeneo ya sheria katika maeneo ya sheria kwa kuja kuitayarisha kanuni ambayo itakuja kuwasaidia wenzetu wa *diaspora* pamoja na

usimamizi mzima wa masuala la *real estate*. Hii itafanya tukamilishe hii sera haraka na kuanza kuitekeleza ili iende ikasaidie zile changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge hapa wamekuwa wakizungumza kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la pili nigusie kidogo kuhusu suala zima la mipaka ya kimataifa; kazi nzuri imekuwa ikifanywa katika kuainisha na kuweka mipaka katika maeneo mbalimbali lakini bado hatuendi kwa kasi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tu, Mheshimiwa Waziri na hivi zaidi tusimlauimu Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ni Waziri wa Fedha, kwa sababu wao wanafanya kazi kulingana na kiwango cha fedha ambazo wanakasimiwa. Sasa ningeomba tu Waziri wa fedha akatenga fedha za kutosha ili hili zoezi la kuainisha na kuweka mipaka ya kimataifa kwa haraka basi likaenda kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea fedha kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha nafikiri hayupo, lakini anatusikia huko aliko, kwamba tuisaidie fedha hii Wizara ya Ardhi, kwa sababu hawawezi wakafanya miujiza kama hawana fedha za kutosha katika kulifikia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi pia nilikuwa na ombi moja hapa. Mheshimiwa Waziri najua tunashughulika na mipaka zaidi ya kimataifa lakini na mipaka ya ndani vilevile tuiangalie na haswa masuala ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wenzetu wa usimamizi hasa baharini wanapata shida wakati mwingine katika kusimamizi wa rasilimali za bahari na rasilimali nyingine za uvuvi na ulinzi kwa sababu mipaka ya Zanzibar na Tanzania Bara hasa katika eneo la bahari vilevile nalo ni kiini macho, kwa hiyo, ningeliomba na hili nalo tukaliingiza katika kuweka mipaka, basi na hili pia nalo tukaliingiza katika kubainisha ule mpaka hasa tukajua tukawasaidia watendaji wetu wa uvuvi, watendaji wetu wa kilimo, watendaji wetu wa

Serikali kwa ujumla wakajua ile mipaka ili usimamizi wao na utendaji kazi wao tukaurahisisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala la tatu nigusie katika suala zima la upimaji na usimamizi mzima wa ardhi; changamoto nyingi zimekuwa zikizungumzwa hapa kwamba mipaka imekuwa ina shida lakini pia upimaji hauendi kwa kasi. Lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kweli tumeona kuna maendeleo makubwa yamekuwa yakiendelea katika sekta nzima ya upimaji wa ardhi Tanzania na kwa kweli nimpongeze sana mpima na zaidi Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Upimaji ya Ardhi nchini, anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa na mapendekezo machache; kwanza, tukaangalie migogoro ambayo kwa kipindi kirefu imetamalaki Tanzania. Kuna mgogoro wa Tarime. Mipaka inajulikana toka mwaka1968 na wameenda watendaji kule wakiongozwa na mwenyewe mwenye hatimiliki ya kuainisha na kutafsiri mipaka Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, lakini ameondoka kule bado shida ameiacha iko vilevile. Lakini pia juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amenda Mbarali nako vilevile akaenda akatoa maeneo na maeneo yale kwa kweli maeno oevu, maeneo ya majimaji, ya chemchem, lakini pia tukawa tume–*risk,* tukawapa wananchi lakini alipoondoka yale maeneo ambayo tumekubaliana watu wakaanza kuvamia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hali kadhalika kuna hekta karibu 950,000 tumezitoa tukawapa wananchi na tumeyakata maeneo ya hifadhi, hifadhi nyingine tumeziondoa, hifadhi nyingine tumezimega tukawapa wananchi, lakini bado matatizo ya ardhi yanaendelea. Kwa hiyo, hapa tatizo la migogoro ya ardhi tuliweka kama ni suala ambalo litaendelea kwa miaka mingi itakayokuja. Tuweke utaratibu wa watu kuweza kwanza, kuwa wazalendo na kutii sheria hili la muhimu na tukiweka utaratibu Mheshimiwa Waziri

wa kwamba kila mtu tumridhishe kwa atavyotaka basi nchi nzima itakuwa ni kama vile uwanja wa mpira tunanyang'anyana tu mpira utacheza wewe kwa atakayekuwa na nguvu ndio atafunga goli, kama Mayele ana nguvu nzuri zaidi ana magoli 16 sasa. Kwa hiyo itakuwa mwenye nguvu ndio anashinda sasa unaona. *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi ninaloomba tuendeleze utii wa sheria kwa wananchi wetu. Mipaka ikishakutafsiriwa na Mheshimiwa Waziri ambaye ndio tumempa nafasi hii ya yeye ndio atafsiri mipaka ya ardhi ya nchi yetu, akishatafsiri basi pande nyingine ziridhike. Lakini leo Mheshimiwa Waziri unaitwa uende na timu yako wanakwenda sio kwamba ukafanye utatuzi, unaitwa uende ukatoe haki kwa upande ambao watu wangependelea uwape, siyo kwa sababu ya kwamba ukafanye haki kwamba tunavyoona mimi mpaka uko hapa, nyie kuweni huku. Kwa mfano, kama Tarime, Tarime Mheshimiwa Rais amefanya *favour* mpaka *buffer area* ya zile mita 500 zile amewapa wananchi, baada ya kusema kwamba nusu tuwape hifadhi na nusu tuwape wananchi Mheshimiwa Rais amesema zote wapeni wananchi. Ametoa *favour* kubwa lakini bado tatizo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba mipaka hii ya ardhi itaendelea kuwepo, lakini Serikali isimame katikati, itoe haki kama inavyohitajika na mimi nitoe ushauri nimalizie kwa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza huu mradi ambao wa usalama wa miliki za ardhi Mheshimiwa Waziri twende tukaushughulikie na tukausimamie ipasavyo, kwa sababu una malengo mazuri na mimi nimeusoma mradi mzima ule nimeusoma vizuri. Tunakwenda kuandaa hati milioni mbili kwa wakazi wa mijini na tunakwenda kuandaa hati 500,000 zile hati za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunakwenda kuandaa miundombinu ya kidijitali ambayo itarahisisha kufanya shughuli zetu kwa haraka. Sasa hivi ni 10% ya mradi tunaenda kupima, lakini tukiumaliza mradi tutakuwa tumeandaa miundombinu ya kuweza kusaidia upimaji kwa haraka zaidi na hivi Mheshimiwa Waziri ningependa sana utakapokuja hapa ukawaeleza wananchi huu mradi una tija kiasi ngapi? Kwa sababu wananchi wengi hasa Waheshimiwa Wabunge bado hawajaelewa pamoja na semina ambayo umetufanyia pale Msekwa bado hawajaelewa tija ya huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia tija ya matokeo ya huu mradi unakwenda kumaliza tatizo la upimaji wa ardhi nchini, unakwenda kumaliza tatizo la migogoro ya ardhi nchini. Hebu Waheshimiwa Wabunge wenzangu tumpe muda Mheshimiwa Waziri na timu yake wakatekeleze huu mradi kwa sababu tunasema huu mradi fedha nyingi zimewekwa kwenye uratibu. Uratibu ukijenga ofisi nao ni uratibu, ukienda kutayarisha miunombinu ya *communication* ikawa mawasiliano mikoa kwa mikoa nao ni uratibu. Isionekane kwamba labda shilingi bilioni 45 zinaenda kwenye uratibu kwamba hizi fedha labda ni watu watakuwa wakikaa kitako ndio wanatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naangalia mradi mzima sikuangalia lile jedwali la fedha tu. Nimengalia mradi mzima *in totality,* nimeona kwamba kwa kweli mradi huu una tija na Mheshimiwa Waziri tukiushughulikia basi utakwenda kutuvusha katika suala zima la migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, nilimuita Mheshimiwa Robert Chacha Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru, halafu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii asubuhi hii ya leo kwa kunipa pumzi ili niweze angalau kuchangia na mimi kwenye Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kuhusiana na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mimi leo nachangia kwenye jambo moja tu kubwa ambalo ni mahususi kwangu, linalohusiana hasa na kata ile ya Nyatwali ambayo wananchi wangu pale takribani 13,000 wanahamishwa kutoka katika eneo lile. Lakini wahusika ambao wanatarajia kuwahamisha wananchi hawa ni Wizara mbili, Wizara ya Ardhi ambayo ndio inafanya tathmini na Wizara ya Maliasili ambayo ndio yenye Mbuga ya Serengeti, hawa ndio wahusika wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi imepewa nafasi ya kufanya tathmini na kufanya *valuation* kwa ajili ya majengo ya wananchi wetu na kuwafanya ili waweze kupata stahiki zao vizuri. Wizara ya Maliasili ndio mlengwa na muhusika ambaye ndio anapaswa kuwalipa hawa wananchi wetu.

Nyatwali sasa jambo lile la wananchi wa Nyatwali kuhama kutoka katika kata yao ile ya Nyatwali ni jambo ambalo mimi nimelisikia kwenye mahusiano yangu zaidi ya miaka 20 leo na nimelikuta likiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sababu pia jambo hili limekaa muda mrefu sana kwenye vichwa vya wananchi wetu, kwanza lilishawaumiza kisaikolojia, wananchi walishapoteza *direction,* kwa hiyo, hata leo ukiwauliza wanananchi wa Nyatwali kwamba mnatakiwa kufanya nini?

Jibu la ndio wanaweza kusema hapana na jibu la hapana wanaweza kusema ndio kwa sababu lile jambo lilishawaumiza kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili tumeshawahi kukutana na Mawaziri pale walikuja kwenye kata yetu ya Nyatwali, Mawaziri wale nane. Walisikiliza maoni ya wananchi wao wenyewe kwa michango yao. Sasa jana niliona Mheshimiwa mmoja anachangia hapa anatoa taarifa kwamba wale wananchi wa Nyatwali wao walikuwa tayari kuondoka kwenye eneo lao. Mimi nasema hapana wananchi wa Nyatwali hawakuwa tayari kuondoka kwenye eneo lao isipokuwa wametakiwa kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametakiwa kuondoka kwa sababu ya manufaa makubwa ya nchi yetu. Kwa maana ya kuhakikisha kwamba ile Mbuga ya Serengeti imeongezwa kwenye eneo lao hilo ili Wanyama wetu wawe wanaenda kupata maji kwenye Ziwa letu la Victoria. Sasa wananchi wetu walioko pale Nyatwali wengi wameshaumia na sasa hivi akili yao imebaki tu Serikalini kwamba Serikali lazima itumie utu, kwa sababu wale wananchi ni wananchi wake, wanaipisha Serikali pale kwenye eneo lao ili Serikali ifanye uwekezaji wa kutosha pale ndio maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali imeenda kununua eneo kwa wananchi, siyo kwamba wananchi walivamia hapana. Inaenda kununua eneo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapokwenda kununua eneo kwa mwananchi ambaye yeye alikuwa hayuko tayari kununua eneo lake, siyo kwamba wewe unayekwenda kulinunua ndio unatakiwa kumpangia bei isipokuwa yeye mwneyewe anayetaka kuuza ndio atapanga bei. Sasa Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili inawapangia wananchi wa Nyatwali bei ya kununua eneo lao badala ya wananchi

wa Nyatwali wao wenyewe kupanga bei yao kwa yule anayetaka mali yao wamuuzie kwa bei wanayoitaka wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda mrefu wananchi wetu wa Kata ya Nyatwali wameridhia kukubali wakaona hakuna sababu ya kuendelea kubishana na Serikali wakasema walitoe eneo lao lile ili waache shughuli za Serikali ziendelee na shughuli za hifadhi zifanyike. Lakini pia ufahamu tu kwamba Halmashauri ya Mji wa Bunda ndio Halmashauri kubwa pia inayopata athari kubwa kupitia Mbuga ya Serengeti kwa wananchi wake, kwa sababu pale wananchi wanalishiwa mashamba yao na fidia yenyewe kutoka katika Wizara ya Maliasili na Utalii inaweza kuchukua miaka mitatu, bei yenyewe anayolipwa heka yake ya shamba ni shilingi 100,000. Lakini hiyo fedha mwananchi ataidai zaidi ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwananchi huyohuyo anayeishi pembezoni mwa Mbuga ya Serengeti, ng'ombe wake wakiingia kwenye Mbuga ya Serengeti kila ng'ombe mmoja atakuwa–*charged* kwa shilingi 380,000 kila ng'ombe aliyekanyaga kwenye Mbuga ya Serengeti. Huku yeye heka moja ya shamba analipwa shilingi 100,000 tena kwa kuidai kwa muda wa miaka mitatu.

Sasa mimi nilikuwa nawaomba watu wa Wizara ya Ardhi na Maliasili wale wananchi wa Bunda wakihamishwa kwa viwango vyao hivi walivyovipanga, pamoja na umaskini wao walionao watu wa Nyatwali, watazidi kuwaongezea umaskini mara tano Zaidi kuliko vile walivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu wale wanachi wa Nyatwali na wao Mbuga ya Serengeti ni mali yao, wala sio mali ya mtu mwingine, ni mali yao, kwa hiyo wanapisha ili wao wafanye maendelezo kwneye mali yao. Sasa kama wanapisha kwa nini wasilipwe fedha stahiki

zinazoweza kuwafanya waridhike kwamba mali wanayoiondokea pale ili wanufaike nayo ni mali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wafanya tathmini wale wa Serikali walioko pale, wanafanya tathmini kwenye majengo ya wananchi wetu. Nyumba zile ni nyumba zimejengwa toka miaka ya 1968, leo wale wananchi wanaambiwa wahame kwenye eneo lile ambalo wamekaa toka mwaka 1968.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mwaka 1968 mpaka leo kwamba yule mwananchi alijenga nyumba yake ya majani. Kipindi hicho majani ya kukata kwa mikono yalikuwepo maeneo hayo, leo hii majani yale hayapo, halafu unamwambia leo huyo mwananchi utamfanyia *valuation* kwenye nyumba yake ya majani, utamlipa fedha kulingana na nyumba yake ya majani halafu yeye ataenda huko atakapokwenda, ataenda kutafuta majani aezeke nyumba yake kwa majani atayatoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, kila mwananchi, kila raia wa nchi hii sasa hivi kule alikokuwa anataka kutoka ili aende mahali pengine, hivi leo unawezaje kumfanyia *valuation* mwananchi kwenye nyumba yake ya majani, halafu ukamwambia ukitoka hapa ukajenge nyumba ya majani hiyo hiyo wakati kila mmoja anatakiwa kufanya kila jitihada akajenge nyumba ya bati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Utalii, wananchi wa Kata ya Bunda Mjini, wananchi wa Kata ya Nyatwali katika Halmashuri ya Mji wa Bunda, lolote litakalowapata katika haya, machozi yao yatabaki Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ardhi. Wale

wananchi wameshaumia kwa kiasi kikubwa, ni mategemeo yangu, ni maombi yangu na tumeshazunguka nao mara kadhaa kila sehemu kwenda kupeleka jambo hili kusema ili Serikali iweze kuwasikia, lakini bado jambo halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe watu wa Wizara ya Maliasili na Ardhi wahakikishe kwamba wanawatendea wananchi wa Nyatwari haki yao ili wapate fedha stahiki ambazo zinaweza kuwafanya pale wanapotoka na huko wanakokwenda wakanunue eneo, na kwa sababu katika kuwahamisha kwao pale hawakuwatengea eneo maalum ambalo watakwenda kuishi wao wanawalipa fidia, wanawaambia nenda mtanunua ninyi wenyewe huko mnakokwenda kitu ambacho ukija kuangalia kwa sasa hivi mfano kwa mazingira ya sasa hivi ndoa nyingi baba na mama wanaishi, lakini hawako pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo fedha zile zinaenda zinawekwa kwa baba aidha zinawekwa kwa mama kati ya hawa wawili mmoja anaweza akaondoka nazo halafu wale Watoto wakabaki wanarandaranda pale mjini na hawatapata sehemu nyingine ya kwenda. Hawa watakapokuwa wanaanza kulia watakuwa wanaililia Serikali kwa sababu Serikali ndio ilichukua eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna wajane, kuna nini na watu wengi unajua Watanzania wameshaathirika kisaikolojia sana wale wananchi, Serikali ikapata eneo maalum ambalo itawapeleka wale wananchi wa Nyatwali, hautakuja ukaa ukasikia Kata ya Nyatwali na ukajua raia yoyote wa Nyatwali baada ya kuwa wamelipwa walihamia wapi hutakuja kukaa ukapasikia eneo hilo, kwa sababu watakuwa wamepotea katika mazingira ambayo hayawafanyi wao waende kutafuta sehemu nyingine ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia wanayopewa ni kidogo sana, nimuombe sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu

Hassan anaamini kutokana na michango mingi ya Wabunge wenzangu hapa ameliona na amelisikia jambo hili alishike na alifanyie kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Robert Chacha Maboto kwa mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimuita Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, wakati huo Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, wanajiandaa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama hapa na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa niipongeze Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri sana ambayo wameiwasilisha katika Bunge hili na nipende kusema jambo moja Wabunge tunapochangia tuangalie Kamati yetu imetuelekeza wapi kwa sababu hawa wenzetu ndio wanaojua mambo yote yanayoendelea katika wizara hii kwa sababu ndio wanaofanya nao kazi wakati wote. Kwa hiyo, tunavyotaka kuishauri na kuisimamia Serikali tujaribu kuangalia wenzetu wamesema nini? Kamati ndio Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kupitia taarifa ya Kamati ya Bunge na nimeona ni kwa namna gani

ambavyo Wabunge wenzetu wameweza kuchanganua na kufafanua yale yote ambayo waliyoyasema katika hotuba aliyosoma Mwenyekiti. Nikupongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii ndugu yangu Mnzava kwa kazi nzuri na kubwa uliyoifanya na wajumbe wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa kwenye Kamati hii kwa kipindi cha miaka miwili na nusu ninaijua vizuri sana, na ninaamini yale uliyoyaandika siyo majungu ndio ukweli uliopo na uhalisia na unachofanya ni kuisaidia Serikali ili iweze kutekeleza majukumu yake, ili iweze kuondoa migogoro inayowasumbua Watanzania kwenye maeneo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za ardhi katika nchi yetu ni nyingi sana na kila siku ni afadhali ya jana, unapomuona Mbunge anasimama anazungumza kwa uchungu anajua ni namna gani wananchi wake wanapata adha na shida kubwa ya ardhi. Tunapozungumzia suala la kupanga matumizi bora ya ardhi siyo kwa sababu tuna kitu tunachokitaka zaidi ya kwamba tuondoe migogoro kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inayo Tume na nimwambie Mheshimiwa Waziri ana Tume nzuri sana, ina watendaji wazuri kweli kweli, hawa watu wakipewa mshiko, wakipewa fedha wanaenda kufanya kazi kweli kweli. Mimi hapa leo ninavyozungumza katika Mkoa wangu wa Tabora fedha kidogo walizopewa wameshakwenda kwenye vijiji zaidi ya 16 mpaka sasa ninavyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Tume, tulikuwa na mgogoro mkubwa sana wa vijiji katika Jimbo la Igalula, Kata ya Kizenga kuna vijiji viwili mgogoro umedumu pale kwa zaidi ya miaka nane, lakini wamekwenda juzi wamemaliza mgogoro ule kwa sababu ulikuwa kila siku unawafanya watu wanafungwa, unawafanya watu

wanapelekwa mahabusu bila sababu zozote. Mimi ninavyozungumza hapa Mwenyekiti wangu wa Kijiji wa wakati huo mwaka 2017 aliwekwa ndani kwa sababu ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri na Wizara yake asifikiri Wabunge wanaposimama na kuzungumza masuala ya kupanga matumizi bora ya ardhi tunazungumza tu, lakini tumeona na tunajua faida ya kutoa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yetu tumechoka kufiwa kwa sababu ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanalia kila leo kwa ajili migogoro ya watu wanauana na mimi nafikiri na nilisema hii migogoro huenda inanufaisha Wizara kwa namna moja ama nyingine, kuna manufaa wenzetu ambayo wanayapata kwa sababu haiwezekani kama hakuna manufaa wasisikilize haya ambayo tunasema na wanayaona na wanayajua, lazima wafike mahali wajue kwamba migogoro ya ardhi inachosha na niwaambie niwakumbushe tu...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Nimemuona Mheshimiwa Waziri.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atajibu anamaliza muda.

**MWENYEKITI:** Naomba upokee Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, karibu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hawa siyo kwamba namaliza muda.

Ninakushukuru sana na ninakupongeza kwa kuisifia Tume kwa kumaliza huo mgogoro, ili kusaidia Bunge hili lijue kwamba Wizara ya Ardhi haina manufaa yoyote na migogoro hiyo Tume inafanya kazi chini ya Wizara ya Ardhi, kwa hiyo kama unaona kuna mafanikio yoyote yamepatikana kupitia kwenye hiyo Tume ni kwa sababu Wizara ya Ardhi imeisimamia vizuri Tume, ni kwa sababu ya Serikali imeisimamia vizuri Tume. Kwa hiyo, naomba nikupe tu taarifa kwamba hivyo vitu vyote ni taasisi za Kiserikali na ni Serikali inayofanya hiyo kazi nzuri kwa pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwaifunga unapokea taarifa

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sijakuruhusu.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anhaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amenielewa Dada Jenista na anachokisema ina maana anakubaliana na mimi, migogoro ikiondolewa ina maana migogoro ikiondolewa hawa wa Tume wakipewa fedha ina maana hakutakuwa na mazingira yoyote ya watu wetu kufa kwenye maeneo yetu na ndichi hiki ambacho nimekisema kwamba inawezekana kuna baadhi ya migogoro inawanufaisha na hili silifuti ndio ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa baadhi ya Makamishna ambao wako kwenye mikoa yetu mbalimbali. Mimi nimpongeze Kamishna wa Ardhi amefanya kazi kubwa sana, amechukua ushauri

vizuri sana wa Kamati, tulimuomba Mheshimiwa Kamishna atusaidie labda kufanya *rotation* ya hawa Makamishna inaweza ikasaidia kwa kiasi fulani kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa na Kamishna katika mkoa wangu wa Tabora tunamshukuru sana amefanya kazi kubwa sana, sasa hivi kuna maeneo kwa kweli husikii migogoro, Wabunge sasa hivi kuna maeneo tumepumzika kusikiliza migogoro Kamishna aliyekuwepo, lakini hata huyu aliyeletwa sasa ninaona anaendeleza kazi ambayo imefanywa na mwenzake aliyetangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo mengi yana migogoro ukiwepo Mkoa wa Dodoma, Dodoma yaani ni kasheshe. Kwa hiyo mimi nimuombe sana Mheshimiwa Waziri hawa Makamishna mliowafanyia *rotation,* wapeni muda waweze kufanya kazi, waweze kuonesha kile ambacho mnakitaka sasa, kama mmeamua kupata mabadiliko kwenye Wizara kupitia hawa Makamishna, wapeni muda, wapeni ushirikiano waweze kufanya kazi ili muweze kuona matunda yao, mkiweka au kuhamisha watu bila kuangalia kwa nini mnawahamisha mnaharibu na matokeo yake huyu anamlaumu huyu na huyu anamlaumu huyu, mwisho wa siku migogoro inakuwa haipungui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba na nizungumze kidogo kuhusiana na hili suala la hii fedha ya mkopo na Kamati imefafanua vizuri sana. Mikopo tunapokwenda kukopa Serikali ninyi mnakwenda kwa niaba yetu sisi Watanzania kwa sababu mwisho wa siku hamlipi ninyi hiyo mikopo ni sisi Watanzania tunalipa kupitia kodi zetu. Sasa kama unapewa mkopo una masharti ambayo unayaona hayana manufaa kwa Watanzania una sababu gani ya kuchukua mkopo huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichukua mkopo hapa wa trilioni 1.3; Mheshimiwa Rais alipata huu mkopo na masharti

ya mkopo huu ilikuwa tununue barakoa na *sanitizer.* Trilioni 1.3 Mheshimiwa Rais aliona hivi trilioni 1.3 naenda kununua barakoa na *sanitizer* wakati kuna watoto wanakaa chini, wakati kuna watoto wanasoma chini ya miti, wakati kuna wanawake wanajifungulia majumbani, wanawake wanajifungua barabarani, kwa nini mkopo usiwe wa kuweza kusaidia Watanzania kule walipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkopo wa trilioni 1.3 tumeona manufaa yake, kila unapokwenda kwenye majimbo kuna madarasa yamejengwa, kila unapokwenda kwenye majimbo yetu kuna zahanati na vituo vya afya vimejengwa, leo tunapozungumza hapa tunalalamikia vitu vidogo vidogo, siyo majengo tena, je, mama angechukua huu mkopo akaenda kununua *sanitizer* na barakoa tungekuwa tunagaragara nazo tu hapa Bungeni kwa sababu hazina kazi, *corona* imeshakwisha au kama bado ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkopo wa trilioni 1.3 fedha ya uratibu iliyotumika, *monitoring and evaluation* hawa walitumia bilioni tano tu, katika trilioni 1.3 walitumia bilioni tano peke yake, lakini wenzetu wamechukua bilioni 345 uratibu peke yake wanatumia zaidi ya bilioni 47, hatukatai kwamba wanaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Watanzania wanauana kwa sababu ya ardhi nani atakwenda kwenye Ofisi za Ardhi hizo ambazo mnataka kuzijenga? Leo mnachukua fedha eti mnaenda kununua *furniture,* ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge niwambie leo tunapokaa tunazungumza hapa Watanzania wanatuangalia na wanatuona, mwaka 2025 *is around the corner,* hakuna mtu atakayekuja kukusaidia kwenye jimbo lako utapambana mwenyewe. Mheshimiwa Jenista kakaa pale ataenda Peramiho, mimi nitakuwa Tabora hakuna atakaye kuja kunisaidia lazima nipambane na hali yangu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema huu mkopo lazima uangaliwe ili uendane na tija kwa ajili ya Watanzania na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, nilimwita Mheshimiwa Festo Richard Sanga wakati huo Mheshimiwa Dunstan Kitandula anajiandaa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii, jambo la kwanza nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kuhakikisha masuala kwenye Wizara ya Ardhi inakwenda vizuri, lakini pili nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na kwa moyo wa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri nakushukuru pamoja na Wizara ya Maliasili, tulikuwa na mgogoro uliochukua takribani miaka karibu kumi pale Kata ya Mfumbi, Wilaya ya Makete ulikuwa na changamoto kati ya Mpanga Kipengele na wananchi wa Mfumbi. Tunapozungumza haya ni kabisa wananchi wangu wanawashukuru sana kwa sababu mgogoro ule umeenda kutatuliwa katika ekari milioni 2.3 ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa kwa wananchi na sisi Wanamakete tumenufaika kwenye eneo lile, wananchi wale wanawashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Makete tunawashukuru kwa haya yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nipende kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara hii *Engineer* Anthony Sanga kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na kwa kweli kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii tunafahamu *Engineer* Anthony Sanga

saa hivi yuko na jukumu la kuhakikisha kwamba mifumo ya ulipaji wa kodi kwenye Wizara hii yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Katibu Mkuu na tunategemea kwamba suala la kwamba mfumo uko chini, watu wanashindwa kupata hati kwa wakati, litakuwa limeisha kwa sababu kote alikopita Anthony Sanga ameacha rekodi nzuri ya utendaji, kwa hiyo tiunaamini kabisa kwamba atatusaidia kwenye Wizara hii na mimi niamini kabisa kwamba kwa sisi Wanamakete tunajivunia kuwa na mtumishi ambaye anafanya kazi vizuri kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kumpongeza Mkurugenzi wa *National Housing*, Ndugu Hamad Abdallah, unajua Watanzania hawafahamu sasa hivi umekuja mfumo mpya wa *PPP* kwenye ujenzi wa hizi nyumba za *National Housing* na Mkurugenzi ameshatuonesha kwamba kuna viwanja kadha wa kadha kwenye Taifa letu na vipo kwenye eneo *potential* kama Kariakoo na maeneo mengine ambapo Watanzania wanaweza kushiriki kujenga nyumba hizi ambazo zinaweza kusaidia kwenye ukuaji wa sekta binafsi, lakini pia kwenye Shirika letu la Nyumba, kwa hiyo nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo yangu mawili, la kwanza ni tuna migogoro mingine Mheshimiwa Waziri ndani ya Wilaya ya Makete, tuna mgogoro kati ya Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya kwenye eneo la Mbarali kwa maana Kata ya Mfumbi. Watu wako kutoka Wizarani walifika kwenye eneo husika wakaainisha eneo la mipaka, lakini changamoto iliyopo ni kwamba hamjaweka *beacon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuweka *beacon* kumesababisha bado mgogoro uendelee kuwepo na hili ilitupa changamoto kubwa Mheshimiwa Waziri kwenye anuani na makazi, tuna vijiji zile anuani za makazi hazijawekwa kwa sababu ya mgogoro wa mpaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba mgogoro kati ya Mbeya na Njombe eneo la Chimala, eneo la Mbarali uweze kukamilishwa kwa kuweka *beacon* ili wananchi wa Makete wajue mpaka wao ni upi na wananchi wa Mbarali wajue mpaka ni upi ili tuondoe changamoto ya migogoro ambayo sisi Wanamakete tumeanza kuipata ya wafugaji kutoka Mbarali kuingia kwenye Jimbo letu la Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mgogoro mwingine upo kati ya Njombe na Mbeya kwenye eneo la Kikondo ambapo huko nyuma ilikuwa ni kati ya eneo la Hifadhi ya Kitulo na baadae tukawaondoa wananchi likabaki kuwa eneo la Makete, lakini kuna changamoto pale kati ya wananchi wa Makete na wananchi wa Mbeya Vijijini, tunaomba mtusaidie kwa ajili ya kutatua mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mkitusaidia sisi Wanamakete tutashukuru sana ili shughuli zetu za kiuchumi ziweze kwenda vizuri na shughuli zetu za kiuchumi kwa wananchi wetu ziweze kwenda vizuri na niseme wazi kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri suala la ardhi ndio suala mtambuka kwenye Taifa letu ambalo linaweza likatatua migogoro mingi sana. Sisi hatukuwepo na migogoro hii ya wafugaji na wakulima, sasa imeanza kujitokeza kutokana na kwamba matumizi bora ya ardhi yamekuwa ni changamoto na hayajafanyika katika Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ni kwenye suala la huu mkopo wa bilioni 350; Mheshimiwa Waziri na hii *is for the good* na ni kwa maslahi mapana ya Taifa letu, Taifa la Tanzania, Mheshimiwa Waziri tusaidie jambo moja tu hizi bilioni 350 Watanzania wanatusikiliza huko nje unapozungumza kwamba kwenye bilioni 350 kwenye uendeshaji tumekwenda kuweka bilioni 2.4, kwenye uratibu tumeweka bilioni 29 na kwenye dharura tumekwenda kuweka bilioni 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hata kwenye vikao vya harusi siku hizi wameacha kuweka kitu kinaitwa *contiguous* kwa maana ya fedha ya dharura kwa sababu unapoweka fedha ya dharura kwenye eneo lolote lile una-*rise doubts* kwa sababu unapoweka hela ya dharura wakati kuna uhitaji wa fedha kwenye Tume ya Mipango kuhakikisha maeneo yetu ya ardhi mengi yanapimwa nchini, lakini unafedha ya dharura ya bilioni 17; hii dharura ni dharura ipi ambayo inaweza kwenda kutokea na ikatumia fedha zote hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposhauri Mheshimiwa Waziri tunashauri *for good,* kwa sababu Watanzania wanatusikiliza na sisi ni Wajumbe wa Kamati, hizi bilioni 17 tungeweza kuwapa Tume ya Mipango wakatusaidia kupima ardhi kwenye maeneo mengi zaidi kuliko haya ambayo mmeyaainisha na Mheshimiwa Waziri wanapozungumzia bilioni 47 kwamba ziko kwenye uratibu, kwenye udharura na kwenye uendeshaji; trilioni 1.3 ya Mheshimiwa Rais tulitumia bilioni tano tu kwenye kuratibu mkopo mzima wa trilioni 1.3 kwenye mkopo wa *Covid.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni jambo jema kama mtachukua hatua kuhakikisha kwamba fedha hizi bilioni 17 au bilioni 47 zinaenda kufanya kazi iliyokusudiwa. Mheshimiwa Waziri haileti tija na haina mantiki kwa mwananchi yeyote yule awe ameenda shule au hajaenda shule katika mkoa wa bilioni 350 tunaenda kutumia bilioni kumi tu kupima ardhi ni sahihi? *(Makofi)*

Ni sahihi Mheshimiwa Waziri? Unaweza ukazungumza kwamba tunakwenda kusimika mitambo, tunaenda kujenga nyumba, si tunataka tuangalie kipaumbele chetu kama nchi ni kipi? Ni kutatua migogoro ya ardhi au ni kujenga nyumba? Kwa sababu nchi hii ina majengo ya halmashauri sehemu zote ambapo tunaweza tukatumia ofisi za halmashauri

tukafanyia kazi hii, tukapima ardhi yetu hizo nyumba zikafuata baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna uhitaji mkubwa wa kutumia hela nyingi kwenye…

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna haja ya kutumia fedha nyingi sana kwenye kujenga nyumba na hivi vitu vingine ambavyo mmevizungumza tukaacha kupima ardhi yetu.

Mheshimiwa Waziri kipaumbele cha Taifa na cha Mheshimiwa Rais ni kuona migogoro ya ardhi kwenye Taifa letu inaisha na sio kuhakikisha kwamba kila ofisi au kila mkoa au kila wilaya imejenga ofisi ya ardhi. Hiyo sio kipaumbele chetu, kwa sababu gani Mheshimiwa Waziri? Sitaki kuamini kwamba hadi dakika hii Maafisa Ardhi wa Wilaya wanafanya kazi chini ya miti maana yake wanamaeneo yenye ofisi. Kwa hiyo, huu mkopo ungekuwa na tija endapo ungeelekezwa kwa kiwango kikubwa kwenda kupima ardhi. Mheshimiwa Waziri tulikuwa wote pale Arumeru Mashariki… *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga pokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe Mheshimiwa Sanga taarifa kwamba kwa maneno ya msingi anayoyazungumza na kwa uzalendo ninaoujua kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Ardhi, nina imani kabisa kwa uzalendo nimeshafanya naye kazi, ninajua ushauri

wa Mheshimiwa Sanga ataupokea Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga unapokea taarifa hiyo aliyokupatia Mheshimiwa Kingu?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa moyo mzuri kabisa, kwa nini kwa sababu *in their records* wanajua kwamba Kamati ya Bajeti iliwashauri kuhusu mradi, Kamati ya Maliasili na Ardhi tunawashauri kuhusu mradi na sisi ni Bunge na sisi ndio Watanzania walioko nje tunasimama kwa niaba yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunachokizungumza hapa hatuzungumzi *for bad,* tunazungumza kwa jambo jema tu. Ngoja nikupe mfano kwenye Halmashauri ya Arumeru Serikali ilikopesha bilioni 1.6, Halmashauri ya Arumeru inaenda kuzalisha bilioni nane na imeshalipa na deni lote. Maana yake tukipima ardhi kwa kiwango kikubwa tutaingiza fedha nyingi kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ni Wizara mtambuka, hii Wizara inafanya *parallel* na Wizara ya Kilimo, hii Wizara inafanya *parallel* na Wizara ya Maliasili na Utalii. Leo hii Mheshimiwa Rais ameshusha mikopo ya kilimo kuja kwenye *single digit* kwa maana kwa asilimia tisa. Ukienda NMB, ukienda CRDB mikopo imeshuka, sasa mkulima hawezi kukopesheka kwa sababu ardhi yake haijapimwa. Kwa hiyo, hatuwezi kuwekeza bilioni 350 kwenye eneo ambalo linaenda kwa ajili ya kujenga ofisi, kusafiri, kununua nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi si kwamba haina magari, ina magari, ina ofisi, inavyo vyote. Nimuombe Mheshimiwa Waziri *this is for good, this is for your record,* utaondoka kwenye Wizara hii, utaandika kitabu chako kama Mzee Mwinyi alivyosema cha kwamba ulifanya jambo kubwa la kupima ardhi kwenye Taifa letu, kutoka kwenye asilimia 23

zilizopimwa kwa sasa ukafika zaidi ya asilimia 50 kwa kutekeleza Ilani ya CCM na kwa kuokoa mauaji yanayoendelea Tanzania kutokana na migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri tunaamini wewe ni mtu rahim, wewe ni mtu mwema, wewe ni msikivu, wewe ni mtu ambaye hutashupaza lolote kwamba sisi labda tuna nia mbaya kwa ajili ya hili, *no this is our money,* ni mkopo ambao wananchi wa Makete, mwananchi wa Bulongwa, mwananchi wa Iwawa, mwananchi wa Karagwe, mwananchi wa Mpanda, mwananchi wa wapi atalipa fedha hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunasimama kwa niaba yao ili bilioni 350 zikapime ardhi na sio bilioni 47 ziende kwa ajili ya kusimika mitambo ya ofisi wakati nchi yetu ina ofisi kila kona.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ahsante, naamini Mheshimiwa Waziri ametusikiliza, naamini kabisa nimewawakilisha wananchi, mawazo ya wananchi wa Makete na mawazo ya Watanzania kwamba ….

*(Hapa kengele ililia kiashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Kwa maslahi yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MWENYEKITI:** …Mheshimiwa Festo Richard Sanga kwa mchango wako, nilimwita Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula wakati huo Mheshimiwa Boniphance Mwita Getere anajiandaa.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kuendelea kutulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la mipaka katika eneo letu la bahari, tuna changamoto kule Mkinga kwenye mpaka wetu na Kenya na changamoto hii ni ya miaka mingi. Mheshimiwa Waziri nafurahi uliwahi kuja Mkinga tukatembelea mipaka yetu kwenye ukanda wa ardhi, lakini tukaenda vilevile Kijiji cha Jasini kwenye ukanda ule wa baharini, uliziona changamoto zetu, nakumbuka ulifika kwenye nyumba ile upande mmoja ni Kenya na upande mmoja ni Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yetu kubwa, hili la watu kujenga mpakani kabisa tunalisema kiutani utani hivi, lakini athari yake ni kubwa. Niliwahi kusema hapa kwamba wenzetu wa vyombo vya ulinzi vya Kenya wanafika mpaka ndani ya maeneo ya kijiji chetu wakiwa na silaha. Nikasema ni hekima tu za viongozi wa Serikali wakati ule vilisaidia tusiingie kwenye mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja tena leo kwa unyenyeku mkubwa naiomba Serikali yangu itusikie. Mwaka 1972 kilifanyika kikao cha kujadili jambo hili la mgogoro wa mpaka, tarehe 8 Mei kikao kilifanyika pale Mombasa; tarehe 4 Septemba, 1975 tulifanya kikao Dar es Salaam; tarehe 9 Julai, 1976 Mawaziri wetu wa nchi mbili hizi aliyekuwa Waziri wetu wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Ibrahim Kaduma na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya Dkt. Munyua Waiyaki walisaini *document* ya makubaliano inayoonesha mambo kadhaa na *document* ile niliwahi kuileta Wizara na leo tena nitaiweka mezani ili iwe rejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na makubaliano yale kupitia *document* hii bado kumekuwa na chokochoko

hizo. Vyombo vya ulinzi vya Kenya vikiingia kwenye eneo letu, wananchi wetu wa Jasini wanapoenda kuvua wakikamatwa baharini wakapelekwa Kenya kwenda kufunguliwa kesi, mali zao zikataifishwa. Sisi kama Taifa lazima jambo hili tulichukulie kwa uzito mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwneyekiti, maboya tuliyoweka ya mipaka kule baharini yameharibiwa, sitaki kusema ni makusudi, lakini nasema yameharibiwa. Wakati hali ikiwa hivi nataka niikumbushe tu au niiambie tu Serikali kwamba kwenye ukanda huu tuna leseni ya utafiti wa mafuta, kwenye ukanda huu tuna leseni ya utafiti wa madini, madini ya kimkakati baharini, lakini wakati hali ikiwa hivi kwenye mpaka wa Kenya na Somalia ambapo kuna dalili zote za kupatikana mafuta kuna mgogoro sasa hivi kule, sijui naeleweka? Tusingoje utafiti utuambie tuna mafuta halafu tushindwe kuyachimba. Tusiache kuchukua hatua watu wetu badala ya kwenda kuhukumiwa Kenya ikafika mahali vyombo vyao vikazamishwa baharini tukapoteza maisha ya watu wetu, nawaomba tuchukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili Mheshimiwa Waziri ni jambo ambalo nimelizungumza katika kipindi chote cha Ubunge wangu ni shamba la kwa Mtili, zaidi ya miaka kumi nalizungumza jambo hili. Miaka kumi na zaidi nalizungumza jambo hili, kuna shamba pale limetelekezwa na anayejiita mwekezaji, zaidi ya miaka 25 limetelekezwa. Huyo mwekezaji hayupo, wameshafariki, wapo tu watu wanasimamia kiujanja ujanja pale wakiwakodisha wananchi wetu kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilituagiza mwaka 2012 ikatumwa ilani ya kufuta shamba lile, lakini ikaonekana ina makosa mwaka 2017 ikatumwa ilani nyingine, mlipotupa shamba lile la kule kwenye kata kule ambapo kipo Kijiji cha Jasini, Kata ya Mahemboni kule nikawaambiwa kuna shamba lingine, tunaomba na hili mlishughulikie, aliyekuwa Waziri wakati ule Mheshimiwa Lukuvi akatuma timu kwenda

kufanya uhakiki. Ikaonekana ni kweli, imetumwa ilani, baadaye ikaonekana imetumwa kimakosa kwa sababu kalitumwa kaeneo kadogo, ikatumwa timu nyingine kutoka Wizara ikaja kufanya tathmini, mkajiridhisha kwamba shamba lile limetelekezwa. Ikatumwa ilani nyingine, lakini baadaye ikaambiwa eti huyu jamaa miaka ya 1960 alichukua mkopo mahali huko nje, kwa hiyo tukatuma ilani nyingine kwenye hizo benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilani hizi zimepita zaidi ya miezi saba sasa au nane Waziri unalijua jambo hili,…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Nimekuja kwako ukaniambia watu wa mkoani wamechelesha, watu wa mkoani wamekamilisha kazi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kitandula naomba upokee taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mnzava.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kaka yangu mzungumzaji anayezungumza, pamoja na mchango wake mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumpa taarifa kwamba jambo hili la kupeleka ilani, lakini utekelezaji hauonekani na tunakaa kwa muda mrefu kusubiri sio tu kwa yale mashamba ya Mkinga, hata Korogwe, shamba la Mwakinyumbi zaidi ya miaka saba kila siku ilani zinatengenezwa, utaratibu unakamilika, lakini ufutaji au ubatilishwaji wa miliki mpaka leo haujafanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula unapokea taarifa?

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii kwa sababu katika mkoa ambao una changamoto ya ardhi ya mashamba makubwa ya mkonge na mengine yaliyotelekezwa, Korogwe, Mkinga, Muheza tuna changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, ndugu zenu tunapowaambia tusaidieni, kwa hiyo nimeambiwa kwamba taratibu zote zimekamilika jambo hili lipo Wizarani, Wizara naomba mchukue hatua. Wapo watu kule wanazunguka zunguka wanakuja kutafuta fursa tuwaunge mkono kwa sababu yule mmiliki amejua hana ujanja, anataka kuuza eneo lile, tunaomba mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, ni lile ambalo kila mmoja wetu analisema, nimeisikiliza taarifa ya Kamati, wote tunajua Kamati ndio inafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Kamati inaposema kwamba leteni hayo maamuzi kwenye Kamati tuyajadili wanasema kiustarabu tu kwamba hawaridhishwi kuna jambo linakwenda sivyo. *(Makofi)*

Naomba muisikie Kamati, tulijadili jambo hili, sisi sote ni viongozi tumeaminiwa na wananchi tusikilizane. Tukifanya maamuzi tuyafanye maamuzi kwa manufaa ya Taifa letu. Mheshimiwa Waziri ushirikishwaji unaujua ulivyo na tatizo, unajua timu ile ya Mawaziri ilipokuja Tanga mimi nilishiriki kikao kile kwa namna gani unajua. Sitaki niseme nilivamia, lakini unajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasikia kuna timu huko Mkinga inaendelea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Naomba tuwashirikishe wananchi, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitandula.

Tunaendelea na uchangiaji, lakini naomba niwatambulishe wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; moja ni wageni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, wanafunzi 34 na walimu sita kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Ujenzi ya Jijini Dodoma, wako wapi? Wanafunzi 34, karibuni sana wanafunzi na walimu wetu sita, ooh kutoka Mkuranga. *(Makofi)*

Naona Mheshimiwa Ulega ilibidi asimame mwenyewe kuhakikisha kwamba *Hansard* inakaa vizuri. Kwa hiyo naomba isomeke kutoka Mkuranga sio Dodoma, karibuni sana wanafunzi na walimu kutoka Jimboni kwa Mheshimiwa Waziri wetu. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo, hawa ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Zuzu kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi pamoja na walimu wetu. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni wa Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia hawa ni wanafunzi 95 na walimu tisa kutoka Shule ya Awali ya Msingi Zamzam ya Jijini Dodoma, ahsante sana wanafunzi pamoja na walimu, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wazalishaji na wasambazaji wa Dawa ya Meno Ndugu Isha kutokea Jijini Dar es Salaam, karibuni sasa Dodoma. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Dodoma. Wageni wa Mheshimiwa Shangazi, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo hapa tunao wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi ya Fransalian iliyopo Jijini Dar es Salaam, wanafunzi 90, karibuni sana. Wanafunzi wetu 90 pamoja na walimu wao 10, wako wapi walimu tuwaone? Ahsanteni sana. Hawa ni Shule ya Msingi ya Fransalian ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na uchangiaji nilimwita Mheshimiwa Boniphance Mwita Getere, wakati huo Mheshimiwa Mary Masanja - Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa TAMISEMI wanajiandaa.

**MHE. BONIPHANCE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara ya Ardhi.

Kwanza nawashukuru Wizara kwa maana ya Waziri, Naibu, Makatibu wake na wote walioko hapo kwenye maeneo ya ardhi kwenye Wizara ya Ardhi. Nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kweli kimsingi toka Rais amekamata hii nchi imekaa vizuri sana na inakaa vizuri inaendelea vizuri. Mheshimiwa Rais amefuata misingi ya Baba wa Taifa, anaijenga nchi katika misingi isiyo ya matabaka na wale wanaohubiri matabaka watakuja kuona kwamba hii nchi imejengwa kwa matabaka na haiwezi kuwa matabaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mtaniwia radhi tu yaani tu, yaani kusema lazima niseme tu. Katika Wizara sielewi kabisa ni Wizara ya Ardhi yaani sielewi, yaani sielewi, yaani sielewi naanza moja/mbili wapi, sielewi yaani ni Wizara ya

Ardhi na kusema kweli kipindi hiki naunga mkono ila bajeti ijayo nitakuja na hoja binafsi ya kuichunguza Wizara ya Ardhi.

Kabisa yaani sielewi, haitokei kichwani yaani. Wizara ambayo ina Mkurugenzi wa Ardhi, Kamishna wa Ardhi, Katibu Mkuu Ardhi, msaidizi gani - ardhi. Wana mipango, wana wasomi, wana maprofesa, wana makamishna wa mikoa, wana wa ardhi wa wilaya. Hakuna migogoro mahali popote imeisha, yaani hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mabula mimi niulize swali; hivi kweli kwa mfano ulikuwa Naibu, umekuwa Waziri, hivi kweli hata kwenye majiji yetu basi, tuseme leo Dar es Salaam migogoro imepungua imebaki asilimia labda 10, 15; Jiji la Mbeya imebaki lazima asilimia ngapi; Jiji la Mwanza yaani hakuna mahali unaenda ukute ardhi sasa imepunguza migogoro. Sasa tunajiuliza, sasa humu ndani kuna nini kinaendelea? Nenda kwenye mipaka ya nchi migogoro, mipaka ya vijiji migogoro, kila mahali migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jamani mambo gani haya? Kwa kweli mimi niombe na nikuombe mama yangu nikuombe kwa kweli ujitahidi. Mimi nadhani kuna matatizo kwenye hii Wizara na matatizo makubwa ni mipango ya Wizara hii. Sijui kama inaenda vizuri, sielewi yaani sielewi kama inaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano mimi nikienda benki nataka kufanya biashara, mimi ni mfugaji labda nataka kufanya biashara ya ng'ombe wakanipa shilingi milioni 300 halafu milioni 300 nikapita barabara nimetoka Dar es Salaam nikatamani gari nikanunua shilingi milioni 200. Jamani, mambo ya ajabu haya. Mmepewa shilingi bilioni 350, badala ya kwenda kupima viwanja mpewe hela za kudumu miaka yote, mnajenga majengo. Hayo majengo si yapo? Yako pale Bunda yamejengwa, majengo ya ardhi yapo, yako kila mahali. Juzi juzi hapa mmejenga mmetengeneza mtandao

pale Dar es Salaam mzuri kabisa mmepewa sijui mkopo kutoka nje. Migogoro imeisha? Mimi nadhani kuna shida, kuna shida.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri ufanye kazi ya kutosha kwenye Wizara yako. Ukiona imekushinda, hivi kwetu hapa hakuna mtu kujiuzuru? Si inakuwa imekushinda tu unasema Mheshimiwa Rais hii Wizara imenishinda basi. Kwa hiyo mimi nikafikiri kwamba hii hali ni hali ngumu sana ya Wizara hii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere namomba upokee taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba naomba tukumbuke kwamba migogoro hii haijaanza hivi karibuni na mnakumbuka kabisa kuna Kamati ya Mawaziri nane iliundwa kwa ajili ya kutembelea kila eneo kuangalia changamoto zilizopo za migogoro ya ardhi na sasa kamati hii iko kwenye utekelezaji. Sasa inapofika mahali inaonekana kwamba kipindi hiki ndiyo migogoro imekuwa mikubwa, siyo kweli. Migogoro hii ni chimbuko la kuundwa kwa Kamati ya Mawaziri nane. Nataka hili Waheshimiwa walitambue, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere unapokea taarifa?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niendelee na uchangiaji wangu kwa sababu mimi sijazungumza hakuna Wizara inaitwa Kamati ya Mawaziri.

Wizara inaitwa Wizara ya Ardhi, hakuna Wizara ya makamati ya Mawaziri. Kwa hiyo, mimi niendelee na mchango wangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunapozungumza ukweli kwenye jambo hili tunataka Waziri au Wizara hiyo ijirekebishe basi au kama kuna matatizo imalize. Kuna migogoro ya kudumu ya muda mrefu ni kweli, lakini kuna migogoro ya viwanja kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa yale yote ambayo Wabunge wamejadili humu wamemuomba aende atekeleze ikiwa ni pamoja na kutazama hizi fedha za kujenga majengo badala ya kwenda kupima viwanja. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kwa kweli hili ulitazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naongea haya kusema kweli kwa sababu hatuwezi kuwa na miaka 60 tuna Wizara halafu hakuna eneo, hakuna hata mkoa mmoja ambao tunasema sasa huu mkoa uko nafuu labda twende Dodoma hapa iko nafuu. Hata tunakoishi hapa ni shida. Nenda pale kwenye Wizara ya Ardhi hapo, watu wanazunguka tu wamejaa kila mahali, ni shida. Kwa hiyo, nafikiri kwamba hili nalo tulitazame tuone tunafanyaje ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika Jimbo la Bunda nimeomba nimeandika barua ya kupima vijiji 30, sijawahi kupata majibu, lakini Mheshimiwa Waziri wewe ulikuwa Mara na mimi nakujua ni mkakamavu, mimi sijui Mawizara humu yanakuwaje mimi sielewi, lakini wewe ni mkakamavu kweli kweli yaani sasa sielewi ukifika Wizara fulani sijui ni watu wamekushinda akili sijui nieleweje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ulikuja pale unajua mgogoro wa Mkomariro, siyo mgogoro sasa hivi ni changamoto; za Mkomariro, Sirorisimba, Mgonyamirwa na Kijiji cha Mahanga na Manchimweru kuna migogoro ile ambayo iko kwenye mipaka. Siyo sana kama ilivyo huko

nyuma lakini tupeni fedha, wanahitaji shilingi milioni 60 tu kupima hata hati za kimila wawape ili kila mtu awe na ardhi yake wapunguze migogoro. Nikuombe kwenye hilo nitakuja ofisini kwako niweze kukuomba ili uweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumza hapa ni suala la Nyatwali. Sasa Mheshimiwa Waziri ulikuja Nyatwali nikakusikiliza na tukakufuata, tukakuuliza kwa nini wananchi wa Nyatwali ambao wana *GN* ya vijiji vyao mnawahamisha kinyemela tu bila kuwapa fedha shilingi bilioni mbili au laki mbili au laki ngapi wafanye kazi. Mheshimiwa Waziri ukasema unajua Sheria za *Valuation* zinasema hivi, zinasema hivi.

Sasa nataka nijiulize, hivi wananchi wa Nyatwali wao ni Warundi au ni watu gani? Wana tofauti gani na watu wa Ngorongoro waliohamishwa ambao tena hawakuwa na *registration* yoyote, wakapewa fedha, wakapewa nyumba, wakapewa mashamba, wakapewa vitu vya, wakapewa umeme, wakapewa, yaani wana tofauti gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli hivi Mama Samia analijua hili kweli? Mimi nimuombe mama kwa sababu mama watu wote ni watu wake. Aliwaonea huruma watu wa Ngorongoro wanavyoteseka na leo wanasifia sana kila mahali. Kwa nini hatuwaonei huruma watu wa Nyatwali? Hivi unamhamishaje mtu Mheshimiwa Waziri unasema Sheria ya *Valuation* inasema hivyo? Pale ni shilingi laki saba, sijui heka laki ngapi? Hivi Ngorongoro hakuna hiyo sheria? Hapo Ngorongoro sheria ilipotea? Ni watu ni wale wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo hata mimi ungeniuliza Nyatwali wahame wasihame, ningewaambia wahame kwa sababu si tunataka tuweke Hifadhi ya Serengeti iwe mbuga ya maajabu? Si unataka ishikane na Ziwa Victoria? Sasa wale watu tumekwenda kuwahamisha kwa hiari yao, kwa nini tulete kutumia sheria na wamekubali kuhama, kwa nini?

Nikuombe Mheshimiwa Waziri unajua mimi huwa najiuliza swali moja huwa najiuliza sana, hivi Wabunge mbona Wabunge mkiwa siyo Mawaziri naona kama vile mna-*act* vizuri, mkiwa Mawaziri mnakaa pembeni. Mkitenguliwa mnaanza na maneno, hivi mkoje ninyi? Kwa nini msihurumie watu? Yaani mkitenguliwa ndiyo mnajua huruma ya wananchi, mkiwa kwenye Uwaziri huruma hamuioni. Hivi mkoje ninyi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini msione huruma ya wale watu? Nenda kawatembelee mama wale watu. Wale watu wa shilingi milioni moja, milioni mbili, milioni tatu waone. Wale waliopata mabilioni, mabilioni achana nao. Muone basi wa kuwaona. Kwa nini huwaonei huruma, hivi siku nyingine mama wewe ni wa pale. Hivi siku ile unapita pale watu wanalia machozi, wanajigaragaza, mmekwenda kuwahamisha kwa hiari yao halafu mnawalipa shilingi laki moja, laki mbili, laki tatu? Jamani kwa kweli hii kwamba hiyo haiko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Rais hili kwa kweli alione, mimi sijui kama analifahamu vizuri, mimi sifahamu. Mimi nadhani kwamba sasa tumebaki tutafute *alternative* mtuombee wananchi na wazee sisi wa kule tumuombe tumwone mama na tumwambie mama watuongeze basi badala hata ya shilingi milioni mbili iwe milioni tatu. Hivi shilingi milioni mbili unaenda kununua; kiwanja bure ni shilingi milioni nne, unaenda kununua nini? Huna mahali pakwenda, hujapewa eneo, hujapewa chochote, yaani wahame tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe kwa kweli hiki kitu hakiko sawa. Nikuombe tutamuomba Mheshimiwa Rais hili ataliona aweze kutusaidia kwamba hii hali itakwendaje kwenye jambo hili ambalo siyo zuri kwa kweli, halina wema wowote.

Mheshimiwa Waziri hivi mipaka hii sasa, mipaka ya vijiji mimi niwaombe na nikuombe na Wizara yako, wakati fulani msitumie ramani kwa sababu unaweza kutumia ramani kwa sababu walikuja siku moja kutumia ramani Kijiji cha Tiling'ati wakakuta kijiji hicho kiko Butiama, siyo Bunda. Ukaenda sehemu nyingine kuangalia ramani kijiji kiko Serengeti siyo Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani kwenye migogoro ya muda mrefu nendeni mkajiridhishe, wewe unaishi hapa mwaka gani? Miaka fulani, wewe unaishi hapa miaka gani? Miaka fulani basi mnapima mnaachana nao. Kwa nini hatufanyi hiyo akili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna mtu mmoja anaitwa Albert Einstein alisema akili ni kile ambacho wewe umetolewa vitu vyote ulivyojazwa kichwani ukabaki nacho, hicho ndiyo akili. Kwa nini watu wazito wa busara? Kwa hiyo muende kwenye maeneo ambayo watu wamekaa kwa muda mrefu muwasaidie, muangalie uhalisia wao siyo kufuata ramani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Getere.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa sana ya kuliongoza Taifa letu. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Makatibu Wakuu wote kwa utendaji uliotukuka katika sekta ya ardhi, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo nikianza na urasimishaji; kwa kweli Mkoa wa Dar es Salaam tulipokea vizuri sana, lakini tuliingiliwa na watu ambao hawana maadili, wakavuruga na wakachukua fedha za watu na hati hazijatolewa mpaka leo hii. Wananchi hawajui hatma yao. Tunaomba Serikali itoe maelekezo jinsi watakavyofanya usuluhishi wa jambo hilo tuweze kwenda mbele.

Pili ni kuhusu ujenzi wa makazi ya gharama nafuu; naomba Serikali iangalie jinsi ya kujenga nyumba za gharama nafuu zisiwe na bei kubwa. Gharama kubwa za nyumba zinazosababisha nyumba hizo kuishi wenye fedha badala kuishi wananchi wenye kipato kidogo na kipato cha kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi ya ardhi; wananchi wengi wamekuwa na madeni makubwa ya kodi ya ardhi ni vyema Serikali ikafanya mahesabu ya madeni wakaangalia wastani wa makusanyo yao kama ni machache kuliko madeni Serikali iweke punguzo la kodi kwa kipindi cha mpito wananchi wengi waweze kulipa kodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa

Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali kwa kuanzisha mikopo inayotolewa kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) ardhi. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni mnufaika wa programu hii na imekopeshwa shilingi 1,857,586,634. Mji Mdogo wa Mbalizi kumepimwa viwanja 35,000 kwa gharama ya shilingi 1,273,038,500 na Kijiji cha Mwashoma, Kitongoji cha Inolo vimepimwa viwanja 565 kwa gharama ya shilingi 584,548,134 na umefanyika kwa ufanisi mkubwa sana. Kutokana mahitaji makubwa na faida itayopatikana kwenye mauzo ya viwanja hivi, ipangiwe matumizi yanayolenga kuendeleza ardhi ikiwemo kuweka miundombinu kwenye maeneo yanayopimwa. Kutokana na mafanikio katika utekelezaji huu wa mwanzo, napendekeza Serikali iweke kipaumbele cha kuendeleza programu katika maeneo mengine hususani yanayolizunguka Jiji la Mbeya kutokana na mahitaji makubwa ya makazi yaliyopimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iendeleze programu hii katika vijiji vya Swaya; Lupeta; Nsenga; Ifiga; Nsongwi Mantanji; Nsongwi Juu; Izumbwe; Iwindi; Igoma; Ilembo; Idimi na Haporoto. Upimaji kwenye vijiji ambavyo ni vinakuwa haraka kuwa Miji *(growing towns)* utawezesha

kupunguza na hata kuondoa kabisa makazi holela na pia kuongeza wigo wa walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na programu ya makazi, Serikali iweke usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi. Katika kupangilia matumizi mazuri ya ardhi, ihusishe Wizara za Kilimo, Wizara za Maji na Wizara inayosimamia mazingira. Kwa vile binadamu tunaongezeka ni muhimu kuhakikisha ulinzi kwa kuhifadhi ardhi inayofaa kwa kilimo na pia kutenga ardhi kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hatua zinazochukuliwa na Serikali kurejesha mahusiano mazuri kati ya *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Ulenje na Inyala suluhu haijapatikana. Serikali ichukue hatua pia za kumaliza mgogoro wa miaka mingi wa mpaka kati ya *TFS* na wananchi wa Kijiji cha Mwashoma. Wananchi wa Wilaya ya Mbeya wamekuwa walinzi wazuri wa hifadhi zetu na ni jukumu la Serikali kuhakisha uendelevu huu na kuondoa migogoro ambayo haina maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wizara kwa hotuba, lakini pia kwa ushirikishwaji, tulipata semina kama Bunge, lakini mimi binafsi kama mmoja wa Wabunge ambao Halmashauri zetu zitanufaika na Mradi wa Kuboresha Umiliki wa Ardhi maarufu kama hakimiliki salama, nilishiriki pia katika semina ya kujengewa uwezo kuhusu mradi huu. Napongeza pia uwepo wa banda la Wizara hapa Bungeni, imekuwa ni fursa nzuri kupata huduma binafsi lakini pia kupata huduma kwa niaba ya wananchi na hata ndugu, jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala machache ya kuchangia kama ifuatavyo; kwanza ni kuhusu Mradi wa Miliki

Salama; nilipohudhuria semina ya kwanza kuhusu mradi huu, niliona hoja kutoka kwa Wajumbe wa Kamati kwamba fedha nyingi inaenda kwenye masuala ambayo *it is more of administrat*ive badala ya kupanga, kupima na kumilikisha maeneo mengi zaidi, kwamba ujenzi wa majengo, uimarishaji wa mifumo na kadhalika sio masuala ya muhimu kuliko kupima vijiji vingi zaidi na kutoa hati nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo napongeza kwamba sasa vijiji vimeongezeka kutoka 250 hadi 500 na pia hati na leseni za makazi kutoka laki tano hadi milioni moja kwa kila kipengele. Kwa hiyo, yapo maeneo ambayo mawazo yamezingatiwa. Hata hivyo bado kuna maoni na malalamiko kwamba ilibidi tuongeze zaidi eneo la kupimwa, maoni ni kwamba kwa nini fedha nyingi ziende kwenye majengo na kuimarisha mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, suala hili ni muhimu sana, ujenzi wa ofisi na kuimarisha mifumo utakuwa ni jambo la kudumu, itatumika kwa ajili ya mradi na pia hata baada ya mradi kukamilika majengo kwa maana ya ofisi na mifumo itaendelea kutumika, kwa hiyo ni wajibu wa Serikali kufanya ushirikishwaji kuanzia ngazi za Mitaa/Vijiji, Kata na Halmashauri ili kuleta uelewa wa pamoja na *ownership* ya mradi. Nafahamu kwamba kutafanyika vikao kuanzia ngazi ya *CMT* katika Halmashauri, lakini nashauri kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani katika kila ngazi. Vikao vya ngazi za chini katika Mitaa/Vijiji, ni muhimu ushiriki wa Madiwani uwepo. Utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hivyo pamoja na kuwa jambo hili ni la Serikali, nashauri ushirikishwaji wa viongozi wa CCM kama *observers*, kwa mfano katika vikao vya ngazi ya Halmashauri kwa maana ya Madiwani ni muhimu Mwenyekiti na Katibu wa Chama katika Wilaya/Halmashauri husika wakaalikwa kama watazamaji ili tu kujua *from the horses mouth* maana na faida ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kupunguza upotoshwaji katika *level* zote. Kuhusu gharama za ujenzi wa majengo ya ofisi na kuimarisha mifumo, nadhani ni suala ambalo Wizara inabidi ifafanue kwamba huu ni msingi imara katika kuboresha na kuimarisha sekta ya ardhi kama sehemu ya kufikia hatua sio tu ya kumaliza migogoro, lakini pia kuhakikisha mipango ya matumizi bora ya ardhi inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango kabambe katika Mji wa Mafinga/*industrial park;* kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 37, Mji wa Mafinga uko katika hatua za mwisho kukamilishwa, nashauri na kupendekeza jambo hili ambalo mimi binafsi nimelisukuma sana toka nilipochaguliwa mara ya kwanza mwaka 2015 wakati huo akiwa Mkurugenzi wa Mipango Miji Profesa Lupala, kwa kushirikiana na Ndugu Mahenge na *Dean of Students* wa Chuo Kikuu cha Ardhi tulianza kushirikiana na Wizara katika hatua za mwanzo za kukusanya *data.* Ninaomba Wizara itusaidie tukamilishe suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili ninaomba Wizara kama ambavyo imekuwa ikiniahidi katika mazungumzo ya siyo rasmi na viongozi wa Wizara, tusaidiwe kukamilisha ndoto ya Wana-Mafinga kuwa na *industrial park,* tayari tuna eneo tumetenga ekari 750 kwa ajili ya *industrial park* na mara kadhaa tumezungumza na Kamishna Mathew juu ya jambo hili. Namshukuru Kamishna Mtui tulianza naye lakini pia hata alipokuja Kamishna Minja amelipokea vizuri sana. Ushauri wangu, kama ni kwa utaratibu wa *revolving fund* au kwa namna Wizara itakavyoona inafaa basi tulitekeleze suala hili kwa kuzingatia kuwa kuna *potential* kubwa ya viwanda vya mazao ya misitu, na kama sehemu ya jitihada za kufanikisha suala hili, wenzetu wa *EPZA* walitembelea kuona *potential* hiyo na hasa kwa kuzingatia pia kuwa tupo kando ya *highway* ya *TANZAM* ambayo ni kiungo muhimu sana katika biashara kati ya Tanzania na nchi

za *SADC* na hasa *DRC*, hivyo *industrial park* inaweza pia ikatumika kama *logistics center.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Wizara tulipe suala hili uzito. Huko kwingine mnakosema kuwa fedha za *revolving fund* zimetumika sivyo, *it won't be in Mafinga.*

Kuhusu Baraza la Ardhi Mufindi, wanasema haki iliyocheleshwa ni sawa na haki iliyokoseshwa, wananchi wa Mafinga/Mufindi kilio chao ni huduma ya Baraza la Ardhi, *issue* ilikuwa ni majengo na sasa *issue* naambiwa wajumbe wameshapatikana, tatizo ni Mwenyekiti. Kwa hiyo, wananchi wanalazimika kwenda Iringa Mjini, naomba na nashauri tupate Baraza la Ardhi kwa ajili ya wananchi wa Mafinga/Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na Naibu Waziri Mheshimiwa Geofrey Pinda, Katibu Mkuu - Ndugu Anthony Damian Sanga pamoja na wataalam wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kuhusu umuhimu wa kupima ardhi yote hapa Tanzania, na migogoro ya umiliki ardhi katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa sehemu iliyopimwa na kupatiwa hati hapa Tanzania haijafikia asilimia 30. Hali hii imesababisha Taifa letu kushindwa kuweka mipango thabiti ya maendeleo katika maeneo mbalimbali, na kulinyima Taifa fedha ya kodi ya viwanja vilivyopimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupima ardhi ya Tanzania ni ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi. Jukumu hili hutekelezwa kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi *(NLUPC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo sasa hivi kuna umuhimu wa hii tume kupiga kambi kwenye maeneo yote nchini na kusaidia kupima maeneo yote na kuyapatia hati. Watumishi wa tume hii watoke maofisini waende mashambani kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria za Ardhi upimaji wa mipaka ya vijiji ni lazima uwe shirikishi kwa kuwahusisha Halmashauri za Vijiji kwani wao ndio wasimamizi wa ardhi za vijiji. Ni muhimu sana kuwashirikisha ili kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili zoezi la upimaji liwe na mafanikio, baada ya makubaliano ya mipaka, ni muhimu kuwekwe alama za kudumu *(beacon)* au zikatumika alama za kudumu kama vile maumbile ya asili ya kudumu ikiwemo mito au milima. Ni vyema kwenye kuweka kumbukumbu vizuri, muhtasari wa makubaliano yakawekwa kama kumbukumbu ili zitumike kama rejea ikiwa litajitokeza tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu la Moshi Vijijini kuna migogoro ya umiliki wa ardhi baina ya wakulima na wafugaji katika Kata za Mabogini (Kijiji cha Mserekie) na Arusha Chini (Mikocheni na Chemchem) zilizoko maeneo ya tambarare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii imeshasababisha madhara makubwa ikiwemo vifo na uharibifu mkubwa wa mali kama mazao ya wakulima. Mpaka sasa Serikali ya Wilaya na Mkoa haijaweza kupambana na changamoto hii, kwani tatizo hili linajirudia mara kwa mara. Migogoro ya wakulima na wafugaji jimboni kwangu inasababishwa na uhaba unaoendelea kukua wa rasilimali ardhi. Kutokana na

hali hii, wakulima wamekuwa wanafungua mashamba kwenye maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii kwa kiasi kikubwa husababishwa na yafuatayo; kwanza, Serikali haijayapima maeneo ya wafugaji na wakulima na kuyamilikisha kwa wahusika kwa kutoa hati za kimila na za Serikali.

Pili, kubadilika kwa tabia nchi kunakopelekea malisho kukauka na kusababisha uhaba wa chakula cha mifugo na kuwafanya wafugaji kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima; na tatu, kupanuka kwa shughuli za kilimo na makazi ya watu ambapo maeneo ya ufugaji yamepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii ninaishauri Serikali kama ifuatavyo:-

a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri fedha za ndani za Serikali na zile za mikopo kutoka nje zitumike vizuri kuwezesha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi *(NLUPC)* kukamilisha jukumu lake la kupima ardhi yote ya Tanzania. Idadi kubwa iende kazini na si kwenye makongamano, mafunzo na semina.

b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na migogoro inayoendelea jimboni kwangu, kuna umuhimu wa Serikali kuingilia jambo hili na kuhakikisha kuwa maeneo husika yamepimwa na kumilikishwa rasmi kwa wahusika. Pa kuanzia Serikali iharakishe zoezi hili kwa kutumia mifumo ya hati za kimila zinazotambuliwa kisheria na baadaye wapewe hati za Serikali za kumiliki ardhi.

c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira ya Kitanzania, ninaishauri Serikali ipitie sera za umiliki wa ardhi zenye utata zinazoweza kuchochea migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Sera nzuri na rafiki itasaidia kutoa haki bila malalamiko.

d) Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, Wizara za sekta husika (Ardhi, Kilimo na Mifugo na Uvuvi) zishiriki kikamilifu kwenye zoezi hili, na kila Wizara itenge bajeti ya kusaidia kupima ardhi na kushughulikia changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Mary Francis Masanja - Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii wakati huo Mheshimiwa Kairuki anajindaa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini pia nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuwa muumini mzuri hususan kwenye masuala mazima ya uhifadhi, lakini na utunzaji wa mazingira, lakini ni dhahiri kwamba uhai wetu kwa ujumla unategemea sana vyanzo vya maji, lakini pia viumbehai wakiwemo wanyamapori na mimea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Wabunge imeelekeza zaidi katika Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini pia na Wizara ya Ardhi. Sisi ni wadau wakubwa kabisa kwenye maeneo mengi yenye migogoro hususan maeneo ya hifadhi na tunatambua changamoto hizi zipo na ndiyo maana ilimpelekea Mheshimiwa Rais kuunda Kamati ya Mawaziri nane kwenda uwandani kuchunguza kina na kadhia wanayoipata wananchi hususan kwenye migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niendelee kuwapongeza Wabunge kwa namna ambavyo wameendelea kuwa wavumilivu. Nimejaribu kuongea hapa kwamba chimbuko la migogoro hii ni la muda mrefu. Tunakumbuka tangu Serikali

ya Awamu ya Tano iliyokuwa inaongozwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, kulikuwa kuna migogoro hii na aliweza kuunda Kamati ya Mawaziri nane wakaenda uwandani wakaanza kuchunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeenda uwandani kwa ajili ya kutekeleza na ninyi mtatambua mwaka jana tumezunguka Mawaziri, tumepita kila sehemu kuangalia hizi changamoto. Niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge changamoto hizi ni za muda mrefu na utatuzi wake unahitaji sana busara, lakini na hekima lakini na tuvumiliane kwa sababu unapoenda unakuta mwenzio kaingia huku inahitaji busara sana kutatua changamoto hiyo na ndiyo maana Mheshimiwa Rais alielekeza kabisa kwamba hahitaji kuona taharuki inatokea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumeenda hatua kwa hatua na pale ambapo kuna kuwa kuna mabishano, Serikali inaangalia, kama kuna umuhimu sana wa kung'ang'ania hili eneo basi kuna maslahi mapana ya Taifa letu, lakini pale ambapo tunaona tunaweza kuachia, basi tunakaa tunazungumza na Mheshimiwa Rais ameweza kuachia takribani vijiji 975 vilivyokuwa vimesajiliwa ndani ya hifadhi vyote ameviachia. Tumpongeze sana na tuendelee kumtia moyo kwa sababu migogoro hii ni mingi, lakini tunaenda kuimaliza kabisa na Mheshimiwa Waziri wangu ameahidi kabisa kabla ya bajeti ya Maliasili tutakaa na Waheshimiwa Wabunge wote wenye migogoro tutajadiliana eneo kwa eneo ili tufikie mahali migogoro hii tuimalize maana lengo la Serikali ni tutembee pamoja na siyo tena kuendelea na migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuzungumzia suala la Mbarali ambalo lilijitokeza jana na suala kubwa hapa ni kwamba mchakato mzima wa kuainisha hii mipaka tayari umeshakamilika isipokuwa tunachotarajia sasa hivi ni kuleta

kwenye Bunge lako hili tukufu ili liweze kuridhia marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kabla ya kuisha Bunge hili tayari azimio hili litaletwa katika Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuwaondoe shaka Wanambarali, tuwaondoe shaka Wanambeya ambao wamekuwa wakishughulika na hizi shughuli za kilimo hususan katika maeneo ambayo yanazunguka Bonde la Usangu kwamba tutakamilisha na kila mtu ataelewa mipaka yake na wale ambao wameainishwa kwamba wataainishiwa mipaka yao basi wataweza kuiona kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumejitokeza kwenye suala hili la Nyatwali. Suala la Nyatwali malengo ya Serikali ilikuwa ni kupunguza migogoro ya wanyama wakali na waharibifu. Kama ambavyo umekuwa ukisikia, tumekuwa na changamoto kubwa sana ya wanyama wakali na waharibifu kwa hiyo, tunajaribu kuongoa zile shoroba ambazo tunaweza angalau tukaruhusu wanyama pia nao wakaweza kupita katika maeneo ambayo kusiwe na mgogoro kati ya jamii pamoja na wanyama wakali na tukitambua kwamba Serengeti ni hifadhi maarufu na imekuwa ya kwanza inaongoza kimataifa kwa maana ya uhifadhi bora na ni chanzo kikubwa cha mapato katika sekta ya utalii. Hivyo tunaendelea kuwaomba Wananyatwali kwamba Serikali imeendelea kusikia maombi yao, lakini tunashukuru kwa sababu wamekubali kwa hiari kwa maana tulienda kuzungumza nao na tukawaeleza kwa nini tunaenda kufanya hivyo. Lengo kubwa ni kuokoa maisha ya wananchi. Hakuna mtu anayefurahi kusikia kila siku kilio cha wananchi wanakufa kwa sababu ya wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umeisha naunga mkono hoja, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Masanja. Nilimwita Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki - Waziri wa TAMISEMI aweze kuchangia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi. Nianze na mimi kwanza kwa kuanza kuunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara yetu ya Ardhi na nimpe pongezi nyingi sana Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu Waziri wa Ardhi na uongozi mzima wa Wizara hii kwa kuja na bajeti hii. Naamini itakuwa ni bajeti ya kihistoria, bajeti ambayo itaweza kutusaidia na kuweza kutoka, lakini zaidi kutatua migogoro mbalimbali na kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na ardhi ambayo imepangwa, imepimwa lakini vile vile imeweza kumilikishwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze mpango walionao katika suala zima la usimamizi wa ardhi nikiamini katika fedha zile za mikopo, zitaweza kusaidia pia wanawake wengi zaidi kuweza kuwa na milki ya ardhi ambayo pia itaweza kuwasaidia wanawake wetu na vijana katika suala zima la uwezeshaji pia wananchi kiuchumi, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nitajikita zaidi katika suala zima la utatuzi wa migogoro. Tumeweza kuwasikia Waheshimiwa Wabunge na mna hoja ambazo ni za msingi tumezipokea. Hakuna hoja hata moja ambayo hatutaitilia maanani, tutaendelea kulifanyia kazi suala hili na kuhakikisha kwamba tunaendelea kushirikiana na wananchi lakini pia nanyi kama viongozi wao na wawakilishi katika suala zima la utatuzi wa migogoro hii yetu ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili tutaendelea pia kusimamia suala zima la utatuzi wa migogoro ya mipaka katika vijiji na vijiji, kata na kata, wilaya na wilaya lakini pia na mikoa, mmoja na mwingine kuhakikisha kwamba kila mmoja anajua mipaka yake sahihi na wananchi wetu wanajua pia

wanaangukia katika eneo gani la mipaka, lakini kubwa zaidi kuweza kutatua migogoro ambayo kimsingi siyo ya lazima na ninaamini hili linawezekana kama ambavyo tumekuwa tukiendelea kufanya hivyo kwa kushirikiana na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea pia kuweka mkazo katika suala zima la mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kushirikiana na Tume yetu ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi tumeendelea kufanya hivyo. Ukiangalia mfano katika Wilaya ya Ifakara tumeweza pia kupima muda siyo mrefu. Mwaka jana tu vijiji zaidi ya 30 lakini vilevile kwa upande wa Serengeti zaidi ya vijiji 33 na tunaendelea pia kutenga fedha na hata Ikungi muda siyo mrefu pia tumeendelea kushirikiana na halmashauri na wadau mbalimbali ikiwemo *UN Women* katika kuhakikisha kwamba tunaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, lakini kubwa tunaendelea kutenga fedha na tumezielekeza halmashauri zetu ziweze kutenga fedha katika suala zima la Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ili kuwa na matumizi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kujikita pia katika eneo la Kamati za Mipango Miji; tunaendelea kusimamia Kamati zetu za Mipango Miji kuhakikisha kwamba kwanza zinafanya kazi kwa uadilifu, lakini vilevile kwa weledi unaokusudiwa kuhakikisha kwamba tunaenenda kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ambayo ipo na kwa kamati zile ambazo zitaonekana pia hazitimizi wajibu wao ipasavyo hatutaendelea kusita kuzivunja na kuweza kuunda zingine. Lengo tu ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na kamati ambazo kweli zina weledi, zina uadilifu lakini pia zinafanya kazi kwa ufanisi kuhakikisha kwamba hatuleti migongano na migogoro ambayo haina msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia tu kulihakikishia Bunge lako tukufu, tunaweka mkazo katika suala zima la kupanga, kupima na kumilikisha kama mamlaka za upangaji kupitia halmashauri zetu na tushukuru sana Serikali yetu.

Tumeweza kupata zaidi ya shilingi bilioni 42.3 ambazo tumeshazikopesha kwa halmashauri takribani 54 na mwelekeo ni kuhakikisha kwamba fedha hizi tunaweza kuzikopesha, lakini pia zimetengewa mfuko maalum, hazichanganyiki na fedha zingine za halmashauri ili ziweze kuwa na mzunguko na kuweza kupanga miji yetu vizuri zaidi, kuweza kumilikisha, lakini pia wananchi wetu waweze kupata hati au kupata milki ambazo zitakuwa salama na ambazo zimeweza kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kushirikiana na Wizara yetu ya Ardhi tutaendelea kusimamia suala zima la usimamizi wa sekta yetu hii sekta ambayo ni muhimu sana katika uchumi, lakini vilevile katika suala zima la maendeleo ya jamii, lakini pia maendeleo ya kiusalama na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema naunga mkono hoja na ninashukuru kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Angellah Kairuki.

Sasa namwita Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda - Naibu Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati huo mtoa hoja anajiandaa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii na mimi kuwa sehemu ya wachangiaji wa hoja iliyopo mezani, lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na leo hii tuko mbele ya Bunge lako tukufu kwa ajili ya kupangilia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa mara ya kwanza kusimama na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa

kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa jinsi alivyoniamini nahaidi kwenda kufanya kazi ya kuishauri Wizara kwa maana ya Waziri, lakini na kutoa matokeo ambayo ni matarajio ya waliyo wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana sana familia yangu kwa utulivu, kwa sababu muda mwingi siko nayo, waendelee kuwa wavumilivu wakati huu tunapotekeleza majukumu ya kuiendeleza nchi. Niwashukuru wapiga kura wangu kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuwa mwakilishi wao na baadaye kutokana na hayo ndiyo nikaaminiwa kuwa kwenye nafasi hizi ambazo ni za kiutendaji Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwashukuru Wabunge wote mliopata nafasi ya kutoa michango yenu. Watu karibu 30 na zaidi mmechangia kwa uzito wa hali ya juu masuala yote yaliyowasilishwa ambayo yanaisoma bajeti yetu kwa mwaka huu ambao ni mwaka tarajiwa unaokuja na kimsingi mawazo yote ni ya muhimu sana sisi kuyazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Kamati kwa kuonesha ule uelekeo wa nini ambacho kama Wizara tunatakiwa tulibebe na mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, maoni na mapendekezo na maelekezo ambayo mmetupatia kama Wizara itakuwa ni ajabu sana tukatoka nje ya maoni yenu tukaenda kufanya vitu vingine ambavyo vitakuwa haviendi sambamba na maelekozo ya nchi ambayo ndiyo mwelekeo wa nchi yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ukienda kwenye hili eneo la migogoro, migogoro hii ina sura mpaka tatu; tunayo migogoro ya ndani ambayo hii ni mimi nimeibiwa kiwanja, mimi nimefanya nini, nimecheleweshewa hati nimefanya nini? Hii ni migogoro ambayo iko kwenye eneo la utendaji wa Wizara katika kusimamia watendaji wetu

kufanya kazi zao kwa uadilifu na uaminifu na ninashukukuru sana Waheshimiwa Wabunge wengi mmeungana na sisi katika mabadiliko mbalimbali ambayo tumeendelea kuyafanya ndani ya Wizara katika kuimarisha utendaji. Mojawapo ni lile lile la kutambua hata watumishi wetu ambao walikuwa wanafanya kazi moja kwa moja kwenye halmashauri, lakini badaye Serikali iliamua kuwarudisha na kuwa chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwatoe wasiwasi kwamba kurudi kwao Wizarani bado hakutafisha au kudhoofisha utendaji katika maeneo yote ya Serikali yetu kwa maana ya halmashauri na hii itasaidia sana kuimarisha usimamizi kwa sababu kama mtabaini katika muundo wa utumishi ukitoka ngazi ya Waziri mpaka Kamishna wa Mkoa palikuwa pana *gap* kubwa sana kwenda kukuta watendaji wetu ambao wako kwenye halmashauri, lakini sasa tunakwenda kuhakikisha kwamba hawa wanarudi kwenye nguvu ya Wizara ili usimamizi wao uwe karibu zaidi ili waweze kuwajibika ipasavyo, hii itatusaidia sana kutoka matokeo, kwa sababu taasisi nyingine zote zilifanya hivyo hata TAMISEMI yenyewe ilitambua kwa mfano Mamlaka kama za *TARURA* kwa ajili ya kuongeza usimamizi mzuri. Hata sisi Wizara ya Ardhi tunaendelea kutengeneza mpango ambao utaletwa mbele ya Bunge lako tukufu kwa maana ya kutengeneza Kamisheni ya Ardhi ambayo itakuwa maalum kwa ajili ya kusimamia shughuli za ardhi hapa nchini na inaweza ikaleta ufanisi mkubwa sana ambao ndiyo matarajio ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye migogoro; kuna migogoro ambayo ni ya kati kati hapa na migogoro mingi ni kwa muda mfupi niliyokaa Wizara hii migogoro hii ya kati ambayo inasababishwa na mgongano wa kimipaka ndani ya nchi, ndani ya wilaya na wilaya, ndani ya kijiji na kijiji na hii inayohusisha kwa maeneo ya hifadhi tunajaribu kupitia vilevile hata sheria zetu kuziangalia. Kwa sababu utaona

kuna kachangamoto kadogo unaweza ukakaona ni kama ni kadogo lakini kanagonganisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano zile *GN* zinazosomwa katika kila maeneo ni mamlaka tatu zimepewa mamlaka ya kutoa *GN* ambazo ukiliangalia unaweza ukakuta linaleta mgongano ule ambao unasababisha migogoro kwa wananchi wengine, kwa mfano TAMISEMI kwenye kupima vijiji imepewa mamlaka ya kutoa *GN*, Maliasili imepewa mamlaka ya kutoa *GN*, Ardhi ambao ndiyo wasimamizi halisi wa ardhi nao wanatoa *GN*. Sasa mgongano huu lazima tukae, tutakaa katika Wizara hizi ili tuweze kutafsiri nani hasa awe wa mwisho kwenye kuzungumza juu ya matumizi ya ardhi kitu ambacho kitasaidia sana kuondoa hii matatizo makubwa ambayo yanatukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano niwape mfano mdogo tu hapa Wilaya ya..., *I mean* mgongano uliyopo kati ya Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara eneo moja linaitwa Mkungunero. Mkungunero TAMISEMI ilienda ikatambua vijiji, baadaye Maliasili ikatambua maeneo ya hifadhi, sisi tukaenda tukaweka mpaka wa mkoa; ule Mkoa kimsingi umesoma vijiji vingine ulikata ule vijiji ile alama ya mkoa imeacha vijiji vingine Dodoma, vingine Manyara.

Sasa migongano kama hii tusipo ikalia pamoja tukaiweka vizuri migogoro hii haitaisha, lakini ndani ya migongano hiyo ya kimpaka mingine ipo kwenye wajibu tu wa viongozi wa maeneo, tunaikuza sana sana mpaka ikapelekewa na Mawaziri nane na nini, lakini kwa mtazamo halisi unaona kabisa *DC* wa eneo anahusika, Mbunge wa eneo anahusika, Mwenyekiti wa Kijiji anahusika, yangeishia kwenye *level* hiyo wala kusingekuwa na mgongano, lakini kule nimeona kabisa na kubaini kuna baadhi maeneo mengine watu wanakimbiana, hawakai pamoja kuzungumzia matatizo ya wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo gani kati ya mwananchi ambaye amepitiwa na mpaka wa Mkoa analima Mkoa wa Manyara anakaa Mkoa wa Dodoma, kuna tatizo gani huyu mwananchi kuachwa katika muundo huo wa kutumia ile ardhi na badala yake tunaandamana.

Mimi niwaombe kwenye eneo hili mamlaka za maeneo zisimame imara kuzungumza mambo haya hadharani, yakija huku Wizara, huku tunafuata sheria, hata tukienda na sheria zetu pale hazitatanzua mgogoro kama ambavyo tungekaa huko katika ustaarabu wetu wa maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi niwaombe ndugu Waheshimiwa Wajumbe na Wabunge wenzangu, tuzungumze, kwenye maeneo haya tuzungumze kwa uwazi kabisa. Tunafanya juhudi mbalimbali na kimsingi lazima muone namna ambavyo Serikali inafanya juhudi za kujaribu kutatua migogoro, lakini migogoro mingi haiwezi kutatuliwa kama viongozi wa maeneo husika wao wenyewe hawawi sehemu ya kumaliza migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lipo hili tatizo la mipaka ya nchi, hilo tunaendelea nalo na Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na kutambua mipaka, kuna maeneo mengine bado kuna mvutano kidogo ila yanaenda kumalizika hivi karibuni na nchi nyingine tumeendelea kuzungumza nao kwa ajili ya kunyoosha mapito, kwa sababu Tanzania na majirani zake hatuna mgogoro wowote wa kimahusiano, kwa hiyo, masuala haya yanakwenda vizuri na ni wahakikishie kabisa kwa mfano hili eneo la Mheshimiwa Kitandula kule juu baharini wala asiwe na wasiwasi kwa sababu mazungumzo ya Kenya na Tanzania ni ya karibu mno kuliko hata mataifa mengine kwenye suala la mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la mabaraza; hili suala la mabaraza Waheshimiwa Wabunge mmetoa mawazo kuhusu uimarishwaji wa mabaraza, ni kweli hata sisi

tumeliona na tumeunda timu maalum ipitie. Hata hivyo Serikali Kuu jambo hili lilikwenda kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuangaliwa, je, lirudi mahakamani au liendelee kuwa Wizara ya Ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa upande wote kwa sababu ni watu ambao tunasubiri maelekezo sisi tumeendelea kujiandaa upande wetu kuimarisha haya mabaraza na mwaka huu wa fedha ambao leo tumewaletea bajeti hapa tunakwenda kwa ajili ile tofauti ya mabaraza 47.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu, ahsante, wale wanao kosekana kwenye halmashauri karibu 47 tunakwenda kuwaajiri mwaka huu wa fedha kwenye zile wilaya ambazo bado hazijapata Wenyeviti, tunaenda kuajiri. Vilevile tuwaombe mshikamano wenu kwamba tunakwenda kuleta wale watendaji lakini tunahitaji maeneo ya kufanyia kazi ambayo kimsingi tunapata msaada kutoka TAMISEMI kwa maana ya maeneo yale ya ofisi za mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sera tumeshaanza kuipitia kwa uzito wa kutosha, hata hili suala la *diaspora* linakwenda kuisha kwa sababu hatuoni kama tunaweza tukaendelea kuwa na msimamo wa kutokutambua Watanzania wenzetu ambao wakija kujenga nyumba Tanzania hawahami nayo. Wakija kuwekeza Tanzania maana yake wanarudisha nguvu walizozikusanya nje nchini mwao, Serikali imeliona na sasa liko katika hatua za mwisho na hawa Watanzania wenzetu wataenda kunufaika na hii huduma ambayo ni ya kupata ardhi na kuwekeza nchini Tanzania na hii ndiyo mataifa mengi yanafanya kuwatumia watu wao ambao wako nje kwa maendeleo yao hata ukienda Ethiopia

pale utakuta wazamiaji wengi ndiyo wanajenga majengo kule ya maana kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** shsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita mtoa hoja Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula aweze kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uhai mpaka tumefika hatua hii tunapokwenda kuhitimisha hoja ya bajeti ya Wizara ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee kabisa niwapongeze na kuwashukuru Wabunge wote ambao kwa namna walivyochangia Wizara hii ya Ardhi. Wengi wamechangia kwa uchungu sana na wamechangia wakiwa na imani ya kwamba kile wanachokizungumza kikifanyiwa kazi maana yake Watanzania wengi wataweza kuwa na amani. Nina washukuru sana kwa sababu ni dhamira njema ya Serikali kuhakikisha kwamba watu wao wanaishi kwa amani na hili sisi kama Wizara tumelichukua, tunaona ni jambo la msingi na michango yote iliyotolewa yote ilikuwa ni michango ya busara ambayo inahitaji kuifanyia kazi kwa namna moja ama nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nishukuru pongezi mlizozitoa kwa Wizara na Serikali hasa kwa Mheshimiwa Rais. Kwa kweli kama ni pongezi zote mlizozitoa kwa Mheshimiwa

Rais ni hakika zinamstahili, kwa sababu katika mageuzi makubwa yanayofanyika ndani ya Wizara kuna mkono asilimia 100 kutoka Mheshimiwa Rais. Wote mnajua Wizara ilikotoka na Wizara ilipo sasa kwa kwa uhakika Wizara ilipo sasa haianzishi migogoro mipya, bali inahangaika na migogoro ambayoo imekuwepo ya miaka nenda-rudi, lakini kwa miundombinu ambayo tunakwenda kuwekeza tuna imani tutakwenda kuimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji jumla ya Wabunge 34 wamechangia 30 wakiwa wamechangia kwa kuwaongea na wanne wamechangia kwa maandishi, niombe kutolea ufafanuzi kwa hoja za Wabunge ambazo wamezitoa katika mjadala huu ambao ulikuwa unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na lile ambalo lilikuwa linaongelewa ya kwamba Serikali ilikosea sana kuwahamisha watumishi wa TAMISEMI na kuwapeleka Wizara ya Ardhi.

Naomba niseme tu kwamba sababu za msingi zilizopelekea Serikali kufanya jambo hilo ni kwamba sheria zote zinazohusu masuala ya ardhi zimekasimiwa mamlaka na usimamizi wa ardhi kutoka kwa Waziri mwenye dhamana. Sasa hawezi kuwa Waziri mwenye dhamana wakati wale ambao unawasimamia hawako kwako wewe siyo mamlaka ya nidhamu, wakifanya kosa la kiutalamu, wakifanya kosa la kiutumishi, huna mamlaka ya kuweza kuwagusa, lakini wanachokifanya ni kile ambacho wewe umepewa dhamana ya kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kitendo cha kuwahamisha kuwaleta katika Wizara, Serikali ilikuwa na lengo zuri la kutaka kuwaweka katika mstari ambao utaweza kusimamiwa kitaaluma, kwanza kutoka kwa Waziri mwenye dhamana mwenyewe, lakini pia katika usimamizi wao kuna bodi ambazo zinawasimamia na zote ziko chini ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia Sheria ya Ardhi Sura 113 kifungu cha 8 cha sheria hiyo na kifungu cha 5 cha Mipango Miji kwenye Sheria Namba Nane ya mwaka 2007 aya ya 18.11 na bahati nzuri mtoa hoja alikuwa ni mwanasheria anajua hii. Kwa hiyo, Serikali imeweka hiyo kuhakikisha ya kwamba haya yanakwenda katika utaratibu huo. Lakini pia majukumu ya Wizara wameainishwa kwenye Tamko la Mheshimiwa Rais Namba 385 la tarehe 7 Mei, 2021 na Waraka huu wa Utumishi Namba 01 wa mwaka 1998 ulifanyiwa marekebisho mwaka 2019 na katika kufanya hivyo sekta tatu zilitolewa kwa wakati mmoja; maji, barabara pamoja na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara ya Maji, niwapongeze pia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambao tayari waliunda vitengo. Sasa ukiangalia namna bora ya utoaji huduma kwa maji ndiyo hiyo hiyo inatakiwa ikawe bora katika sekta ya ardhi ambayo ni Wizara wezeshi katika suala zima la kuweza kutoa huduma kwa wananchi.

Kwa hiyo, katika hiki ambacho tunakifanya sisi sasa ni kwamba watumishi wameletwa Wizarani waweze kusimamiwa na hatua mbalimbali zimechukuliwa katika wale ambao wamesababisha migogoro ikiwepo hapa Mkoa wa Dodoma watumishi wengi wameachishwa kazi na wengine wamepewa maonyo kwa sababu tu ya kukiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama huyo mtu hauko nae ndani ya Wizara yako anayefanya sekta yako huwezi kumsimamia, lakini hatua hiyo pia ilikuwa imelenga suala zima la kuboresha na tunavyokwenda hata mabadiliko ambayo Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ameyasema, yanafanyika kwa nia njema na dhamira njema ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge analalamikia labda mtu huyu hafanyi kazi vizuri, unachunguza unakuta labda kazi haiendi vizuri, lakini wakati mwingine anafanya vizuri katika kuboresha

zaidi unamtoa pale alipo, unapeleka kwenye changamoto nyingi ili aweze kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano yule wa Tabora ametoka Tabora ameletwa Dodoma na anafanya kazi nzuri sana. Aliyekuwepo Dodoma hapa naye amepanda cheo kafika hatua ya kwenye nafasi nyingine nzuri zaidi. Kwa hiyo, ni kwamba tunapeleka huduma hii kulingana na uhitaji uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nitamuomba tu aliyetoa hoja hiyo atuletee watumishi au Halmashauri zilizogoma kufanya kazi kwa sababu tu zimehamishiwa Wizara ya Ardhi. Sisi kama Wizara hatuna taarifa wala nyaraka zozote za watumishi kuamua kuacha kazi au kugomea kazi, kwa sababu tu wametoka katika Wizara ya TAMISEMI na kupelekwa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaomba sana hilo tulipate kwa maandishi ili tuweze kufuatilia hao na tujue kwa nini wametoka maana hatuna taarifa hiyo tumeisikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine ambalo amelizungumza Mheshimiwa Mtemvu; mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Mtemvu amekuwa akiliongelea sana suala hili la maeneo ambayo yamechakaa na kutaka pengine kufanya miji yetu ipendeze. Niseme kwa Watanzania hii ni fursa ambayo hata yule Mtanzania wa kawaida mwenye ardhi yake mjini ambaye ana nyumba yake ya toka mwaka 1947 lakini unapoangalia mipango ya majiji yetu na miji yetu pale alipo sasa hapatakiwi kuwa na jengo kama lile. Niwaombe sana wasiuze maeneo na kuondoka, lakini watumie ardhi zao kuwezesha kujinufaisha na kuleta utajiri, waingie kwenye ubia kama una jenga ghorofa tano pale mwenye hati ni mimi nina jengo langu la kawaida wewe jenga ghorofa zako tano tukubaliane zangu ni ngapi? Maisha yanaendelea mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kumejitokeza wahuni wachache wanaenda katika maeneo hayo hasa kwa akinamama waliozeeka zaidi wanawadanganya, wanawanyang'anya zile ardhi na mtu anajenga jumba pale anaendelea na kufaidika, lakini yule aliyoitunza ile ardhi kwa muda mrefu anakosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Jiji la Dar es salaam kumekuwa na mipango mingi zaidi ya kumi ambayo imefanyika tulikuwa na *Buguruni Development Plan* ya 2014-2024 inakwenda kuisha na hali inayokwenda katika uendelezaji bado ni wa kusuasua. Kuna *Kurasini Development*, kuna *Dar es salaam Central Area Development Scheme* ya 2018 – 2028; kuna Magomeni ambayo imeshaanza sasa hivi ile *Magomeni Quarter* tunaona inavyokwenda na ndiyo muelekeo. Kwa hiyo, *plan* ziko nyingi kinachotakiwa ni zile Mamlaka za Usimamizi za Upangaji kuweza kutekeleza hiyo mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wakati mwingine tunachanganya, sisi kama Wizara tunasimamia sera, kanuni na miongozo mbalimbali suala la uendelezaji miji lina mamlaka yake ya kusimamia, lakini kwa sababu Serikali ni moja na tunafanya kazi moja, ukiona mambo hayaendi vizuri unatia mkono katika kuhakikisha kwamba suala hili linakwenda vizuri.

Kwa hiyo, katika mambo ya ushauri mliyoyatoa tunayachukua na nimshukuru sana Mheshimiwa Angellah Kairuki anayesimamia mamlaka za upangaji, amejibu suala la migogoro na mambo mengine ambayo pengine mamlaka za upangaji zinatakiwa kuisimamia kwa karibu hasa walioko kule chini Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mtemvu ameenda mbali zaidi akasema tuangalie namna bora ya

kuendeleza maeneo ambayo pengine yamechakaa kwa kutumia *National Housing*. Mpaka sasa *National Housing* kazi inayofanyika ni nzuri na katika ufanyaji kazi wake tayari wameishaingia katika mikataba mbalimbali wakati wa hotuba yangu nilizungumza na hiyo haiishii katika wafanyabiashara tu, inakwenda pia katika kubadilisha kabisa maeneo mengine ambayo yapo na tayari katika mipango yao wamefungua milango ili watu waweze kuingia, na Mheshimiwa Rais kafungua milango kuruhusu wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi wachukue fursa hiyo sasa kwa sababu suala la uendelezaji milki bado liko chini sana tunahitaji kuongeza kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, milango imefunguliwa kwa hiyo anatakiwa kuingia kusaidiana na Shirika la Nyumba, lakini bado anaweza akaingia na mtu binafsi kama nilivyosema, lakini bado hata kama wewe Mheshimiwa Mbunge una ardhi yako bado ni ruksa kuingia katika makubaliano na likaendelezwa tukabdilisha sura ya miji yetu. *Magomeni Quarter* ni mfano mzuri na tumekwenda kujifunza hata kwa wenzetu Morocco walikuwa wanakweneda *block* kwa *block* wanaondoa zile *squatters* wanajenga majengo, lakini wale walioko pale hawaondolewi, wanatolewa kwa muda wanakaa sehemu baadaye majengo yakikamilika wanaingia na maisha yanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Mdee amezungumzia habari ya *National Housing* katika mradi ule wa *Kawe Seven Eleven* pamoja na ile miradi mingine ambayo ameitaja. Naomba tu niseme ya kwamba ni kweli *NHC* kuna kipindi walisimamishwa kuchukua mikopo wasiendeleze maeneo yao na wakati wanasimamishwa kulikuwa na miradi mikubwa inaendelea pamoja na *Mororcco Square* ambayo sasa imekamilika. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Shirika lenyewe la Nyumba katika suala zima la kuondokana na hili suala Mheshimiwa Rais ameridhia *National Housing* waendelee kukopa na wameshakopeshwa,

wamekubaliwa kukopa shilingi bilioni 173 ambazo sasa zinakwenda kukamilisha ile na hao ambao miradi yao ilikuwa imesimama ambao pengine wangeweza kuidai *National Housing,* tayari tuko nao katika mazungumzo kuweza kuona ni kwa namna gani pengine ubia uliokuwa unaendelea katika kufanya kazi au ule ukandarasi uliokuwa unaendelea utaendelea bila kuingiaza hasara *National Housing* kwa sababu kosa lile halikuwa la *National Housing* na ndio maana Serikali imeingia kwa karibu sana kuweza kulizungumza suala hili liweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la migogoro ambayo imezungumzwa na Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Bahati, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Yahaya, Mheshimiwa Ally Makoa na Mheshimiwa Robert nadhani Wabunge kama kumi hivi wamezungumzia suala la migogoro hasa ya vijiji 975. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mary Masanja ameweza kujibu kwa namna nyingne ambayo imekwenda kulizungumzia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu, migogoro hii kama tulivyosema ni ya muda mrefu, lakini imekuwa sugu kwa sababu kule chini ambako ndio mgogoro unaanzia, wanaacha mgogoro unaanza mpaka unafukuta unafikia mahali ambako hauwezi tena kusuluhishwa. Lakini kama tungekuwa tunafanya kazi kule, bahati nzuri sisi wote ni Madiwani na migogoro yote hii iko kwenye maeneo yetu, tunasikia mpaka hapa na hapa kuna kelele, lakini tumekaa kimya tunasubiri kuyaleta kwenye Bunge. Tukiyasimamia kule kule chini hasa wale watendaji wetu, kwa sababu ndio jukumu lao, kama *GN* imezungumza habari ya maeneo ya utawala na kazi ya Wizara ya Ardhi ni kutafsiri *GN,* kazi yake ni kutafsiri *GN* ambayo mipaka inakuwa imewekwa inaweza ikawekwa kwa *features* zilizoko ardhini au kwa kufata *coordinates* na katika maeneo ambayo tunafata *coordinates* peke yake wananchi wengi wanakataa, lakini

ukienda kwenye milima ukienda kwenye mito, mito inahama leo ulikuwa umeweka *coordinates* kesho inakataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo matokeo yake ni kwamba tunakwenda na vyote viwili kunakuwa na *coordinates* lakini na zile *features* zilizoko ardhini. Lakini sasa wananchi wetu mara nyingi wengi hawataki kukubali ule ukweli hata wale walioingia katika maeneo hawataki kukubali ukweli na sheria haiwezi kusema uongo katika masuala ya tafsiri. Bahati nzuri ukienda kwenye migogoro wanakwambia tafsiri iliyoko kwenye *GN* au *GN* iliyoko wanaitambua. Ukisema unaenda kufanya tafsiri kwenye ardhi anakataa, sasa tunataka kujiuliza katika hilo kipi ambacho unakiona kinafaa? Ukienda kwenye ramani iko sawa, lakini mwananchi anasema hapana sisi hapa kulikuwa na mto, lakini mto haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tufate taratibu zile zote za kitaalamu na haya yameweza kupelekea Mheshimiwa Rais aridhie kwa sababu ya wananchi ambao walikuwa wamekaa maeneo mengi, ameweza kuridhia ekari 2,385,316 kuwapa wananchi pamoja na kwamba waliingia katika maeneo ambayo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika hili kwa sababu amepunguza migogoro na kero za wananchi. Niwaombe tu Watanzania wenzangu pale ambapo Mheshimiwa Rais amesharidhia, mipaka tumeshaibadilisha, tumeshaweka mipya na tumeshaweka zile alama kwa maana ya *beacon* tuheshimu, kwa sababu changamoto nyingine zinakuja mpaka umewekwa na unaonekana, lakini mtu anavuka anaingia kule ndani. Ukienda kule unaingia kijinai, maana yake wewe ni mhalifu kama wahalifu wengine. Lakini tukisema siku zote tusitekeleze kile ambacho kiko kisheria inaweza ikatuletea shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ya migogoro ambayo ipo mimi nitoe rai tu kwa Watanzania wenzangu wote tutii sheria bila shuruti kwa sababu ardhi ndio wezeshi katika shughuli zote za kimaendeleo, ukiwa na mgogoro huwezi kwenda popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Nyatwali na fidia; bahati nzuri alililianzisha Mheshimiwa Halima akalizungumza, akaja Mheshimiwa Ester mtoto wa pale pale akalizungumza, akaja na Mheshimiwa Getere naye akalizungumza. Wamelizungumza kwa uchungu sana na sisi tunakubaliana na hisia wanayokuwa nayo, lakini Serikali inachokifanya haina maana yoyote, yaani haina lengo la kudhulumu mwananchi yoyote. Katika masuala mazima ambayo yamefanyika hakuna mwananchi aliyedhulumiwa. Kabla ya kufanya uthamini kuna utafiti unafanyika, bahati nzuri wanasheria wanajua wanazisoma sana hizi sheria, kile ambacho wananchi walikuwa wanauziana na kile ambacho Serikali inatoa ni vitu viwili tofauti. Serikali imetoa kikubwa kuliko kile walichokuwa wanauziana, kwa hiyo, kinachofanyika pale wananchi tunayo na mikataba yao walikuwa wanauziana wengine ekari moja shilingi 500,000 wameenda sana mpaka shilingi 1,500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikaongeza pale *top-up* pale ya shilingi 500,000 lakini thamani ya ardhi ya pale haifiki ile thamani ambayo wamepewa. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba Serikali haina dhamira ya kumnyanyasa Mtanzania lakini Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba inalinda pia maisha ya Mtanzania katika kuwezesha kuweza kumlipa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati amezungumza kwa kirefu sana amesema nisipotaja maeneo ambayo yametolewa kwa sababu amekuwa akisikia Waziri Mkuu kasema hivi, *statement* ya Waziri Mkuu na tunayosema Wizara ni ile ile wala haina tofauti yoyote. Katika eneo la

Hifadhi ya Ruaha kule Mbarali jumla ya vijiji 13 vimeondolewa katika maeneo ya hifadhi ambavyo ulitaka tuvitaje ni Azimio, Igava, Ruiwa - Mahango, Mapogoro, Mbalino, Miyombweni, Mlungu, mpolo, Mwatenga, Nyakazobe, Magululu, Sonyanga na majina magumu kweli kweli, lakini ndiyo hivyo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo vyote vimebaki *I mean* vinatakiwa kutoka kwa 100% kwa maana ya vijiji ni Kijiji cha Msanga, Iyala, Makulusi, Kilambo na Luhanga. Lakini katika hivi vijiji vitongoji katika haya maeneo vitongoji 38 katika vijiji 16 vya Mwanavala, Imalilosongwe, Warumba, Igulunya, Vikai, Ikunda, Ihuta, Iwalanje, Magigiwa, Mkuya, Mahango, Nyamakuyu, Ukwavila, Mvunguni, Isimike na Ruanze vitaondolewa kupisha shughuli za hifadhi. Kati ya 38 kuna hivyo ambavyo vinaondoka.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alichosema, alisema kwa idadi ya vijiji lakini kuna vijiji ambavyo sehemu yake ya vitongoji vinaondoka kwa maana ya kwamba havijaathiriwa na hifadhi na sehemu ambayo inaingia kwenye hifadhi yenyewe itabidi waondolewe. Kwa hiyo, vimewekwa kwa maana vijiji ni vitano, lakini vingine ni sehemu ya vitongoji ambayo vinabaki kwenye hifadhi. Pori la Swagaswaga ameshalizungumzia sitaki kulirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye eneo ambalo limeleta changamoto kubwa kwa Wabunge wote wamelizungumza.

Kwanza naomba nikiri wazi tu kwamba mradi huu siyo mradi wa leo, mradi ulianza mwaka 2016 kwa maana ya kuanza mchakato. Mwaka 2018 ndio *discussion* zikaanza na wenzetu wa *World Bank,* mwaka 2021 wakakubali ku–*finance* na mradi huu uli–*appear* kwenye bajeti ya mwaka 2020/2021, ume–*appear* kwenye Bajeti ya 2021/2022 na sasa 2022/2023 ndio tumeanza kuutekeleza. Lakini mradi huo wakati wa

makubaliano ulivyokuwa vijiji vilikuwa vimepangwa vilikuwa ni 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Kamati ninawashukuru walipiga kelele sana katika hili wakasema haiwezekani mnapeleka kwenye miundombinu pesa nyingi na nini tunataka vijiji viongezwe. Wizara ikaenda ikakaa, tukafanya mawasiliano na wenzetu ratiba zao kidogo zikawa haziko sawa sawa kwa sababu huwezi kufanya mabadiliko katika mkataba ambao mmeingia na *World Bank* bila kukaa nao na kuridhia. Lakini tuliangalia ndani ya mkataba ulivyokuwa na kwa sababu tulikuwa na ule mradi wa kuimarisha suala la upimaji kulikuwa na pesa ilikuwa imetengwa kwa ajili ya kununua ramani. Sasa mradi huu kama unafanya maana yake huhitaji kununua ramani, unaweza ukatengeneza mwenyewe. Tukahamisha zile pesa tukaenda kuongeza vikawa vijiji 250 suala ambalo tulitoa taarifa na walikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waheshimiwa Wabunge naomba niwaambie, tumekaa miaka yote ya uhuru ambayo tunaizungumza vijiji 12,000 tunavyo 319 sasa ni 318 baada ya kijiji kimoja kuondoka. Lakini vijiji zaidi ya 10,000 vimepimwa na vina vyeti; vyenye mpango wa matumizi ni 2,675 kwa nini ni vichache? Kwa sababu hakuna miundombinu ya kurahisha upimaji na hiki kinachotakiwa kufanyika kinafanyika *once and for all* maana yake ni kwamba ukishasimika miundombinu ile ya upimaji, ukarahishisha ile *distance* ya upimaji kutoka kwenye kilometa 90 zikwa kilometa 20, 25 kasi ya kupima itaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kuongeza kasi ya kupima hata ule uzalishaji wa viwanja, uzalishaji wa kupanga matumizi ya ardhi utakuwa mkubwa kwa sababu muda utakuwa ni mfupi na gharama itakuwa ni ndogo. Tukisema tuhamishe pesa tupeleke tukapime leo, bado kasi itakuwa ni ile ile ni ndogo utapeleka pesa lakini huna nyenzo za ku-

*speed up* kazi yako. Bado utapima vijiji 50, utapima vijiji sijui vingapi kwa mwaka ambayo haifadhiliwi pia.

Kwa hiyo, kinachofanyika ndani ya Wizara ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu ya uhakika ambayo haitaturudisha nyuma kwenye kasi, ukishaiweka maana yake sasa ni kazi ya kubanana kila mwaka hatuitaji kwenda kuweka miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo zile *points* ambazo zinatumika katika suala zima la upimaji ambazo zilikuwa tatu tu, sasa hivi tunaenda kuweka nyingine 30 na mradi unaweka 22 tunakwenda kuwa na kama 25 ambazo zile zinakurahishia katika kazi ya upimaji. Ukishaweka zile ndugu zangu kazi itakayobaki sasa kufanyika ni kazi ya kupima tu uwandani hata kama watafanya usiku na mchana, lakini wana uhakika na nyezo zile wanazozitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili tutapeleka pesa ndio, lakini wana uwezo gani? Hawana vitendea kazi, zile mashine za kupimia za kileo, wanahangaika na *total station,* wanahangaika sijui na vitu gani, ambayo hayawezi kufanya kazi ile inayokusudiwa na lengo letu tupime vijiji vingi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia pia tuna Dar es Salaam na Dodoma peke yake ambapo sasa tumewekea Mfumo wa *ILMIS,* tunakwenda kuweka Mfumo wa *ILMIS* kwa nchi nzima katika mikoa yote na ile inaweza kurahisisha sasa wale watendajii wanaokwenda kutumia hiyo mifumo hawana huo uelewa wa kuweza kuingia kwenye mfumo na kufanya kazi ile na ndio maana sasa hivi tuna timu ya wataalamu ambayo inahakikisha kwamba inaweka mfumo vizuri ina-*clear data* zote, halafu tunakwenda kusimika mifumo katika kila mikoa. Mifumo ile itatusaidia kuongeza kasi ya upimaji, kuongeza kasi ya upangaji, lakini kutunza kumbukumbu za kila mmiliki wa ardhi kiasi kwamba hatuwezi

kuwa tena na kelele za *double allocation,* hatuwezi kuwa na kelele za upandanaji wa ramani hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kufanya *data conversion* limefanyika kwa kiasi kikubwa 100% ramani za mipango miji pamoja na ile ambayo inakwenda kwenye ramani za upimaji wa ardhi, sasa usipokuwa na hiyo huwezi kwenda.

Waheshimiwa Wabunge, tunaheshimu kile mnachokizungumza, wala hakuna ambaye hakiheshimu na ndio muelekeo tunaotaka sisi Watanzania wetu waweze kufikiwa, lakini tutaenda kwa kusuasua mpaka lini? Mimi nadhani hili mkiipa nafasi Serikali, halafu mkaja kuihoji hapa itakuwa ni vizuri zaidi, lakini ile dharura mnayoisema tunasahau kwamba hii ni fedha za kideni, kuna *fluctuation* ya *currency* na mpaka tunapoongea sasa hivi hizo dola mnazozisema hazipo, zimeshaliwa na mfumuko wa bei, kwa hiyo sio kwamba ni *cash* imewekwa ya dharura kwamba labda tutajisikia kama Wizara sasa tumepungukiwa tuchukue Hapana. Ile imewekwa kwa sababu kuu ya kuangalia mabadiliko ya *currency* zetu kwa maana ya *inflation* ambayo inakuwepo. Kwa hiyo, ni vitu ambavyo siyo kwamba tunaila sisi, na ukienda leo pesa imeingia toka mwaka jana jinsi ilivyokuja, ukienda sasa hivi siyo shilingi bilioni 345 tunazozisema leo, zimeshashuka kwa sababu siyo tena dola za Kimarekani milioni 150 kwa sababu ya suala la kibenki pia, kwa hiyo, ile siyo dharura ya kwamba inakwenda mfukoni kwa Waziri au kwa nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala haya niongelee suala zima la shamba lile la *DDC* la Mlolo Mheshimiwa Halima amesema. Mheshimiwa Halima wewe ni wakili, wewe ni wakili msomi na hili unalijua. Hivi kisheria unapokuwa na umiliki wa ardhi unaweza ukaukataa katika njia ipi? Una nyaraka ndio makaratasi sawa, lakini mwenye umiliki halali ana hati yake toka mwaka 1998 na bahati nzuri Mheshimiwa Gwajima leo

hayuko hapa, wameshafanya vikao zaidi ya mara tatu wakishirikiana na wale *DDC* wenyewe pamoja na Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Dar es Salaam, walianzia shilingi 8,000 kwa *square meter* wananchi wakagoma, wakaja 6,000 wakagoma, wamekwenda kushuka kwa makubaliano wenyewe mpaka shilingi 4,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Halima unalolizungumza wale watu hawatalipa wasipimiwe ndio maana yake ile ardhi hawana faida nayo, hawawezi kuitumia mahala popote. Lengo la Serikali ni kuhakikisha wanamwezesha anapata hati na anakuwa mmiliki halali sio sasa leo unaambiwa ya *DDC,* kesho unatolewa na hayo hayo yako kule Chasimba Chachui.

Mheshimiwa Halima wananchi wamevamia maeneo lakini mtu tayari ana hukumu ya mahakama anatakiwa awaondoe, hasa katika kuwaondoa Serikali ime–*intervene* ikasema hebu tukae mezani, basi ninyi mmeshavamia hebu mrudishieni huyu hela yake ya ardhi aweze kuchukua ardhi nyingine na ninyi mmilikishwe muweze kutumia ardhi zile kisheria na kuweza kufanya kile ambacho kinaweza kuwasaidia katika maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuwaombe wananchi wetu kwanza wasivamie maeneo, kama wanataka kujenga wajenge maeneo kwa kufuata taratibu na kwa kutumia mamlaka za upangaji, asiingie kwenye eneo eti ni shamba limekuwa pori kwa muda mrefu halafu akasema kwamba hili sasa mwenyewe hayupo mimi naingia, tutakuwa tunafanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Kitandula namshukuru kwa hoja yake ambayo ilikuwa *supported* pia na Mwenyekiti wangu wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara tunapokea kile ambacho kimekuja kwa maana ya *notice* zinapokuja na kama zina kila ushahidi hamna tatizo. Sasa unapokuja shamba limepewa *notice* sawa muda umetosha anatakiwa kunyang'anywa, lakini hati yake iko kwenye benki. Sasa lazima taratibu nyingine za kifedha zifanyike, na huyu bahati mbaya zaidi amekopa benki ya nje na ndio maana kama mtakumbuka miaka mitatu iliyopita tulibadilisha sheria hapa kwamba ardhi ya Tanzania kama unataka kukopa ukope ndani ya nchi na ukaendeleze hapa hapa ndani ya nchi, kwa sababu tumekuta wengi walikuwa wamekopa zamani kwa kutumia mashamba hayo hayo na hawayaendelezi nawamekopa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pale tulikuwa tunaweka dhamana mbaya kwa Tanzania yetu kwamba ardhi yetu tunayo kubwa, lakini kwa sehemu tayari imeshawekwa dhamana nje ya nchi. Akishindwa kulipa huyo mtu anakuja na hati yake anadai ardhi yake, huwezi kukataa. Tukabdilisha sheria hapa nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mlisaidia tulibadilisha sheria.

Kwa hiyo, mimi niwaombe tu Mheshimiwa Kitandula kwa sababu masuala mengine lazima yafate taratibu, tutalifuata tu kama ambavyo lilivyo na tutafikia maamuzi na Mheshimiwa Rais sasa hivi ukimplekea hati za kufuta wala haichukui muda, amefuta amshamba zaidi ya 11 Morogoro na wakarudishiwa wananchi pale kawa ajili ya kupanga matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hilo tunasema likishakamilika Mheshimiwa Rais hana neno na sisi kama Wizara, mimi kama mshauri nitapeleka kwa ajili ya kumshauri sasa afute ili ipangiwe matumizi mengine. Kwa hiyo, niwaombe tu kwamba maeneo yote hayo ambayo mnayazungumzia kwamba pengine mlishaomba yafutwe lakini hayajafanyika ni taratibu tu zikikamilka tunafuta.

Changamoto tunayoipata tukiwarudishia kwenye Halmashauri/Mamlaka za Upangaji mnataka kupima viwanja vyote, mnasahau kwamba tunahitaji kuwa na mashamba. Kuna maeneo mengine hayatakiwi kuendelezwa *I mean* kurudishiwa ukapanga viwanja, bado lilikuwa ni shamba limeshindwa kuendelezwa na halijaharibiwa mle ndani kwa maana watu wameweka miundombinu ya kudumu labda majengo bado unaweza ukalitumia kama shamba na kwa mjini pia *urban farming* inakubalika heka tatu unalima. Sasa tutajikuta mjini kote tunajaza viwanja, viwanja halafu mashamba yanakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mahali pengine pia tukiwaletea kwa ajili ya kufanya mpango wa matumizi basi tuombe tu tuangalie kama kweli tunatoka kwenye shamba tunaingia kwenye mji au tunafanyaje, lakini lengo la Serikali, lengo la Wizara ni kuhakikisha haya yote tunayafanya katika utaratibu ambao ni mzuri na haumuumizi mtu yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambazo zimezungumzwa zingine tutazileta kwa maandishi kwa sababu zilikuwa ni hoja nyingi, lakini nirudie kwa kusema tunaheshimu michango yenu na bahati nzuri katika lile suala la mradi Kamati ya Bajeti pia ilishalichukua na walikuwa wanalifanyia kazi. Kwa hiyo, tuna imani ya kwamba kile tulichiokieleza na kama kutakuwa na changamoto nyingine yoyote katika suala zima hili tutaweza kuona tunafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chege naye aliongea kwa uchungu sana suala la Utege, naomba tu nimwambie ya kwamba, sisi tutakuwa tayari kwa wakati wowote kuweza kuona ni jinsi gani tunaweza kutatua matatizo hayo bila kuwa na shida yoyote. Lengo letu ni kumsikiliza mwananchi aseme anachokisema na Serikali itaeleza kwa nini inataka kutwaa eneo lile, ili wote tuwe katika *win-win situation* kwa sababu, hakuna anayetaka kumuumiza

mwenzie. Kwa hiyo, tukishamaliza hivyo maana yake mtu anapewa haki yake anayostahili na tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu ya kwamba kwa Wabunge wote changamoto zote mlizonazo tumezipokea. Kule tutakakotakiwa kufika tutafika, tutashirikiana na wenzetu wa mamlaka za upangaji kuhakikisha kwamba migogoro inatatuliwa. Hatuhitaji migogoro mipya, tunahitaji kumaliza iliyopo na kwa sababu tunaingia kwenye digitali, taarifa zote mtazipata kiganjani na haya ni mabadiliko makubwa chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Ardhi inakwenda kuwa Wizara wezeshi kikweli kweli na sio Wizara ya migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru mtoa hoja.

Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida Fungu 48 ukurasa wa 426 na kwenye kishkwambi ni ukurasa wa 426.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……..........................Sh. 10,708,759,671

**MWENYEKITI:** Hapa ndio kuna mshahara wa Mheshimiwa Waziri na kuna Waheshimiwa Wabunge takribani wanne ambao wanahitaji kupata ufafanuzi, tutaanza na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kweli sina lengo la kuzuia mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuwa nataka tu ufafanuzi katika mradi huu wa kuimarisha usalama wa milki za ardhi nchini kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba katika utekelezaji wa huu mradi unakwenda kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja pamoja na umilikishaji wa ardhi kwa wananchi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka kujua tu ni kwa kiasi gani Mheshimiwa amejipanga katika kipindi hiki cha mradi, *commitment* yake kwamba tunakwenda kuona matokeo hayo kwa haraka na kuona ile michoro ambayo inaenda kubadilishwa kutoka michoro migumu na kwenda kwenye michoro laini, sijui kama Kiswahili sahihi, maana Kiswahili kimekuwa kigumu siku hizi.

Sasa karibu michoro milioni moja ambayo tayari imeshatayarishwa na wenzetu wa ardhi, sasa nikiangalia ni *burden* kubwa, ni kazi kubwa, lakini kwa sababu amesema kwamba tunakwenda kubadilisha utaratibu mzima wa kidigitali na tunaenda kuweka ofisi zetu katika kila mkoa na hizi ofisi zitakuwa *equipped* na vyombo vya kidigitali na kuweza kuimarisha *communication*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka *commitment* yake Mheshimiwa Waziri, kwa haraka kiasi gani tutaona hayo matokeo katika kipindi cha mradi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi, tunaomba.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Soud kwa swali lake ambalo anahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu Serikali imejiandaa vizuri katika hili, jambo la kwanza ambalo nataka pengine mlifahamu kama Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kulikuwa na changamoto kubwa katika suala zima la upimaji. Unapokuwa huna ramani zile za msingi ambazo zinakuonesha maumbile ya ardhi yako ya nchi kwamba wapi kuna mabonde kwa maana ya zile kontua na mambo mengine ambayo yapo, kama huna huwezi kufanya kazi yako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa katika huu mradi tunakwenda kuandaa zile ramani za msingi ambazo tulikuwa tunapata kutoka nje ya nchi, kwa mfano *South Africa,* Nairobi, Kenya, kwa gharama kubwa sana na hata kwenye huu mradi ilikuwa imewekwa kama bilioni 11 kwa ajili ya ramani za msingi, lakini kwa sababu tutalifanya wenyewe

hapa, maana yake ile pesa tumei-*save* kwa maana ya kwamba tunaenda kufanya kazi nyingine, lakini kikubwa ambacho nataka kusema ni kwamba unapokuwa umeandaa ramani za msingi, unakuja kuweka vile vituo kwa ajili ya upimaji. Sasa hivi nimeeleza wakati naelezea pale, tulikuwa tunapata tabu kwa kutumia huo upimaji wa mwendo mkubwa sana na ufanisi unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapokwenda kuweka zile *continuous operated reference stations* zitakuwa karibu karibu na kuongeza ile kasi ya upimaji, kwa maana ukitaka kupima leo hapa viwanja 100 unaweza ukavipima ndani ya muda mfupi, lakini kwa teknolojia tuliyonayo sasa viwanja 100 unaweza ukapima kwa mwaka mzima au miaka miwili.

Sasa hii teknolojia tunayokwenda kuiweka sasa inakwenda kutusaidia kuongeza ile kasi na huu mradi utaokoa fedha nyingi sana ambazo tumekuwa tukizitoa katika Halmashauri zetu au kwenye Wizara ya kila leo na kuweka bajeti ya kupima ambazo gharama zinakuwa ni kubwa. Sasa hatutakuwa na hiyo kwa sababu *post* zote zipo, vifaa vitanunuliwa, kazi itafanyika kwa kasi.

Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa nasema kwamba Serikali imejiandaa vizuri na kujenga pia kanzidata za kijiografia ambayo inatusaidia zaidi, lakini kujenga uwezo kwa Watanzania, na kwa sababu tumetoka kwenye analogia tunaingia kwenye digitali, Watanzania hawa wanahitaji *capacity building,* lazima wafundishwe, huwezi kuweka mfumo katika eneo halafu unaowapelekea hawawezi. Unapeleka mfumo kwa watumishi ambao wako kwenye chumba kimoja, watumishi wako saba, halafu tunasema ni ofisi. Kwa hiyo, ni lazima wawekewe pia ofisi ambazo zitaweza hata kuhimili hata vile vifaa vya ki-TEHAMA vinavyowekwa mle na wao wenyewe pia kuweza kufanya kazi kwa uhuru kama Watanzania.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ameridhika, ahsante tunaendelea. Namuita Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, lakini ameridhika naye, ame-*withdraw,* kwa hiyo tunaendelea.

Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi amehitaji kupata ufafanuzi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nasimama kwa unyenyekevu mkubwa kwa niaba ya Watanzania wote ambao wanaenda kulipa mkopo huu, lakini pia nasimama kwa unyenyekevu mkubwa kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais katika kutafuta fedha za maendeleo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama na hoja yangu ni ya kisera na mahsusi kwenye eneo hili la matumizi ya fedha za mradi huu ambazo zimekopwa Benki ya Dunia shilingi bilioni 345. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata ufafanuzi wa kuniridhisha na wa kuwaridhisha Watanzania hasa wananchi wa Mlimba ninakwenda kushika shilingi ya mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayozungumzwa hapa fedha hizi ni mkopo na mkopo lazima uwe na tija. Naomba nitoe mfano, Serikali ilipata mkopo wa Benki ya Dunia kwenye ule mradi wa UVIKO, pamoja na masharti magumu lakini Mheshimiwa Rais aliweza kuwa mbunifu, akaachana na maelekezo ya mkopo, akawaeleza changamoto za Watanzania sio kununua *sanitizer,* changamoto za Watanzania sio kununua vifaatiba, changamoto za Watanzania wanafunzi wanamsomgamano kwenye madarasa, vituo vya afya hakuna, huduma za afya zinakuwa sio nzuri. Mheshimiwa Rais akaelekeza zile fedha, leo hii Watanzania wanaona vituo vya afya vimejengwa, wanaona

hospitali zinafanya kazi vizuri, lakini wanashuhudia pia shule watoto wanakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachoshindikana kwenye mkopo huu, kwa sababu mkopo ule ulikuwa wa Benki ya Dunia na huu pia ni mkopo wa Benki ya Dunia, kinachoshindikana hapa kwenye mkopo huu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa kina.

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha na Mheshimiwa Waziri amesikia. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa hoja yake na kuweza kulinganisha fedha za UVIKO na hizi ambazo tunaziongela hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapolinganisha fedha ya UVIKO na kilichofanyika halafu ukalinganisha na kitu ambacho ni cha kitaalam kinachokwenda kumaliza migogoro hiyo, mkopo tumeukopa ndiyo, lakini kazi inayokwenda kufanyika itazalisha viwanja vingi na kuweza kupata *return* yake kutokana na kile kinachokwenda kufanyika, kwa sababu uwekezaji huu, mkopo huu sio wa mwaka mmoja. Uwekezaji huu unaokwenda kufanyika wa miundombinu unaweza kufanyika ndani ya mwaka mmoja/miwili unamaliza. Kitakachofuata kingine ni *generation of income* na kuongeza *tax base* katika kile unaachoenda kufanya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huwezi ukalinganisha mkopo ule wa kujenga madarasa, ni hitaji la wakati ule kwa sababu tu *Covid* unayoisema, kubanana kule kulikuwa kunaweza kufanya iwe *escalated* zaidi, lakini hiki tunasema kile ambacho kitatufanya kama Watanzania tuweze kufanya kazi yetu vizuri, tuweze kupima nchi yetu na tunasema

imepimwa kwa asilimia 25. Tutaweza kupima hiyo asilimia 75 kama hatuna nyenzo za kuweza kutufanya kazi yetu iwe ya *speed* zaidi. Kwa hiyo, tunawekeza katika mahali ambapo tunajua tutaweka miundombinu ambayo sasa itaufanya kwa miaka yote kazi yetu inakuwa ni kuzalisha viwanja, kazi yetu ni kupima vijiji, kazi yetu ni kuweka mipango ya matumizi ya ardhi kwa sababu tayari vitendea kazi tunavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe tu airudishe shilingi kwa sababu lengo la Serikali sio kumuumiza Mtanzania, lengo la Serikali ni kuhakikisha tunamhudumia Mtanzania, lengo la Serikali ni kukomesha au kumaliza migogoro iliyopo sasa, watu wanajenga hovyo kwa sababu ardhi haijapimwa, vijijini wanagombana kwa sababu ya ku-*scramble* kwenye matumizi ya ardhi na hata wale waliowekewa mpango wakati mwingine mfugaji anaenda kulisha mazao ya mkulima, lakini ana mpango wa matumizi kwenye maeneo, lakini ukiweza kuipima nchi yako yote, ukaweka matumizi hayo vizuri maana yake ni kwamba utakuwa umeondoa adha moja kwa moja badala ya kurudi kila siku unataka ufanye kitu kilekile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge arudishe shilingi kwa sababu tunachotaka kukifanya hapa ni kwa uendelevu wa sekta nzima, ni kwa kuondoa migogoro ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi naona amesimama, hujaridhika au umeridhika?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sijaridhishwa na ufafanuzi wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, hivyo basi naomba nichukue fursa hii nitoe hoja ili jambo hili lijadiliwe na Wabunge wenzangu kwa maslahi mapana ya Watanzania, ahsante.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Haya nilimuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tuanze tumsikilize.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana, nasimama hapa kwa niaba ya Serikali, lakini nasimama hapa pia kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya kisera na kisekta kwenye masuala yote ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imejadiliwa sana na Wabunge, Mheshimiwa Waziri alipokuja hapa amefanya hitimisho na ametoa maelezo ya kina kuhusu mradi ama progamu hii ambayo kwa nia njema ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika malengo yale yale ya kuhakikisha inapunguza migogoro, lakini kwa kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka katika kupima ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini, Mheshimiwa Rais aliona mkopo huo utumike kwa kazi hiyo fasaha na naomba niungane na Wabunge na naomba Wabunge wenzangu kwanza tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi hizo anazozifanya ndani ya nchi katika kuhakikisha sekta mbalimbali nchini zinatendewa haki ili kutoa huduma bora kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha amesema amekwishakutoa maelezo ya kina kwenye Kamati, lakini vilevile kwa sasa amekwishawasiliana na Kamati ya Bajeti, Kamati ya Bajeti nayo imeomba kupatiwa ufafanuzi wa kina kuhusu mradi huu ili Serikali na Bunge tuweze kuelewana na kuongea lugha moja yenye maslahi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili limeshafikia hapo, Serikali inaomba kwa muktadha wa majadiliano yenye afya kati ya Serikali na Bunge, Kanuni ya 124 ambayo imekuwa ikitumika mara zote kunapotokea mjadala wa namna hii ili kuwa na mukhtadha wa pamoja na kuhitimisha hiyo hoja kwa maslahi mapana ya wananchi, ninaomba niisome Kanuni hiyo ya 124(1); “Baada ya Bunge kuwa limekamilisha mjadala wa makadirio ya Wizara zote ndani ya siku sita kabla ya hotubaya Bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha wa makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unafuata.”

Mheshimia Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ninaona kuna umuhimu sasa Serikali na Bunge kwa pamoja kuzingatia maelezo ya Serikali, lakini maelezo ya Waheshimiwa Wabunge. Hoja hii sasa tukaimalize kwenye Kamati ya Bajeti kama inavyozungumzwa kwenye Kanuni ya 124. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Tusikilizane Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Tusikilizane Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ukibishana na Kiti utaweza kutolewa sasa hivi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sibishani na Kiti. Kanuni inasema nikisema Kuhusu Utaratibu unatakiwa unisikilize.

**MWENYEKITI:** Naomba tusikilizane. Mheshimiwa Halima Mdee naomba uketi.

Haya kuna Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa ajili ya kuchangia, nitamuita Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nakushukuru kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ukiliangalia inaonesha kwamba limepata uzito kwa pande zote mbili hasa baada ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa maelezo aliyoyazungumza sasa hivi kiasi kwamba kwa sababu Serikali inaona kuna haja ya kuliangalia suala hili upya kupitia Kamati yetu ya Bajeti basi mimi naona sasa tukubali tukitegemea kwamba kutakuwa na jambo litafanyika kwa faida ya wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu namfahamu Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, amekuwa ni mtu muadilifu na msikivu; Katibu Mkuu ambaye ameenda sasa hivi kwenye Wizara hii amekuwa ni mtu mwenye rekodi nzuri katika kushughulikia Wizara yake na kwa sababu jambo hili lilianza muda mrefu, labda ndio maana liliwapa kigugumizi kuamua mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ushauri wangu ni kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu na aliyetoa hoja kwamba, kwa sababu sasa limefikia mahali ambapo panaenda kuangaliwa zaidi, basi turidhie tukitegemea kwamba kwa sababu mchakato wa bajeti bado unaendelea na ndio maana kulifanyika mabadiliko, zamani ilikuwa unachangia mwisho unasema naunga mkono hoja na hakuna kinachobadilika, lakini kwa sasa baada ya kurekebisha sheria tunachangia na tunapoona kuna ugumu ina maana kuna jambo linaenda kuangaliwa tena.

Mimi niwaombe tufuate hayo kwa kuiheshimu pia sheria yetu tuliyoitunga sisi wenyewe inayotupa sisi Wabunge nafasi ya kusema hili liende hivi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Manyanya kwa ufafanuzi wako.

Kanuni ya 123(2), Katibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*............................Sh. 10,708,759,671
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 1,135,503,242
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*................................Sh. 1,163,509,192
Kifungu 1004 - *Management Information System Unit*.................................Sh. 1,610,604,898
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*.........................Sh. 535,811,346

Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*..............................................Sh. 609,440,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*..............................................Sh. 572,318,096
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*........................Sh. 576,284,000
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*............................Sh. 13,857,423,615
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*...............................Sh. 9,768,392,425
Kifungu 2003 - *Registration of Titles Unit*...............Sh. 986,300,039
Kifungu 2004 - *Valuation Department*..............Sh. 4,441,774,515
Kifungu 2005 - *Dar es Salaam Land Office*.......Sh. 1,494,273,989
Kifungu 2007 - *Dodoma Land Office*................Sh. 1,004,637,620
Kifungu 2008 - *Tabora Land Office*.......................Sh. 734,306,432
Kifungu 2009 - *Mwanza Land Office*....................Sh. 981,740,758
Kifungu 2010 - *Kilimanjaro Land Office*................Sh. 776,639,902
Kifungu 2011 - *Mtwara Land Office*......................Sh. 650,729,918
Kifungu 2012 - *Mbeya Land Office*.......................Sh. 893,637,375
Kifungu 2013 - *Simiyu Land Office*........................Sh. 631,300,783
Kifungu 2014 - *Arusha Land Office*.......................Sh. 804,860,828
Kifungu 2015 - *Geita Land Office*.........................Sh. 608,077,151
Kifungu 2016 - *Njombe Land Office*.....................Sh. 629,694,836
Kifungu 2017 - *Katavi Land Office*.......................Sh. 570,508,701
Kifungu 2018 - *Coastal Land Office*......................Sh. 808,270,782
Kifungu 2019 - *Iringa Land Office*.........................Sh. 608,756,347
Kifungu 2020 - *Kigoma Land Office*......................Sh. 661,386,381
Kifungu 2021 - *Lindi Land Office*..........................Sh. 622,513,809
Kifungu 2022 - *Mara Land Office*.........................Sh. 766,581,652
Kifungu 2023 - *Morogoro Land Office*..................Sh. 944,935,555
Kifungu 2024 - *Ruvuma Land Office*...................Sh. 700,105,215
Kifungu 2025 - *Shinyanga Land Office*.................Sh. 677,380,343
Kifungu 2026 - *Singida Land Office*......................Sh. 646,308,748
Kifungu 2027 - *Tanga Land Office*........................Sh. 870,465,150
Kifungu 2028 - *Kagera Land Office*......................Sh. 732,179,748
Kifungu 2029 - *Rukwa Land Office*.......................Sh. 526,067,780
Kifungu 2030 - *Songwe Land Office*.....................Sh. 571,247,345
Kifungu 2031 - *Manyara Land Office*...................Sh. 647,177,952

Kifungu 3001 - *Human Settlement Development Department*................................Sh. 8,964,654,035
Kifungu 3002 - *Real Estate Unit*..............................Sh. 360,889,346
Kifungu 3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit*................................Sh. 6,187,785,480

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Directorate of Corporate Services*......................................Sh. 2,166,738,080
Kifungu 1003 - *Procurement and Management Unit*..................................................Sh. 187,295,200
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*..........................Sh. 163,771,180
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*........................Sh. 340,175,300
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Management & Coordination Division*..........................................Sh. 776,432,500
Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance & Information*...............................Sh. 367,105,240
Kifungu 2003 - *Zonal Offices*.................................Sh. 791,110,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*............................Sh. 1,060,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*...................................Sh. 200,000,000
Kifungu 1004 - *Management Information System Unit*...............................................Sh. 4,206,000,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*.........................Sh. 200,000,000
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*...............................Sh. 68,826,000,000
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*..................................Sh. 7,634,645,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Directorate of Corporate Services*.........................................Sh. 103,000,000

Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Management & Coordination Division*.......................................Sh. 1,215,000,000
Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance & Information*.................................Sh. 92,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

**MBUNGE FULANI:** Ayayayaya, kabisa. Mmetisha, Mwenyekiti umetisha, Mwenyekiti shilingi zilikuwa nne, umetoa mbili, mnakimbia kivuli.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Namuita Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitawahoji na hapa ndio mahali pa kusema sasa.

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitatoa matangazo kidogo halafu nitasema neno kuhusiana na kilichokuwa kinaendelea.

Moja, kuna tangazo la Katibu wa Bunge hapa naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Nishati itaendesha semina kuhusu upatikanaji wa umeme na mradi wa uzalishaji na usambazaji wa umeme. Semina hii itafanyika siku ya Jumapili tarehe 28 Mei, 2023 kuanzia saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Waheshimiwa Wabunge wanakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kupata uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya upatikanaji, uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Kwa hiyo, kuna semina ya Jumamosi na ya Jumapili, zote za Nishati. *(Makofi)*

Pia kuna tangazo lingine la Katibu wa Bunge, naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itaendesha semina kuhusu uhifadhi na utangazaji utalii, semina hii itafanyika siku ya Jumatatu tarehe 29 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kupata uelewa wa masuala yahusuyo uhifadhi na utalii ili kusaidia kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi.

Kwa hiyo, Jumamosi, Jumapili; kisha Jumatatu Maliasili na Utalii.

Pia kuna matangazo ya wageni, wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla ambao ni chawa wa mama kutoka Mkoa wa Ruvuma hawa ni wageni wa Wabunge wote wa Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Lakini pia tuna wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango kutoka Taasisi ya Simama Tanzania ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Stephen Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati kutoka Kampuni ya Uuzaji na Uagizaji wa Magari Uingereza Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 32 wa Mheshimiwa Steven Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini ambao ni wanafunzi wa Vyuo Vikuu Jijini Dodoma kutoka Longido Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni washiriki wa Shindano la *Miss Central Zone* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia kuna wageni kumi wa Mheshimiwa Deodatus Mwanyika ambao ni Maafisa Elimu Kata kutoka Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Kundo Mathew ambao ni Madiwani wa kata zinazopakana na Hifadhi ya Serengeti kutoka Bariadi Mkoa wa Simiyu, ahsante. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Judith Kapinga ambaye ni mfanyakazi wa Chama cha Mawakili Tanganyika kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni viongozi Kata ya Uhambingeto kutoka Kilolo, Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Tunao wageni 44 wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni washindi wa Tuzo za Wanawake Wajasiriamali mwaka 2023 wakiambatana na wadhamani wao wakuu ambao ni Bodi ya Nafaka Tanzania pamoja na *TANAPA*. Hongereni sana washindi na karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke kutoka Kasulu, Mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni Madiwani wa Kata ya Kimambi kutoka Liwale, Mkoa wa Lindi, ahsante. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge letu kwa ajili ya mafunzo, kundi la kwanza ni wanafunzi 110 na walimu/walezi 15 kutoka Shule ya Awali na Msingi *St. Peter Clavert* kutoka Mkoa wa Morogoro, ahsante. *(Makofi)*

Wapo pia wanachama 55 wa Sisi Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo Maafisa wa Wizara ya Ardhi wanaoshiriki Maonesho ya Majuku yanayotekelezwa na Wizara hiyo katika viwanja vya Bunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho mwa siku yetu ya leo, tunaipongeza Serikali kupitia Wizara kwa bajeti yao, lakini tumewapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Tunaamini Serikali imepokea *feelings* za Wabunge, na hoja za msingi zilizotolewa hususan changamoto ambazo wanaziona na hivyo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi pia lile jambo liende kwenye Kamati ya Bajeti likachakatwe zaidi ili kuona maoni haya ya Wabunge yanaweza kuchukuliwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitoe rai kidogo kabla sijaendelea kusema, kiti kikisimama, ukiendelea kuzungumza utakuwa unajitafutia matatizo. Kwa hiyo, niwaombe na nitoe onyo kwa wale ambao wana desturi hiyo kwamba tuache kufanya hivyo kwa sababu ni Kanuni yetu na tumeipitisha wenyewe. Kama kuna jambo halikuwa kwenye utaratibu unakwenda kwenye utaratibu kwenye kanuni zetu tunafuata utaratibu wa Bunge letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimeona niseme kwa ajili ya ndugu zangu maana mara kwa mara nimeona kama vile wanataka kuzidi kwenye *level* ambayo wanatakiwa pengine wasifike.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.10 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 29 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*